

**UHAKIKI WA TAMTHILIA YA AMEZIDI KAMA  
KAZI YA KIUBWEGE**

**Na**

**FRED AKEYA MAGARE**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA  
BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI  
'MASTER OF ARTS'  
KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2002**

University of NAIROBI Library



0496800 4

## UNGAMO


TASNIFU HII NI KAZI YANGU BINAFSI NA HAIJATOLEWA KWA MAHITAJI YA SHAHADA KATIKA CHUO KIKUU KINGINE CHOCHOTE.




**WILFRED AKEYA MAGARE**

**(Mtahiniwa)**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii tulioteuliwa na chuo kikuu.



**DKT. MWENDA MBATIAH**



**NDG. TIMOTHY AREGE**

## **YALIYOMO**

UNGAMO.....	i
YALIYOMO.....	ii
TABARUKU.....	iv
SHUKRANI.....	v

## **SURA YA KWANZA**

1.1	UTANGULIZI.....	1
1.2	SOMO LA UTAFITI.....	4
1.3	MADHUMUNI YA UTAFITI.....	6
1.4	SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII.....	7
1.5	MIPAKA NA UPEO.....	8
1.6	NADHARIA TETE.....	8
1.7	YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI.....	9
1.8	MSINGI WA KINADHARIA.....	11
1.9	NJIA ZA UTAFITI.....	19
	TANBIHI.....	21

## **SURA YA PILI**

2.0	HISTORIA NA TANZU ZA DRAMA.....	23
2.1	UTANGULIZI.....	23
2.2	HISTORIA YA DRAMA.....	23
2.3	MAENDELEO YA TAMTHILIA YA KISWAHILI.....	23
2.4	TANZU ZA DRAMA.....	25
2.5	DRAMA YA KIUBWEGE.....	26
2.5.1	DHANA YA UBWEGE.....	26
2.5.2	HISTORIA NA MUKTADHA WA UBWEGE.....	27
2.5.3	DHANA NA SIFA ZA DRAMA YA KIUBWEGE.....	29
2.5.4	MIELEKEO YA DRAMA YA KIUBWEGE.....	31
2.5.5	DRAMA YA KIUBWEGE BARANI AFRIKA.....	33
2.6	HITIMISHO.....	33
	TANBIHI.....	34

## **SURA YA TATU**

3.1	UTANGULIZI.....	35
3.2	DHAMIRA YA TAMTHILIA.....	35
3.3	SUALA LA MUNGU.....	38
3.4	ELIMU NA MKENGEUKO.....	43
3.5	SUALA LA HISTORIA.....	51
3.6	HITIMISHO.....	54
	TANBIHI.....	55

## **SURA YA NNE**

4.1	UTANGULIZI.....	56
4.2	UHSIKA.....	56
4.3	MAZINGIRA.....	68
	4.3.1 PANGO.....	75
	4.3.2 UTUPU.....	80
4.4	MATUMIZI YA NYIMBO.....	82
4.5	MATUMIZI YA SAUTI, KICHEKO NA KILIO.....	87
4.6	LUGHA NA MAWASILIANO.....	92
4.7	PLOTI.....	95
4.8	HITIMISHO.....	97
	TANBIHI.....	98

## **SURA YA TANO**

5.1	UTANGULIZI.....	100
5.2	MAANA YA MAISHA.....	101
5.3	HITIMISHO.....	111
	TANBIHI.....	131

## **SURA YA SITA**

	<b>HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....</b>	<b>114</b>
6.1	HITIMISHO.....	114
6.2	MAPENDEKEZO.....	116
	TANBIHI.....	116
	MAREJELEO.....	117

## TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia mamangu mpendwa Mary Nyaboke Magare.

“Mama umeteseka, umesononeka na umeaibishwa kwa sababu ya malezi yako mema. Naomba usilie mama. Mtoto wangu Lilian aliyezaliwa tarehe kumi julai mwaka huu ningali niking’ang’ana na kazi hii naomba awe kitulizo cha roho yako. Nimempa jina ‘Nyaboke’ – Tuzo lako mama.” Hakuna tofauti kati ya kilio na kicheko, vyote ni makelele.

## SHUKRANI

Kazi hii imetimilika kutokana na ukarimu, juhudi na hisani za watu mbalimbali. Ni muhali kuwataja wote hapa kwa vile ni wengi mno. Naomba kuwataja baadhi yao kwa misaada, wema na uadilifu wao. Wale ambao sitawataja tafadhali mnisamehe, kwa vile hata wao walinifaa pakubwa.

Shukrani za kipekee nazimimina kwa wasimamizi wangu Dkt. Mwenda Mbatiah na Ndugu Timothy Arege kwa kuniongoza na kunielekeza wakati nilipohitaji msaada wao. Ushauri wao uliniwezesha kutia shime na kujizatiti kuikamilisha tasnifu hii.

Aidha nawashukuru wahadhiri wengine katika idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika kwa mawaidha yao. Hawa ni Dkt. Kithaka wa Mberia ambaye ni mwenyekiti wa Idara, Dkt. Kineene wa Mutiso, Ndugu Richard Mgullu, Dkt. John Hamu Habwe, Ndugu James Michira, Prof. Mohamed Abdulaziz, Ndugu Basilo Mungania, Dkt. Marete, Ndugu Manyora, Ndugu Akida, Dkt. Eshun, Ndugu Margaret Njuguna, Ndugu Bi. Kiranga na Dkt. K. W. Wamitila.

Sitawasahau mke wangu mpendwa Pamela Kerubo na mtoto wangu Lilian Nyaboke kwa mapenzi yao ya dhati. Uvumilivu wao ulinipa moyo wa kusoma kwa bidii na kuikamilisha shahada yangu ya uzamili.

Hali kadhalika, nawakabidhi shukrani maalumu wazazi wangu Thomas Magare na Mary Nyaboke Magare kwa juhudi na fadhila zao kwangu. Neema za Maulana naomba zimiminike kwenu nyote kwa kunilea vyema.

Sina budi kuwanyooshea mkono wa ahsante ndugu zangu Rebecca Kemunto, Jane Nyabate, Richard Momanyi, Josephine Kerubo, Mellen Bonareri, Innocent Ng'wono, Dennis, Benjamin, Stella, Jackline Kwamboka, Geoffrey Marube na mpwa wangu mpendwa Evans Ng'wono Nyariki kwa kunitakia na kuniombea mema masomoni na maishani.

Pia siwezi kusahau kuwashukuru jamaa na marafiki kwa hisani zao. Hawa ni Hon. Tola Kofa, Bw. na Bi. Jackson Mose Matimo, shemeji Dismas Mogaka, Ronald, Hilder, Rose, Alice, Thomas Koroso Okenye, John Nyariki Osiko, Bw. na Bi. Obadiah pamoja na watoto wao wakiwemo Elijah, Mary, Job, Callen na Stella. Mwalimu Nicodemus Magara na walimu wote

wa shule ya upili ya Kegochi, Irene Moraa, Gladys Nyaboke, Carolyne Bochaberi, The 3 Akeyas, Tom Mogusu, James Gichuru Ariba, Eddah Wanja, Charles Mose na Henry Nyang'au.

Kadhalika nawashukuru na kuwahongera wanafunzi wenzangu tuliong'oa nanga pamoja katika safari ya kuukweya mlima mrefu wa usomi. Hawa ni David Ondeyo Ombegeera, Sammy Kamau, Peter Muhati, Amadi kwa Adziaya, Sammy Gakero, George Nyandoro na Leonard Maloba. Ushauri na mijadala tuliyoifanya ilininufaisha pakubwa. Aidha, wanafunzi wa uzamili wa mwaka wa kwanza wakiwemo Goefred Osoro Mogere, Priscah Jerono, Grace, Omwenga Makori, Bwire na Nzuki sitaweza kuwasahau kwa misaada na wema wao.

Hatimaye namshukuru Bi. Maureen Atelo kwa kuichapa kazi hii kwa ustadi. Kwake yeye na kundi lake la DownWorld Communications (DWC) wakiwemo Samuel Siringi, Davies Obino, Isaiah Obino na Dennis Marube, nasema ahsante sana kwa ukarimu wao.

Kwenu nyote ambao nimewataja na wale ambao sikuweza kuwataja, nawatakia mema maishani.

Ahsante.

# SURA YA KWANZA

## 1.1 UTANGULIZI

Tamthilia ni mojawapo ya tanzu tatu kuu za Fasihi andishi. Istilahi hii imetokana na kitendo “mithilisha” yaani fananisha. Tamthilia basi ni maigizo ya matukio au visa fulani kwa uhalisi wake kwa ajili ya kuyasawiri maudhui au maelezo fulani.

Dhana ya tamthilia imetolewa ufafanuzi na wasomi na wataalamu mbalimbali:

*Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (1981: 272) inaeleza kuwa:

Tamthilia ni utungo wa kisanaa ambao huweka wazo fulani katika matendo na mazungumzo.

Naye Wafula (1999:2) anasema:

Drama ni somo linalohusu uigizaji wa hali fulani iwe ni vitendo au tabia au hisia za binadamu kwa kufuata taratibu maalum. Tamthilia ni ule mtungo hasa ulioandikwa kwa ajili ya kuigizwa.

Clark (Katika Killam 1973: 19) anatumia neno drama kwa maana ya uigizaji wa hali ya juu wa kitendo fulani muhimu kwa watu; huku elementi za uwasilishaji zikiwa uzungumzi, muziki, nyimbo na pia dansi. (Tafsiri yetu).

Kwa upande wake, Penina Muhando Mlama (1983:203)<sup>1</sup> anaona tamthilia kama;

... ule utungo ambao unaweza kuwa umeandikwa au haukuandikwa, ambao unaliweka wazo linalotakiwa kuwasilishwa katika umbo la tukio la kuliwezesha kutendeka mbele ya hadhira.

Mlama (1983:203), anaendelea kufafanua kuwa tamthilia ni sawa na michezo ya kuigiza. Anashikilia kwamba, tamthilia ni utungo wa drama ambayo ni aina moja ya maandishi ya sanaa ya maonyesho. Msimamo wake ni kuwa, sanaa ya maonyesho ni ile sanaa ambayo huwasilisha moja kwa moja tukio fulani kwa kufuata usanii wa kiutendaji.



Katika semina ya SWAHILI LITERARY TERMINOLOGY iliyofanyika katika chuo kikuu cha Dar es Salaam mnamo Mei 28 mpaka Juni 8, 1979, ilikubaliwa kuwa;

Drama ni tajiriba, kweli au inayofikiwa  
ambayo huletwa au hukusudiwa  
kuletwa na kuihuishwa jukwaani.

Drama ni somo juu ya tungo (tamthilia) ambazo husaidia kuweka au kuwasilisha wazo au mawazo fulani mbele ya hadhira. Hussein (1983: 202) anafafanua kuwa drama inaweza kuwa imeandikwa au haikuandikwa. Drama ambayo imeandikwa, kwa maoni yake huishia kwenye fasihi, ilhali ile ambayo huenda jukwaani moja kwa moja bila kuandikwa, huishia kwenye ulimwengu wa jukwaa.

Uandishi wa drama unabainisha mikondo mingi tangu enzi za Aristotle (384 – 322 k.k), ambaye alichangia pakubwa drama kwa kutoa vipengele vya uandishi wa tamthilia. Alipendekeza kuwa tamthilia iwe na sehemu tatu muhimu. Utangulizi (prologue), kitendo chenyewe (exode) na kimalizio (epilogue). Kila sehemu ina sifa zake bainishi (tazama sura ya pili). Kitabu chake *The Poetics* kilisaidia kutoa mwelekeo wake juu ya uandishi wa tamthilia. Aristotle ameathiri sana uandishi wa tamthilia ingawa vigezo vyake vinajikita zaidi katika tanzia ya Kigiriki mfano tamthilia *Mfalme Edipode* tafsiri yake Mushi, S. 1971 – (Sofokile 496-406 k.k).

Tasnifu hii imejikita katika mkondo huu wa uandishi, ubwege, kwa kuihakiki tamthilia ya *Amezidi* ya Said Ahmed Mohamed.

Uandishi wa tamthilia umepitia historia ndefu kama asemavyo Lewis (1962:1):

Historia ya drama ni historia ya binadamu  
kwa sababu jukwaa la drama hushughulikia  
maisha na migogoro kati ya binadamu na  
ulimwengu anamoishi. (Tafsiri yetu)

Mtindo wa tamthilia zetu umetokana na ule wa fasihi ya Kiingereza ambayo ililetwa kwetu na elimu ya kikoloni. Maandishi ya Shakespeare ni mfano mzuri wa fasihi hii. Tamthilia hugawanywa katika matendo na kila tendo huwa na maonyesho kadha. Kila onyesho huwa na waigizaji ambao hutekeleza majukumu maalum. Hata hivyo tukumbuke kuwa sio tamthilia zote hufuata mtindo huu. Wasanii wengine hawazingatii hali ya kuitaja migawanyiko, yaani matendo na maonyesho. Wengine hutumia maonyesho pekee. Mfano mzuri wa mitindo hii ni ule wa Katalambulla katika tamthilia yake iitwayo *Mirathi* na Said. Ahmed. Mohamed katika tamthilia yake *Amezidi*.

Tofauti mojawapo kubwa kati ya tamthilia na tanzu nyingine za fasihi ni kwamba tamthilia huwashirikisha wahusika katika mazungumzo na au vitendo ambavyo hubainisha mgogoro ulioko. Isitoshe, tamthilia huidhihirisha hali ilivyo kwa uwazi zaidi mbele ya hadhira na kwa muda mfupi maudhui yote huhitimishwa. Kinyume na riwaya au ushairi, tamthilia basi ina uwezo wa kuyatongoa kwa urahisi maudhui yaliyomo kwa dakika au masaa machache tu.

Baadhi ya waandishi wa tamthilia huwaza jinsi kazi zao zingebainishwa jukwaani na ndiposa wengine husisitiza mpangilio maalum wa maleba na au mapambo jukwaani. Hii ni kwa sababu, yote hayo huendeleza hali ya usawiri wa yanayopitishwa. Ebrahim Hussein katika *Kinjeketile* amependekeza mpangilio wa uigizaji wa tamthilia hii jukwaani.

Mtu aisomapo tamthilia yoyote, humbidi aiandae katika jukwaa la bongo lake na kujaribu kuwahisi wahusika wakiubainisha na kuutatua au kujaribu kuutatua mgogoro au tukio ambavyo ndivyo viini hasa vya tamthilia nyingi. *Amezidi*, ni miongoni mwa tamthilia za kisasa na imetajwa na wasomi na wahakiki hapa na pale kuwa tamthilia tata na ambayo si rahisi kuelewa.

Said Ahmed Mohamed, ni mwandishi stadi na mchango wake kwa fasihi ya Kiswahili ni mkubwa. Ametamba mno katika tanzu zote za fasihi. Baadhi ya kazi zake ni *Sikate Tamaa*, *Kina Cha Maisha*, (Ushairi), *Kiza Katika Nuru*, *Asali Chungu*, *Utengano*, *Dunia Mti Mkavu* (riwaya), *Kivuli Kinaishi*, *Pungwa*, *Kitumbua Kimeingia Mchanga*, na *Amezidi* (tamthilia).

Mohamed, katika “Kupatana na Riwaya Zangu” (1981), anatudokezea itikadi yake. Anaamini kwamba:

Lazima mwandishi awe na mtazamo  
madhubuti juu ya jambo au mambo  
mbalimbali ya maisha. Kwa mfano, suala  
la umaskini, unyonge na uonevu kati ya  
mwanadamu na mwanadamu analionaje mwandishi...

Anaendelea kusema kwamba:

Na mwandishi anapaswa kufuata  
itikadi ipi? Bila shaka ile itikadi inayotetea  
wengi; wazee na ndugu zetu ambao maisha  
yao yafanana na maisha ya wanyama ...

Huyu ni mwandishi ambaye ameishi, amesoma, na kufanya kazi barani Afrika na nchi za ng'ambo. Tumemshughulikia kwa vile ni mmoja kati ya waandishi wenye tajriba na mielekeo thabiti katika uandishi wa tamthilia na fasihi kwa ujumla.

## 1.2 TATIZO LA UTAFITI

Utafiti wetu, unajikita katika tamthilia ya *Amezidi*, iliyoandikwa na Said Ahmed Mohamed. Tutaihakiki na kuinakidi tukizingatia kipengee cha ubwege.

Tatizo hasa la utafiti wetu, ni kuchunguza ni kwa kiasi gani *Amezidi* ni kazi ya kiubwege na ni kiasi gani si ya kiubwege kwa kuzingatia yaliyomo na fani.

Tatizo hili ni muhimu kwa vile mwandishi wa *Amezidi* ametumia wahusika ambao wanakatisha tamaa. Kwa kiasi kikubwa wanalingana na wahusika wa tamthilia za Beckett na Ionesco ambao ni waandishi sifika katika tapo la ubwege. Wahusika hawa hawatendi lolote la maana ila kuzungumza tu. Aidha lugha wanayotumia hutatiza mawasiliano kwa kuzunguka suala moja. Kazi inayosawiri vipengele kama hivi inahitaji kufanyiwa utafiti wa kina ili kubainisha mwelekeo wa mwandishi wake.

Somo hili pia linafaa kwa sababu ubwege ni tapo ambalo halijashika mizizi katika uandishi wa tamthilia ya Kiswahili na hivyo utafiti wa aina hii ni muhimu.

Ubwege ni ile hali ya kutokuwa na wiano, ukosefu wa muwala au kutokuwa na lengo chambilecho Eugene Ionesco<sup>3</sup>.

Tamthilia ya Kibwege ilizuka kwanza Ulaya hasa Paris baada ya Vita vya Pili Vikuu vya Dunia. Baadhi ya wasanii muhimu ambao huhusishwa na ubwege ni Samwel Beckett (*Waiting for Godot*) na Eugene Ionesco kupitia kazi kama *The Chairs*, *The Lesson*, *Rhinoceros*, *The Killer*, na *The Bald Prima Donna*. Barani Afrika, Robert Serumaga (*Majangwa*, *The Elephant*), na Athol Fugard (*The Coat*, *The Island*, *No Good Friday*, *The Blood Knot*, *Sizwe Bansi is Dead*, *Nongogo*), ni mfano wa waandishi wa tamthilia za kibwege.

Alembi (2000: 5) anaeleza kwamba;

... dhana ya ubwege ilitumiwa kwanza na Camus  
kuashiria tofauti kati ya fikira za binadamu na  
matarajio yake, na dunia katili. (Tafsiri yetu)

Mnamo 1942, Albert Camus alikuwa tayari ameanza kuuliza kwa nini binadamu aendelee kuishi ilhali dunia ilikuwa haina maana tena. Katika makala yake "*The Myth of Sisyphus*"<sup>4</sup>, Camus ameeleza namna ambavyo ukosefu wa matumaini ulisababisha hali ya ubwege. Hii ndiyo hali ambayo ilitawala katika kipindi cha na baada ya Vita vya Pili Vikuu vya Dunia. Wasanii wa kibwege licha ya kuonyesha ukosefu wa mantiki ya maisha, hutupilia mbali mbinu zenye mantiki na mawazo yanayofululiza katika uwasilishaji wa kazi zao. Kazi zao ni muungano baina ya imani ya kifalsafa na muundo wa kisanii.

Je, *Amezidi* imefaulu vipi kuafikiana na tapo la ubwege? Uchunguzi wetu utamulika swala hili kwa kuhusisha vipengele vya tamthilia hii na muktadha wa tamthilia za kibwege.

Esslin Martin (1961:5) akimnukuu Ionesco, anasema kuwa ubwege ni kile ambacho kimekosa nia – kimetengwa kutoka kwa imani za kidini, tabia za kiungu na mizizi ya kiakili na mawazo. Binadamu amepotea; vitendo vyake vyote ni vya kijinga, ubwege, havina maana.

Kuhusu tamthilia za kiubwege, Esslin (1961:3-4) anaeleza kuwa ikiwa tamthilia ni lazima iwe na hadithi inayofululiza vizuri, tamthilia za kiubwege huwa hazina hadithi au ploti inayoweza kuelezewa kikamilifu; kama hadithi nzuri huamuliwa kwa usawiri na umotishaji mzuri wa wahusika wake, hizi mara nyingi hukosa wahusika wa kutambulika vyema na badala yake hubainisha wahusika batili tu. Kama tamthilia ya kawaida inapaswa kuwa na maudhui pevu, hizi hazina muwala wa maudhui. Tamthilia za kibwege huwa na ndoto nyingi bila kumulika hali ya maisha kiuhalisia – tamthilia za kiubwege hubainisha utengano, upweke wa mazungumzo.

Kwa ujumla, tamthilia za kibwege huvuruga taratibu za kijadi za uandishi wa tamthilia. Vigezo vilivyozoeleka katika uandishi wa tamthilia tangu enzi za Kiaristotle, huvunjwa katika muktadha wa kiubwege. Ubwege, sawa na udhanaishi, hutazama maisha kama fujo. Maisha ni mzunguko, ni duara, ndiposa maudhui, ploti, wahusika, na mazungumzo ya kazi za kiubwege hukosa umantiki.

Licha ya kuchunguza tamthilia ya *Amezidi* ili kuweza kuamua ni kwa kiwango gani imeafikiana na mkabala wa kiubwege, utafiti wetu pia unamulika kwa jicho pevu, chimbuko na maendeleo ya ubwege katika uandishi wa tamthilia ya Kiswahili, huku *Amezidi* ikiwa kama mizani yetu ya kupima athari ya ubwege katika tamthilia ya Kiswahili

### 1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI

Lengo la utafiti huu ni kuihakiki na kuinakidi tamthilia ya *Amezidi* iliyoandikwa na Said Ahmed Mohamed na kutolewa mara ya kwanza 1995, kama kazi ya kiubwege.

Tunadhamiria kuonyesha jinsi mwandishi huyu alivyoathiriwa na mkondo wa kiubwege na kubainisha ni kwa kina gani tamthilia ya *Amezidi* imefaulu kama kazi ya kiubwege.

Utafiti wetu unanua pia kupima mwelekeo wa Said Ahmed Mohamed, ambaye ni mmoja wa waandishi wa kutajika na ambaye amechangia pakubwa fasihi ya Kiswahili.

#### 1.4 SABABU ZA KUCHAGUA SOMO HILI

Ingawa uchambuzi wa *Amezidi* umewahi kufanywa na wahakiki mbalimbali wakiwemo King'ei (1997), Vuzo (1997), Wafula (1999), Ndalu (1998), na Njogu na Chimerah (1999), tahakiki zao zimeshughulikia zaidi vipengee vya maudhui na fani. Wafula (1999) na Njogu na Chimerah (1999) wamejaribu kushughulikia kigezo cha ubwege. Uhakiki wao ni wa kijuujuu, yaani haukuzama katika kumulika teneti zote za kiubwege. Kipengele cha ubwege kwa maoni yetu ni muhimu na kina nafasi kubwa katika tamthilia hii. Hivyo basi, tunakishughulikia kwa kina ili kuziba pengo hilo.

Aidha, wahakiki ambao wameshughulikia *Amezidi*, hawakufuata mikakati ya kitaalamu. Hakuna hata mmoja wao ambaye alitumia nadharia katika kuihakiki tamthilia hii kama ambavyo tunatarajia kufanya katika utafiti wetu.

Uhakiki wa kazi ya fasihi husaidia katika kueleweka na kufafanua kwa kazi hiyo. *Amezidi* ni tamthilia ambayo imechochea mijadala kadha wa kadha kati ya wasomi na wataalamu mbalimbali juu ya muundo na mwelekeo wa tamthilia ya Kiswahili. Tumechagua kuihakiki tamthilia hii ili kutoa mchango mahususi kwa wasomi na hata waandishi wa tamthilia.

Tunaamini pia kuwa, hakuna uhakiki unaoweza kudaiwa kwamba umekamilika. Hivi ni kwa sababu, wahakiki hutofautiana labda kwa mitazamo, misimamo, na pia uhakiki hutegemea mabadiliko ya kijamii, kulingana na wakati na katika maendeleo ya kihistoria ambayo kwa njia moja au nyingine huathiri maendeleo ya fasishi. Ndiposa Hough (1962: 6) akasema:

Hakuna kazi yoyoete ya uhakiki iliyokamilika.

Uhakiki haushughulikiwi wakati mmoja na ukawa ndio ukomo, kwani hutegemea historia na mazingira ya kijamii. Katika kila kipindi kipya cha historia, fasihi ya wakati uliopita yafaa kufasiriwa upya .... jinsi tunavyofasiri maandishi mapya ndivyo fasiri zetu za yale ya zamani zinavyobadilika. (Tafsiri yetu).

Tunaamini kwamba uhakiki wetu wa *Amezidi* utatoa mchango mahususi kwa fasihi na kurutubisha yale ambayo tayari yamesemwa na wahakiki kuhusu tamthilia hii.

### 1.5 MIPAKA NA UPEO WA SOMO HILI

Utafiti wetu unajikita katika tamthilia ya *Amezidi* kwa kuzingatia kigezo cha ubwege. Uchambuzi wa kazi ya fasihi, hasa tamthilia huhusisha vigezo mbalimbali Aghalabu, mhakiki hushughulikia maudhui, dhamira, pamoja na lugha na fani kwa ujumla. Katika uhakiki wetu tutamulika vigezo hivi vyote na vingine zaidi, pale ambapo tutahisi kuwa vimechangia hali ya ubwege katika tamthilia hii. Hivyo basi, kila kipengee muhimu cha tamthilia – hususan maudhui na fani kitachanganuliwa kwa kukihusisha na mtazamo wa kiubwege.

Said Ahmed Mohamed ameandika kazi nyingi za kifasihi. Mawanda ya uandishi wake si haba. Hata hivyo, uhakiki wetu umeelemea utanzu wa tamthilia na hasa tamthilia ya *Amezidi*. Tamthilia zingine ambazo ameandika hususan *Pungwa, Kivuli Kinaishi* na *Kitumbua Kimeingia Mchanga* hatutazishughulikia. Hivi ni kwa sababu, tamthilia hizi, hazielekei kufuata mkondo wa ubwege kama ambavyo tunaamini tamthilia ya *Amezidi* imefanya.

### 1.6 NADHARIA TETE

Utafiti wetu unaendelezwa na haipotesia zifuatazo:

- *Amezidi* ni tamthilia ambayo imevuka mipaka ya uandishi wa kiuhalisia na kuingilia uandishi wa kiubwege.
- Katika tamthilia ya *Amezidi* mwandishi anadhihirisha kuwa maisha hayana maana.
- Tamthilia ya *Amezidi* hukatisha tamaa.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Tamthilia ya *Amezidi* kama ambavyo tumetaja awali, imeshughulikiwa na wahakiki mbalimbali. Mpaka sasa, tahakiki nyingi ambazo zinaweza kupatikana kuhusu tamthilia hii, ni miongozo yenye nia ya kusaidia wanafunzi na walimu wa shule za upili kuelewa kazi hii ambayo ni mojawapo wa tamthilia zinazotahiniwa. Amina Mlacha Vuzo (1997) katika utangulizi wake anasema:

Mwongozo huu umeandikwa ili uwe kama kitulizo cha kilio kikubwa cha watu wengi katika mihadhara mbalimbali ya Kiswahili na hata kupitia kwenye magazeti wakisema kuwa kitabu cha *Amezidi* kimezidi kwa ugumu... mwongozo huu unatazamiwa kuwasaidia wanafunzi na wasomaji wote wa *Amezidi* kuweza kuelewa kitabu zaidi na kukipenda.

Katika uhakiki wake, Vuzo, ameshughulikia vipengee mbalimbali. Ametoa maelezo mafupi kuhusu mwandishi wa tamthilia hii, Said Ahmed Mohamed, jalada la kitabu hiki, na mtiririko na uchambuzi wa kila onyesho. Katika upande wa maudhui, ametaja na kufafanua: ukoloni na athari zake, tamaa, unyonyaji, njaa/ukame, uvivu/ubwete/uzembe, na hongo. Aidha, ametaja ubwege kama mojawapo ya maudhui katika kitengo cha Maudhui Mengine. Hatoi maelezo yoyote kuhusu ubwege wala kudhihirisha kuweko kwake katika tamthilia hii. Kadhalika, ameshughulikia mtindo, muundo, umbo, wahusika, na matumizi ya lugha. Hata hivyo, haonyeshi uhusiano wowote kati ya vipengee hivi na hali ya ubwege.

Kitula King'ei (1997) katika *Mwongozo wa Amezidi*, anaeleza juu ya dhamira, na kutoa muhtasari wa tamthilia, dhana ya kuzidi, muhtasari wa maonyesho, wahusika, maudhui: uvivu na uzembe, wizi na ufidia, utegemeaji wa misaada kutoka ng'ambo, kuburi na ubadhirifu. Hali kadhalika, ameshughulikia mbinu za usanifu na matumizi ya lugha, na nyenzo nyingine za sanaa. Ingawa haya yote ni muhimu, na yenye manufaa, mhakiki huyu hakushughulikia kigezo cha ubwege ambacho ni nguzo katika utafiti wetu.



Ndalu (1998) katika tahakiki yake, hajagusia hali ya kibwege katika tamthilia ya *Amezidi*. Hata hivyo, ameelezea vipengele kadha wa kadha vya uchambuzi. Ametoa utangulizi, muhtasari kwa jumla juu ya *Amezidi*, muhtasari wa maonyesho, dhamira na maudhui ambayo ni pamoja na siasa, ufisadi, uzalishaji mali, sera potovu za elimu, uchochole na usuhuba. Pia ameshughulikia mtindo na matumizi ya lugha, wahusika, mandhari na namna ya maswali ambayo mtahiniwa anaweza kutarajia katika mtihani. Kazi hii ni uchambuzi na mwandishi hakuhakiki kigezo cha ubwege kama ambavyo tunatarajia kufanya.

Maneno (1997) katika *Mwongozo wa Amezidi* anafuata nyayo za wenzake. Baada ya dibaji fupi, anatoa utangulizi ambapo anaelezea juu ya fasihi, tanzu za fasihi na sanaa ya maonyesho. Aidha, anatoa maelezo kuhusu mwandishi wa tamthilia, muhtasari wa kila sura, kiini na dhamira ya mwandishi, maudhui: umaskini na athari zake, ujinga, ufisadi, ubadhirifu na mapuuza, uhaba wa kazi, athari za tamaduni za kigeni, na ubinafsi na choyo. Pia ametoa ufafanuzi kuhusu wahusika, mbinu za kisanaa kama muundo, umbo, mtindo na fani na lugha. Mwongozo huu haukushughulikia kipengele cha ubwege.

Njogu (1997) katika *Mwongozo wa Amezidi*, ameeleza maudhui yakiwemo: maana ya uhuru, elimu, ukoloni mamboleo, umaskini wa Mwafrika, ufisadi na mapenzi. Pia amechambua vigezo vya wahusika, dhamira, pamoja na lugha na fani. Hakuzama katika kushughulikia kigezo cha ubwege.

Wafula (1999) anadokeza juu ya tofauti kati ya *Amezidi* na kazi zingine za mwandishi huyu. Anaeleza kuwa wasomaji waliozoea kudurusu kazi za kisanaa za Said Ahmed Mohamed watashangazwa na pengine kushtushwa na mtindo mpya uliobuniwa na mtunzi katika tamthilia ya *Amezidi* (uk. 68). Aidha, amechambua kwa kifupi vipengele mbalimbali vya tamthilia hii. Ametoa maelezo ya maonyesho na ufafanuzi wa pango, sauti, kicheko na wimbo. Kuhusu suala la ubwege anasema:

Said Ahmed Mohamed ametumia mtindo  
wa wasanii kama Samwel Beckett ... maisha  
ya Ame na Zidi ni ya kibwege<sup>5</sup>.

Uchambuzi huu umetufaa kwa kutupatia miale ya mawazo ya waandishi wa kibwege licha ya kwamba haukuzama wala kutumia mikakati ya kitaalamu.

Sarara (1997)<sup>6</sup> ameshughulikia maudhui katika tamthilia tatu za Said Ahmed Mohamed – Pungwa (1988), Kivuli Kinaishi (1990), na *Amezidi* (1995). Uhakiki huu umetoa mchango kwa utafiti wetu licha ya kwamba mhakiki amejikita katika maudhui tu, na kwamba kipengele cha ubwege hakijitokezi katika kazi yake.

Njogu na Chimera (1999) wametoa maelezo kuhusu *Amezidi* kama tamthilia ya kibwege. Wamebainisha na kufafanua kwa kifupi baadhi ya vipengee vinavyoendeleza ubwege kama vile wahusika, tamaa na matumaini. Ni kazi ambayo imenufaisha utafiti wetu ingawa wachambuzi hawakutumia nadharia yoyote.

Uhakiki wowote ule una manufaa yake. Hivyo basi hatuwezi kupuuza mchango wa wenzetu kama Vuzo, Maneno, na Wafula, ambao wamejikita zaidi katika maudhui na fani. Hivi ni vipengee muhimu chambilecho Ngara (1990:5) ambaye anasema kuwa ili kuelewa kazi ya sanaa, msomaji anapaswa kufahamu yaliyomo na fani yake.

Ni matumaini yetu kuwa, kwa kutumia nadharia mahususi, sisi tutapiga hatua kubwa zaidi mbele katika kuihakiki tamthilia ya *Amezidi* kama kazi ya kibwege.

## 1.8 MSINGI WA KINADHARIA

Nadharia ni chombo muhimu kwa mhakiki kwa vile ndiyo hutoa mwongozo bora wa utafiti. Utafiti wetu utaelekezwa na kuongozwa na nadharia ya udhanaishi.

*A Dictionary of Literary Terms* (1977: 251) inafafanua udhanaishi ifuatavyo:

Kwa misingi ya kifalsafa, udhanaishi hujikita

katika maoni ya hali na maisha ya mwanadamu,  
mahali pake na jukumu lake katika dunia pamoja  
na mahusiano yake, au ukosefu wa mahusiano  
hayo na Mungu. (Tafsiri yetu)

Nayo *Oxford Advanced Learners Dictionary* (1989:420) inaeleza udhanaishi kuwa:

Nadharia inayomtazama binadamu kama  
kiumbe chenye upekee na kilichojitenga  
katika dunia isiyo na maana na yenye ukatili  
na binadamu mwenyewe ana wajibu katika  
vitendo vyake na yu huru kuchagua hatima yake.  
(Tafsiri yetu).

Haya ni maelezo ambayo yanatilia maanani wazo la kuwoko kwa binadamu ulimwenguni. Ni maoni ambayo yanaafikiana kwa karibu na ya *Encyclopedia Americana* (1977:762)<sup>7</sup> ambayo inaeleza udhanaishi kama ambao huhusisha mitindo na imani mbalimbali na mojawapo ya sifa zake muhimu ambayo imeelezwa na asili ya ulimwengu, ni kujishughulisha kwake na kuwepo kwa binadamu. Hususan, hukubali uhuru wa binadamu na kukataa dhana zenye misingi ya kijamii inayodunisha kuwepo kwa binadamu ulimwenguni. Huwasilisha maasi dhidi ya mawazo na asasi ambazo huzuia uhuru wa wa binadamu na kupinga uwajibikaji.

Kwa upande wake, *Cassell's Encyclopaedia of Literature* (1953:213) imefasiri udhanaishi ifuatavyo:

... Kuna makundi kadhaa ya kifalsafa ambayo  
yapo chini ya udhanaishi na yote hutilia mkazo  
uhai wa binadamu na udhabiti wa tajriba yake  
kinyume na nadharia zisizo na mashiko za kuwazika tu.  
(Tafsiri yetu)

Kwa ujumla, udhanaishi ni nadharia inayojikita katika falsafa inayomwalia mwanadamu kama kiumbe maalum na chenye upekee, kilichojitenga na ambacho kimetupwa katika ulimwengu katili ambao haumjali. Mwanadamu hutengwa na wenzake pamoja na jamii yake. Nadharia hii pia hushikilia kwamba binadamu ana mamlaka na uamuzi wa matendo yake pamoja na kuwa ana uhuru wa kuchagua hatima yake. Katika kuchagua hatima yake, wanaudhanaishi wameonyesha kwamba, mwanadamu anaweza kujiua kikweli, au kujiua kifalsafa

kwa kukimbilia faraja nyingine kama vile dini. Mwanadamu anaweza pia kuyaishi maisha jinsi yalivyo huku akingojea kifo.

Kulingana na Benton (1968: 984), neno udhanaishi lilitumiwa kwanza kuelezea mwelekeo au mtazamo wa kifalsafa ambao ulijibaini kule Ujerumani miaka michache baada ya Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia, na baadaye kusambaa hadi Ufaransa na kuathiri fasihi.

Licha ya hayo, udhanaishi ulibainika vyema katika kipindi cha Vita Vikuu vya Pili (1939-1945). Katika vita hivyo, kulikuwa na uharibifu mkubwa wa mali. Watu wengi walipoteza maisha yao ilhali wengine waliachwa wakiwa viwete huku wengine wakiathiriwa kwa namna mbalimbali na zana za kivita zilizotumika. Aidha, jamii zilivurugwa na kusambaratika. Mila na desturi zikavunjika huku jamaa wa jamii moja wakitawanywa ovyo. Watu waliteseka. Hawakuwa na matumaini ya furaha. Kifo na umwagikaji wa damu vilitawala maisha ya watu. Ni kutokana na hali kama hii ambapo falsafa hii iliibuka na kushika nguvu. Maisha ya binadamu yakaonekana kama hayana maana yoyote. Masuala ya dini, Mungu na kuishi, yakapoteza maana.

Dhana ya udhanaishi hata hivyo, inaaminika ina misingi yake katika wakati wa watu kama St. Augustine, Duns Scotus, na Pascal. Ni nadharia ambayo ilirutubishwa na kuanzishwa upya baadaye na Soren Kierkegaard (1813-55). Vitabu vyake hasa *The Concept of Dread, Fear and Trembling* na *Sickness unto Death*, vilisaidia katika kutoa na kukuza msingi bora na imara wa nadharia hii.

*Encyclopedia Americana* (1977: 762), inamtambua Kierkegaard kwa juhudi zake za kuendeleza udhanaishi. Inataja wazo kwamba, mwanathiolojia huyu anaweza kuelezewa kama mwanzilishi wa udhanaishi wa kisasa.

Katika karne ya ishirini, nadharia hii ilipata wafuasi wengine kama vile Friedrich Nietzsche, Martin Heidegger na Karl Jaspers. Baadaye, Jean-Paul Sartre, Albert Camus, Dostoevsky (*Notes from Underground*), na Franz Kafka, na Georges Bataille, walijitokeza, na kazi zao zikausambaza udhanaishi na kuathiri wasanii wengi. Wanafalsafa wengine ambao wamejitambulisha na mtazamo wa udhanaishi ni Martin Buber, Herbert Farmer, Nicholas Berdyaev, John Mackmurray, na Donald Mackinnon.

Nadharia ya udhanaishi, hubainisha matapo mawili makuu. Tapo la kwanza ambalo linaongozwa na mkabala wa Kilimwengu (Atheist Existentialism) lilichochea na kuendelezwa na watu kama Jean-Paul Sartre, Georges Bataille, Maurice Merleau-Ponty, Simone de Beauvoir, na Samwel Beckett. Ni tapo ambalo hutilia mashaka suala la Mungu.

Tapo la pili ni lile ambalo husukumwa na mkabala wa Kikristo (Christian Existentialism). Hapa Gabriel Marcel hujitokeza kama mfuasi stadi asiyeteteleka. Mchango wa Marcel katika kutetea na kusukuma mbele udhanaishi wa Kikristo, unaungwa mkono na Heinemann (1958:218) kwa kukubali kuwa, Gabriel Marcel ndiye mwanafalsafa mkuu katika tapo la udhanaishi wa Kikristo.

Greene (1960:61) anaelezea juu ya viongozi wa matapo haya mawili ya udhanaishi. Anataja kwamba, Gabriel Marcel ambaye anatambuliwa kama kiongozi wa udhanaishi wa Kikristo, alieleza kuwa, Sartre, alipokuwa akishuka kutoka kwa ndege, wakati alitemelea Uswizi, aliwashangaza waandishi wa habari alipowaamkia kwa kauli kuwa 'Mungu Amekufa'. Sartre ndiye kiongozi wa kundi la udhanaishi wa Kilimwengu, ingawa wakati mwingine alikataa. Sartre alinukuliwa<sup>8</sup> akisema:

... Udhanaishi ambao awali ulihusishwa na  
Kierkegaard, ulienda sambamba na imani  
za kidini. Udhanaishi wa Kifaransa leo huelekea  
kuhusishwa na kutosadiki kuwa Mungu yuko,  
lakini hilo hakika sio lazima. (Tafsiri yetu).

Kati ya matapo haya mawili, udhanaishi wa kikristo ndio uliotangulia kutambuliwa. Foulquie (1947:60) anatoa msimamo wake kuwa udhanaishi wa Kikristo ndio mkongwe ukilinganishwa na udhanaishi wa kilimwengu. Kierkegaard anatazama chimbuko la tapo hili katika falsafa za Sokrates. Hata hivyo, udhanaishi wa kilimwengu ndio ambao umeendelea sana na Jean-Paul Sartre anasifiwa kwa matokeo hayo. Mawazo haya yanaafikiana na ya Kaufmann (1956:40) anaposema:

Ni kupitia kazi za Jean-Paul Sartre ambapo  
udhanaishi umesambaa sana kimataifa.  
(Tafsiri yetu)

Kuna vipengele vingine muhimu vya udhanaishi. Suala la ulimwengu mkali unaomtesa binadamu ni dhahiri. Camus (1913-1960), aliamini kuwa mahali pa binadamu ulimwenguni ni duni katika ulimwengu duni<sup>9</sup>. Mawazo haya yanakaribiana na ya Samwel Beckett<sup>10</sup>. Beckett, ambaye alikuwa mwandishi wa riwaya na tamthilia, alidai kuwa, binadamu ni kiumbe aliyetengwa na kuwekwa katika ulimwengu wenye masuala mengi yanayohuzunisha. Kazi zake, zikiwemo *Waiting for Godot* (1956) na *End Game* (1958), ziliigizwa katika kile ambacho kilitambuliwa baadaye kama drama ya kiubwege (Theatre of The Absurd) na mhakiki Esslin Martin (1961:4).

Suala la binadamu na maisha yake magumu katika ulimwengu katili, linaendelezwa na Greene (1960:9-10) anapoeleza kuwa kuteseka na kuhisi maumivu kwa binadamu ni hali ambayo haiwezi kuepukika ulimwenguni. Binadamu ni sharti ayaishi maisha jinsi yalivyo bila kuyakwepa. Binadamu hujikuta katika hali fulani na ingawa hakuchagua hali hiyo, analazimika kushikamana nayo kwa vile hana uwezo wa kutengana nayo.

Kifo nacho ni kipengee muhimu katika muktadha wa udhanaishi. Kifo huchukuliwa kama hali ya kawaida na ni daraja nyingine ya maisha. Inaaminika hapa kwamba, hakuna tofauti kati ya kuishi na kufa. Samwel Beckett<sup>11</sup> anadai kwamba:

Maisha ni kuendelea kufa, mfanyiko ambao  
unaendelea mpaka kiwango kitakiwacho, kifo  
cha hakika. (Tafsiri yetu)

Ni maoni ambayo yanaoana na ya Ignace Lepp (1968:139) anayesema kwamba:

Badala ya kufikiria kifo kama mwisho wa  
maisha, napendekeza tukitazame kama  
kitendo cha mwisho katika tutimiliza  
maisha ya muda. Basi itafuatia kwamba  
tukifaulu katika kuyapa maisha yetu maana,  
vivyo hivyo kifo kitakuwa na maana. (Tafsiri yetu)

Maisha yanaonekana kama kitendawili ambacho binadamu anapaswa kukitegua, na akifaulu, atakuwa pia amejua maana ya kifo, kwa vile maisha na kifo haviwezi kutenganishwa.

Freeman (1971:5) akimnukuu Camus, anatetea kifo kwa kusema kuwa kifo kinaweza kuleta maana katika maisha katili na yasiyo na maana.

Binadamu anajikuta katika hali ya kukabiliwa na kifo, na hana njia ya kuepukana nacho. Hivyo basi ni sharti akabiliane nacho. Katika mtazamo wa kukubali ukweli huu, Warnock (1970:59), anaeleza kuwa binadamu katika kukabiliana na hali ya utupu wa ulimwengu, anagundua kwamba yuko pekee, tofauti kabisa ukimlinganisha na watu au vitu vingine katika ulimwengu. Binadamu anajikuta hana njia ya kuweza kujisaidia wala kupata msaada kutoka kwa watu wengine. Linalobaki ni kifo cha upweke. Hali ya kutoishi kabisa ndiyo ya mwisho ambayo binadamu anatazamia.

Suala la Mungu nalo linapatiwa umuhimu katika nadharia ya udhanaishi. Kuweko kwa Mungu kunatiliwa mashaka. *The New Columbia Encyclopedia* (1975:2427) inaeleza kuwa, Jean-Paul Sartre, mtetesi wa udhanaishi wa kilimwengu alidai kuwa hakuna Mungu na hivyo basi binadamu hana shuruti yoyote ya kutenda jambo fulani. Pengine Sartre alitoa maoni haya kutokana na kuathiriwa na Vita Vikuu vya Pili ambavyo alishiriki kama mwanajeshi, sawa na Camus. Aliamini kuwa binadamu atajiletea maadili maishani mwake peke yake bila kutegemea Mungu.

Kiudhanaishi, wazo la Mungu linamjia binadamu baada ya kushindwa kukabiliana na maisha yake. Wilson na Goldfarb (1991:402) wanasema:

Wana-udhanaishi wanaamini kuwa Mungu  
hayuko na hivyo binadamu yumo pekee katika  
ulimwengu katili. Kitendo muhimu ambacho  
binadamu anaweza kufanya ni kukubali mamlaka  
juu ya yale ayatendayo ulimwenguni. (Tafsiri yetu)

Mmoja wa watetezi wa nadharia hii, Friedrich Nietzsche ambaye anasifika kupitia kwa vitabu vyake hasa *Thus Spake Zarathustra* na *The Will to Power*, alidai kuwa 'Kanisa ni Kaburi la Mungu'<sup>12</sup>. Madai haya ya Nietzsche, yanatiliwa nguvu na Roubiczek (1964:41) ambaye anatupatia swali ambalo Nietzsche alipenda kuuliza:

Makanisa yetu ni nini kama si makaburi ya Mungu?

Mawazo haya ya Sartre na Nietzsche juu ya Mungu, yalikuwa yamedhihirika awali hasa kupitia Pascal (Foulquie 1947:56) ambaye aliandika na kuuliza:

Mungu anaishi au la? Tunawezaje kuamua?

Kigezo cha ukweli nacho husisitizwa katika nadharia hii. Soren Kierkegaard (1813-55) alidai kuwa ukweli wenye umuhimu hauwezi ukapatikana kwa urahisi (1977:762). Aliongezea kuwa ukweli hutegemea mtu – kwamba ukweli ni ukweli tu katika muktadha wa mtu au kundi la watu. Naye Warnock (1970:78) anasema:

Ukweli upo kwa sisi sote, lakini ni wajibu  
wa kila mmoja wetu kuutafuta na kuupata.  
(Tafsiri yetu)

Hoja ya binadamu kufikiri inahimizwa pia. Friedrich Nietzsche alidai kuwa ubunifu wa binadamu ndio utamwoko wa binadamu kutoka kwa genge la watu duni<sup>13</sup>. Aidha, alidai kuwa binadamu na ubunifu wake atafanikiwa tu kutokana na kufikiri kwake. Nietzsche, pamoja na wenzake Kierkegaard na Karl Jaspers waliamini kuwa kufikiri kwa maana huanza wakati ambapo mtu amejielewa mwenyewe. Umuhimu wa suala hili la kufikiri unatambuliwa pia na Wamitila (1997:16) ambaye amedai kuwa Socrates, anayetazamwa kama mdhanaishi wa kwanza, aliwaasa wanafalsafa, wajijue wenyewe kwanza, yaani 'know thyself'.

Udhanaishi pia unatetea wazo kuwa binadamu ni mnyonge na hana hiari na matukio ambayo anashuhudia maishani mwake. Matukio hubainika tu bila kutarajia. Ni mithili ya ajali maishani.

Mwasisi wa imani hii ni Martin Heidegger, ambaye alieleza kuwa binadamu analazimika kuitegemea ajali, ajali ambayo ndiyo chanzo cha mambo ambayo hutokea maishani mwake. Ingawa huu ndio ukweli, binadamu hajaridhika, na hivyo hujaribu kuliondoa wazo hili mawazoni mwake, bila mafanikio yoyote. (1975:1216)

Ingawa sifa ambazo tumetaja na kufafanua ni mhimili wa nadharia hii, fasihi ya ubwege hubainika kama teneti muhimu. Kuna uhusiano wa karibu kati ya ubwege na nadharia ya udhanaishi, hali ambayo imetufanya tutumie nadharia hii katika kuihakiki tamthilia ya *Amezidi*



kama kazi ya kiubwege. Ubwege ni tapo la kifasihi linalofuata falsafa ya udhanaishi. Mwingiliano huu kati ya ubwege na udhanaishi ndio sababu tosha iliyotusukuma kutumia udhanaishi kama chombo cha kuabiria katika utafiti wetu.

Baadhi ya sifa za ubwege ambazo zinaoanisha mada yetu na nadharia tunayoitumia ni suala la mandhari. Mandhari hujitokeza kama nguzo ya kukuzia vipengele vingine vya udhanaishi. Ubwege hutilia maanani mazingira ya fasihi. Kiubwege, mazingira yanayobainishwa huwa ni machafu na ambayo huchukiza. Hali hii hulengwa kuashiria kuchukiza kwa maisha. Suala hili linaingiliana vizuri na imani ya kidhanaishi kuwa maisha ni adhabu, hayana furaha. Albert Camus (Cruickshank 1959:27) anadai kwamba furaha ya kudumu haiwezi kupatikana katika maisha ya binadamu, maisha yake ni ya huzuni tupu.

Udhanishi unatazama hali ya binadamu kama ambayo ni duni na ambayo haiwezi kutamanika. Kwa wana-udhanaishi, furaha ni neno lingine la adhabu.

Umuhimu wa suala la mandhari katika fasihi ya ubwege, unasisitizwa na Mbatiah (1997:8) anaposema kuwa katika fasihi ya uduni (Literature of The Absurd), suala la mandhari ni muhimu sana. Wasanii katika tapo hili, hutumia mandhari kubainisha msimamo wao kwamba ulimwengu ni wa kinasibu, duni na wa kukatisha tamaa na yanazua hisia za uchovu, huzuni na kukata tamaa.

Fasihi ya ubwege huwa haina muumano mzuri wa vitushi ambao ndio mhimili wa ploti. Hivyo basi matukio yake huwa yamevurugwa kiasi cha kutoweza kuyaunganisha. Mambo hutokea tu

kiupweke, ni kama kila jambo limejitenga. Utengano huu wa vitushi katika kazi za kiubwege, unaenda sambamba na imani ya kidhanaishi kwamba binadamu ni kiumbe pweke, na aliyejitenga na wenzake pamoja na jamii yake. Anajikuta katika ulimwengu dhalimu bila msaada wowote. Greene (1960:1) anaeleza kuwa kinachotambulika ulimwenguni ni hali ya kukata tamaa, hofu na upweke ya kuweko kwa binadamu.

Wahusika wa kazi za kiubwege, huwa hawana uwezo wa kuboresha hali zao. Vitendo vya mhusika huwa havina muwala wala umuhimu wowote ila kuonyesha ubatili tu. Mambo madogo madogo kama kutoa viatu, kutembea na kupika, yanawashinda. Hali hii ndiyo

hubainika katika *Waiting for Godot*, *Amezidi*, na *The Blood Knot*. Mazungumzo ya wahusika hukosa ruwaza maalum katika mtiririko wake. Wahusika wa kibwege hawana umotishaji, na vitendo vyao hutokea tu bila msingi wala sababu. Hali hii inaoana vizuri na msimamao wa kidhanaishi kuwa binadamu hana uwezo bali hutegemea majaaliwa maishani mwake. Ni wazo linaloafikiana na madai ya Foulquie (1947:57) anaposema:

Hali yetu inategemea ulimwengu tuliomo.  
Bila ulimwengu huo hatutakuwa chochote.  
Ni kutokana na ulimwengu huo dhalimu  
ambapo tunajikuta tukiishi bila nguvu au  
uwezo wowote. (Tafsiri yetu)

Ni dhahiri kuwa tofauti kati ya nadharia ya udhanaishi, na ubwege ni nyembamba mno. Njogu na Chimera (1999:15) wanasema kuwa, nadharia hii inakaribiana sana na ya “ubwege”.

Mwingiliano huu kati ya ubwege na nadharia ya udhanaishi umetupa mwelekeo unaofaa katika kuihakiki tamthilia ya *Amezidi* kama kazi ya kiubwege.

## 1.9 NJIA ZA UTAFITI

Utafiti wetu utakuwa wa maktabani. Tutaisoma tamthilia ya *Amezidi* kwa undani na makini ili kuelewa vyema na kuichanganua. Pia tatazisoma tamthilia zingine zilizoandikwa na Said Ahmed Mohamed kama vile *Kivuli Kinaishi*, *Pungwa* na *Kitumbua Kimeingia Mchanga*. Hali kadhalika, kazi zingine za msanii huyu mashuhuri zikiwemo mashairi – *Sikate Tamaa* na *Kina cha Maisha*; riwaya – *Kiza Katika Nuru*, *Dunia Mti Mkavu*, *Asali Chungu* na *Utengano*, tutazipitia. Ingawa kazi hizi zingine za Mohamed zinajitenga na suala la ubwege, zitatusaidia katika kupima mwelekeo wa mwandishi huyu hasa katika tamthilia ya *Amezidi*.

Tutajaribu pia kusoma tamthilia na kazi zingine za Kiswahili ambazo kwa njia moja au nyingine zinalingana na tamthilia tunayoishughulikia.

Aidha, tutatafiti maandishi yanayohusiana na tamthilia na au fasihi kwa ujumla. Makala na tasnifu mbalimbali kuhusu tamthilia, pia yatatusaidia kupata mtazamo mpana katika utafiti wetu.

Tutasoma pia vitabu, na maandishi mengine yahusiyo nadharia na falsafa ya udhanaishi. Maandishi haya yatatufaa katika kuifahamu nadharia hii ya uhakiki wa fasihi na kuweza kuitumia ipasavyo.

Mwisho, hatukusahau kutafuta maoni ya wasomi na wataalamu mbalimbali wa fasihi. Mchango ambao tumepata kutoka kwa maoni ya wasomi si haba. Ni matumaini yetu kwamba, mawazo yao yataendelea kusukuma mbele utafiti wa fasihi.

## TANBIHI

---

- <sup>1</sup> Mlama P. M. (1983) "Utunzi wa tamthilia katika Mazingira ya Tanzania". Makala katika *Fasihi III*, Tuki Dar es Salaam Uk. 203
- <sup>2</sup> Taz. Vuzo A. M. (1997) *Mwongozo wa Amezidi*. Macmillan Kenya Ltd., Nairobi. Utangulizi.
- <sup>3</sup> Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.
- <sup>4</sup> Camus Albert (1984) *The Myth of Sisyphus*, Penguin, London. Uk. 88-91
- <sup>5</sup> Taz. Wafula R. M. (1999) *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake*. Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi Uk. 78
- <sup>6</sup> Taz. Sarara, M. M. (1997) *Maudhui Katika Tamthilia za S. A. Mohammed* Tasnifu ya M. A. Haijachapishwa. Sura ya 3
- <sup>7</sup> Encyclopedia Americana Corporation (1977) *Encyclopedia Americana* Grolier Ltd., New York. Uk. 762
- <sup>8</sup> Taz. Pasquier Albert (1950) *Les Doctrines Sociates en France*, Paris. Uk. 152
- <sup>9</sup> Kama 7 hapo juu Uk. 762
- <sup>10</sup> William, H. na Levey J. S. (Wahariri) (1975) *The New Columbia Encyclopaedia* Columbia University Press, New York. Uk. 256

- 
- <sup>11</sup> Taz. Mueller, R. W. (1964) *The Testament of Samwel Beckett*  
Faber and Faber, London.  
Uk. 110
- <sup>12</sup> Kama 7 hapo juu Uk. 762 – 763
- <sup>13</sup> Kama 10 hapo juu Uk. 1941

## **SURA YA PILI**

### **2.0 HISTORIA NA TANZU ZA DRAMA**

#### **2.1 UTANGULIZI**

Katika sura hii tumeshughulikia suala la historia, maendeleo na aina za drama. Tumejaribu kumulika chimbuko la tamthilia ya Kiswahili na kufafanua tanzu muhimu ambazo zimebainika katika uandishi wa drama. Aidha, tumetoa hitimisho ambalo ni muhtasari wa vipengele muhimu ambavyo vimejitokeza katika sura hii.

#### **2.2 HISTORIA YA DRAMA**

Asili ya utanzu wa tamthilia inapatikana katika fasihi simulizi. Tanzu za fasihi simulizi kama vile ngano, sarakasi, nyimbo na hadithi, ndizo kitovu cha tanzu za fasihi andishi. Kumekuwa na madai kuwa, tamthilia imeletwa Afrika na Wageni<sup>1</sup>. Kulingana na dai hili, inabainika kuwa uandishi wa fasihi, hasa tanzu za tamthilia na riwaya ulianza katika nchi za Kimagharibi na baadaye kusambaa hadi barani Afrika.

Hali ya kisiasa ulimwenguni ilichangia na kuendeleza athari ya fasihi. Bara la Afrika lilitawaliwa na wakoloni, wakiwemo Waingereza na Wajerumani. Katika enzi hii ya ukoloni, elimu ya kigeni ilitawala katika mashule. Waingereza kwa mfano, walitumia vitabu vyao kufundishia shuleni ili kuendeleza sera yao ya tenga utawale. Baadhi ya vitabu vya fasihi vilivyotawala kipindi hicho ni *The Merchant of Venice*, *Julius Caesar* na *Romeo and Juliet*. Mafunzo haya yaliathiri wanafunzi Waafrika ambao baadaye walianza kuandika tamthilia. Hata hivyo, tamthilia za awali kabisa za Kiswahili zilibainika miaka ya arobaini kupitia Mzungu, Graham Hyslop.

#### **2.3 MAENDELEO YA TAMTHILIA YA KISWAHILI**

Wafula (1999) ametoa historia fupi ya tamthilia ya Kiswahili. Utanzu wa tamthilia katika uandishi wa Kiswahili hauna historia ndefu ukiulinganisha na tanzu zingine kama vile riwaya. Ingawa kulikuweco na maigizo, mchezo wa kuigiza ulioandikwa haukubainika mpaka miaka ya 1940. Ni katika kipindi hiki ambapo mwandishi wa kigeni, Graham Hyslop, alipojitokeza kama mwandishi wa tamthilia ya Kiswahili. Jitihada zake ziliza mema mwaka wa 1957 alipoandika na kuchapisha tamthilia mbili, *Afadhali Mchawi* na *Mgeni Karibu*. Pengine ni

kutokana na mafanikio haya ambapo Bertoncini (1989) anadai kuwa mchezo wa kuigiza wa Kiswahili ulioandikwa ulikuja na wakoloni. Madai haya yana mashiko.

Katika mwaka wa 1974, tamthilia zingine mbili za Hyslop, *Mchimba Kisima* na *Kukopa Harusi Kulipa Matanga* zilichapishwa. Mwanafunzi wa Hyslop, Henry Kuria aliandika *Nakupenda Lakini* (1957). Baadaye, Gerishon Ngugi aliandika *Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi* (1961). Uandishi wa tamthilia ya Kiswahili uliendelezwa kupitia tafsiri za kazi za kigeni kwa kiswahili. Mojawapo ya tafsiri za awali kabisa ni *Mchuuzi Muungwana* J. B. P. Moliere (1966) ambayo ilifanywa na Morrison.

Mnamo 1967, E. Hussein alichapisha *Wakati Ukuta* na *Alikiona*. Wakati huo huo tamthilia *Dunia ilivyofarakana*, yake Crispin Hauli, ilichapishwa. Mwaka uliofuata Nkwera F. alichapisha *Johari Ndogo* huku S.S Mushi akichapisha tafsiri ya *Macbeth*. Kazi zingine ambazo zilifuata ni kama *Tufani* (1969) S.S Mushi, *Julius Kaisari* na *Mabepari Wa Venisi* (1969) tafsiri za Julius K. Nyerere, na *Mashetani* (1971) E. Hussein.

Miaka ya sabini, baada ya *Mashetani* kuchapishwa ilishuhudia tafsiri na uandishi wa tamthilia nyingi za Kiswahili. Baadhi yazo ni *Mfalme Edipode* (Mushi 1971), *Mfalme Juha* (Farouk Topan 1971), *Hatia* (Mlama 1972), *Kifo Barabarani* (Ngahyoma 1972), *Aliyeonja Pepo* (F. Topan 1973), *Tambueni Haki Zetu* (Mlama 1973) na *Masaibu ya Ndugu Jero* (A. S. Yahya 1974). Mwaka wa 1975, tamthilia *Kortini Mtu Huyu* (Mlama), *Pambo* (Mlama), *Mwanzo na Tufani* (Kulikoyela na Ngerema), *Jogoo Kijijini* na *Ngao Ya Jadi* (E. Hussein) zilichapishwa<sup>2</sup>.

Waandishi wengine waliibuka miaka iliyofuata. Mwangudza Johnson aliandika *Thamani Yangu* (1976) Ibrahim Ngozi (1977), *Machazi ya Mwanamke*, Faraji Katambulla (1978), *Unono* na *Mizani ya Imani Yangu*, Mulokozi M. M. (1979), *Mukwava wa Uhehe*, Felix Osodo (1979) *Hatari kwa Usalama*. Mwaka huohuo, tafsiri *Mzalendo Kimathi*, Ngugi Wa Thiong'o na Micere Mugo), na *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (Mwakasaka Christon) zilichapishwa.

Tamthilia ya Kiswahili ilizidi kupata maendeleo katika miaka ya themanini (karne ya ishirini). Ni katika kipindi hiki ambapo waandishi wengi kutoka Kenya walijitokeza. Ikumbukwe kuwa waandishi kutoka Tanzania ndio wengi. Baadhi ya tamthilia zilizochapishwa ni *Giza Limeingia* (E. Mbogo), *Tazama Mbele* (Jay Kitsao), *Arusi* (E. Hussein), *Watoto Wetu* na *Tone*

*la Mwisho* (E. Mbogo), *Mke Mwenza* (Chacha N. Chacha), *Kilio cha Haki* (Alamin Mazrui), *Malimwengu Ulimwenguni* na *Bibi Arusi* (Jay Kitsao), *Ukame* (Yahya na Mulwa), *Nguzo Mama* (Mlama P.), *Buriani* (Yahya A. S), *Maisha Subira* (Said A. Omar), *Marejeo* (1986) na *Wingu Jeusi* (1987) zake Chacha N. Chacha, *Mama ee* (1987) cha Ari Katini Mwachofi. Mwaka wa 1988, tamthilia kama *Pungwa* (S. A. Mohamed), *Kwenye Ukingo wa Thim* (E. Hussein), *Ngoma ya Ngwanamalundi*, (E. Mbogo) na *Mkimbizi* (Yahya na Mulwa) zilichapishwa.

Kuanzia mwaka wa 1990 mpaka sasa, tamthilia nyingi za Kiswahili zimechapishwa. Ni vigumu kutaja kazi hizi zote. Baadhi yazo ni *Kivuli Kinaishi* (1990) yake Said A. Mohamed, *Hukumu* (1992) cha Chacha N. Chacha, *Amezidi* (1995) Said Ahmed Mohamed, *Natala* (1997) cha Kithaka Wa Mberia, *Wingu la Kupita* (1999) cha K. W. Wamitila, *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000) cha Said A. Mohamed, na *Kifo Kisimani* (2001) chake Kithaka Wa Mberia.

Tukumbuke kuwa, kimaudhui na hata kifani, tamthilia hizi zinatofautiana kulingana na wakati, na wasanii husika. Kutokana na wingi wa kazi hizi, ni dhahiri kusema kuwa, tamthilia ya Kiswahili, ingawa imeibuka miaka michache iliyopita, imepiga hatua kubwa kimaendeleo na kuna matumaini ya mafanikio zaidi kupatikana.

#### **2.4 TANZU ZA DRAMA**

Tangu kuibuka kwake, drama imepata mielekeo mingi. Ingawa tanzia na futuhi ni aina mbili kuu za drama ambazo zimetawala majukwaa kwa miaka mingi, mikondo mingine ya tamthilia imejitokeza na haiwezi kupuuzwa. Tumeainisha aina mbalimbali za tamthilia na kujaribu kuzitolea ufafanuzi na mifano. Hata hivyo, suala la uainishaji lina utata kwa sababu ya mwingiliano wa sifa kati ya tanzu hizi za tamthilia.



## 2.5 DRAMA YA KIUBWEGE

### 2.5.1 DHANA YA UBWEGE

Ni jambo la busara kujaribu kufafanua maana ya ubwege kabla ya kuzama katika drama ya kiubwege. Dhana ya ubwege iliingizwa katika fasihi na mwandishi na pia mwanafilosofia wa Kifaransa, Albert Camus (1913-1960). Kulingana naye, ubwege si kitu ambacho kinaweza kuguswa bali ni uhusiano wa kidhahania kati ya akili pevu na ukweli wa kuweco kwa binadamu ulimwenguni. Hali ya ubwege hutokea kwa sababu ya kutoridhika kwa akili kulingana na matarajio yake juu ya utaratibu wa matukio ulimwenguni. Kinyume na matarajio hayo, hali inayojitokeza ni yenye fujo na ambayo hukaidi umuwala, na haiwezi kufahamika. Hali hii ya ubwege inafafanuliwa zaidi na Cruickshank (1960:41) anaposema:

. . . Kwa ubwege, Camus kwa ujumla anamaanisha ukosefu wa muumano au usawa kati ya mahitaji ya uwiano wa kiakili na ukosefu wa uwiano katika ulimwengu ambao akili hukumbana nao. (Tafsiri yetu)

Mhakiki mashuhuri, Esslin Martin (1961:5) katika kitabu chake *The Theatre of The Absurd*, akimnukuu Eugene Ionesco anasema kuwa ubwege ni kile ambacho kimekosa nia ni kile ambacho kimetengwa kutoka kwa imani za kidini, tabia za kiungu na mizizi ya kiakili na mawazo. Binadamu amepotea; vitendo vyake vyote ni vya kijinga, kiubwege, havina maana.

Camus (1955)<sup>3</sup> anatoa dai kuwa, hali hii ya kutoridhika kwa moyo, huleta kuteseka kwa akili. Aidha, hali hii humpa binadamu suluhisho aina mbili. Anaweza kukubali ukweli wa hali yake na kuukabili, au akaamua kujiua. Hata hivyo, kwa kujiua, binadamu huangamiza akili yake ambayo ingehisi hali ya ubwege. Kwa upande mwingine, kukubali hali ngumu na ya mateso ambayo ndiyo ukweli wa maisha, kunathibitisha utata wake, ubwege.

Lewis (1962:259) anafafanua hali hii duni ya binadamu ulimwenguni. Anasema:

Binadamu yuko pweke na amepotea katika  
ulimwengu ambamo Mungu amemtupa;  
sayansi na kufikiria ni madanganyo; binadamu  
ametekwa na ulimwengu katili. Kitu dhahiri  
ambacho kimebaki ni kifo, ambacho ni kitendo  
cha mwisho cha ubwege. Mawasiliano hayapo  
tena kwa vile hata lugha imekufa. Ulimwengu ni fujo.  
(Tafsiri yetu)

Ubwege ni ukosefu wa utaratibu. Binadamu anaishi katika ulimwengu dhalimu na hana uwezo wa kupanga matukio yake. Hivyo basi anayotenda na kusema hukosa muumano. Hali yake ni ya kiubwege.

## 2.5.2 HISTORIA NA MUKTADHA WA UBWEGE

Chimbuko la ubwege hutazamwa katika Karne ya Kumi na Tisa na mwanzoni mwa Karne ya Ishirini. Kipindi hiki kilishuhudia mabadiliko mengi katika maisha ya binadamu hasa kule Uropa. Vita Vikuu vya Ulimwengu, vilirutubisha misingi ya mtazamo huu. Watu wengi na mali nyingi iliharibiwa. Cruickshank (1960) anaeleza kuwa kuporomoka kwa maadili na thamani ya binadamu katika kipindi hiki, kulipelekea kuibuka kwa ubwege.

Wafuasi wa ubwege walianza kupinga imani za kidini. Ni wakati huu ambapo wanafalsafa kama Friedrich Nietzsche walianza kutilia shaka imani za kidini. Wakati huohuo, jaribio la sayansi kufafanua asili na hali ya dhana mbalimbali za maisha bila mafanikio mema, na kutofaulu kwa mawazo ya kiuchumi na kisiasa kama yale ya Kimarx, kulipelekea watu kama Camus kutafakari zaidi juu ya uwezo na umuhimu wa binadamu ulimwenguni. Maisha ya binadamu yakaonekana kukosa maana na hali ya upweke wa binadamu ulimwenguni ikajibaini vyema<sup>4</sup>.

Kulingana na Camus, hali ya ubwege iliendelezwa na nadharia fulani za tapo la wanafalsafa ambazo zilimkengeusha binadamu na kumfanya hasifahamu ulimwengu wake. Camus (1953:11) anaeleza kuwa:

Tunaishi katika kipindi chenye uhalifu mwingi.  
Wahalifu tunaoshuhudia sasa si watoto dhaifu  
bali ni watu wazima ambao wamepata njia ya  
kujitoka katika lawama kwa kutumia ujanja.  
Wanatumia falsafa, ambayo pia inaweza  
kutumiwa kwa lolote, hata kugeuza wauaji kuwa  
mahakimu. (Tafsiri yetu)

Camus kwa mfano alishangazwa na vitendo vya kinyama vilivyodhihirika katika biashara ya watumwa, vita na mawazo ya kiuchumi ambayo yalienea Uropa na kutetewa kwa kutumia falsafa mbalimbali. Watu wengi wasiokuwa na hatia waliteseka na wengine kupoteza maisha yao. Vita Vikuu vya Pili vilisababisha uhalibifu usiomithilika wa mali na maisha (Camus, 1953:14). Maisha ya binadamu yakapoteza maana, ubwege ukatanda ulimwenguni. Hali hii ilibomoa zaidi imani juu ya Mungu. Watu wakaanza kujiuliza – kama kweli Mungu yuko, kwa nini hasaidii viumbe wake? Camus, akatazama kufuata dini kama kujiua kifalsafa.

Dini ni chombo cha kutuliza binadamu anayeteswa na ulimwengu. Inampa matumaini mema siku zijazo katika mahali palipotayarishwa na Mungu. Camus anaiona dini kama kasumba ambayo imempofusha binadamu asione ukweli. Hivyo basi yeyote atakaye kujua ukweli wa maisha sharti ajitenge kutoka kwa imani na falsafa za kidini. Binadamu anapaswa kukabiliana na hali yake kikamilifu, na kama hawezi, anapaswa kujiua.

Sayansi nayo imeshindwa kutoa maelezo kamili juu ya matukio ulimwenguni. Binadamu, wanasayansi wakiwemo, ameshindwa kuthibitisha sababu inayowafanya watu kutenda wayatendayo na kuwa na tabia waliyonayo. Hali hii ya kutojua ndiyo msingi wa hali ya ubwege. Webb (1972:13-14) anaelezea hali hii ya sintofahamu ya binadamu na ulimwengu anamoishi. Kwake, vuguvugu hili la ubwege linaibuka kutokana na hangaiko la binadamu juu ya hamu ya kujenga picha za ukweli juu ya ulimwengu na wazo la kuamua kama dhana zinazodhihirika zinaelezea ukweli.

Fasihi ya ubwege hujaribu kubainisha ukweli juu ya maisha ya binadamu ulimwenguni. Webb (1972:23) anasisitiza kuwa, fasihi ya kiubwege ni dhihirisho la hali ya fikra za binadamu. Binadamu anajaribu kutafuta ukweli, lakini fikra zake zinamfanya hasiupate. Drama ya kiubwege hukusudia kuonyesha kushindwa kwa binadamu kujielewa yeye pamoja na hali yake ulimwenguni.

### 2.5.3 DHANA NA SIFA ZA DRAMA YA KIUBWEGE

Drama ya kiubwege ni aina ya drama ambayo hujitenga au hujaribu kuvuruga vipengele vya kijadi vya uandishi wa drama. Tangu enzi za Aristotle, tamthilia (drama) zimebainisha utaratibu fulani wa uandishi. Drama ya kiubwege huvunja utaratibu huo, sawa na kukaidi hali ambazo hutambuliwa kama za kiuhalisia.

Esslin Martin, mhakiki sifika wa tapo hili, ametoa muhtasari wa hali ya tamthilia za kiubwege<sup>5</sup>. Anaeleza kuwa ikiwa tamthilia ni lazima iwe na hadithi inayofululiza vizuri, tamthilia za kibwege huwa hazina hadithi au ploti inayoweza kuelezewa kikamilifu; kama hadithi nzuri huamuliwa kwa usawiri na umotishaji mzuri wa wahusika wake, hizi mara nyingi hukosa wahusika wa kutambulika vyema na badala yake hubainisha wahusika batili tu. Kama tamthilia ya kawaida inapaswa kuwa na maudhui pevu, hizi hukosa muwala wa maudhui. Tamthilia za kibwege huwa na ndoto au ruwaza nyingi bila kumulika hali ya maisha kiuhalisia. Kawaida, tamthilia huwa na umantiki wa mazungumzo kati ya wahusika, ilhali za kibwege hubainisha utengano, upweke wa mazungumzo.

Baadhi ya waandishi wa drama ya kiubwege na ambao wameandika tamthilia zinazobainisha mtazamo wa Esslin Martin, ni Eugene Ionesco, *The Killer*, *The Chairs*, *The Lesson*, *Rhinoceros*. Samwel Beckett, *Waiting for Godot*, *End game*, Fernando Arrabal, Arthur Adamov, Harold Pinter na Edward Albee ambaye ameandika *The Sandbox*..

Kuhusu uigizaji wa drama ya kiubwege, Anderson (1972:2) anasema:

Hadhira wanakumbwa na visa vingi visivyo na muwala, na matukio ya mchezo hayana maana kisaikolojia na pia katika muktadha wa matendo ya tamthilia. (Tafsiri yetu)

Hali hii humpatia binadamu picha halisi juu ya maisha yake yasiyo na utaratibu wowote ulimwenguni.

Matukio ya tamthilia za kiubwege hubainika kimzunguko. Matumizi ya duara ni kigezo muhimu katika aina hii ya drama. Esslin (1961:365) anaeleza:

Nyingi ya tamthilia za kiubwege huwa na  
muundo wa kiduara, ambapo zinaisha  
vile ambavyo zilianza; zingine huendelezwa  
kwa hali iliyotangulia. (Tafsiri yetu)

Hali hii ndiyo hudhirika katika tamthilia za Beckett na Ionesco. Katika *End game* (1958), hamu ya Clov kutaka kutoka nyumbani kwa Hamm inajitokeza kuanzia mwanzo hadi mwishoni mwa tamthilia, kwa vile Clov haondoki. Katika tamthilia nyingine ya Beckett *Waiting for Godot* (1956), wahusika Estragon na Vladimir wanaendelea kumngoja Godot mwanzoni na pia mwishoni mwa tamthilia. Eugene Ionesco katika *Rhinoceros* (1959) anatupatia hali ambapo mhusika Berenger anaendelea kuzidiwa na woga wa kubadilika kuwa Rhinoceros. Hali hii pia inabainika katika *The Lesson* ambapo wahusika, Professor na Pupil wanabadilika kadiri mchezo unaposonga mbele hadi kiwango cha mwanafunzi, Pupil, kuzidiwa kabisa na hapo kuuawa na Professor.

Tamthilia hizi ni kiwakilishi cha hali ya fujo inayojibaini ulimwenguni. Wahusika wa tamthilia za kiubwege ni vibonzo. Mazungumzo yao hayana umantiki na hivyo mawasiliano hutatizika. Wahusika hawa hawawakilishi sifa halisi za binadamu bali huwakilisha dhana za kidhahania. Anderson (1972:2) anafafanua hali hii anaposema:

Wakati mwingine wahusika hawa hubadilisha  
hali zao, mazungumzo yao yamejaa ukinzano;  
hukataa kukubali yaliyomo ulimwenguni na  
badala yake kuamini matukio ya kidhahania.  
Maelezo yao juu ya hali na dhana  
mbalimbali hukosa maana. (Tafsiri yetu)

Hali hii hujitokeza katika tamthilia za Ionesco. Katika *Rhinoceros*, wahusika wanabadilika na kuwa Rhinoceros. Wahusika katika *The Chairs* sawa na wale katika *Amezidi* (S. A. Mohamed), wanaamini vitu vya kidhahania – vitu ambavyo hawana. Kwa mfano hawana viti, watumishi, wageni na utajiri. Katika *The Lesson*, Professor anashindwa kueleza na kufafanua kikamilifu dhana na nadharia za hisabati, na hivyo kumtatiza mwanafunzi wake, Pupil.

Katika jukwaa, wahusika wa drama ya kiubwege hukosa motisha katika matendo yao. Wanasawiriwa kama watu waliotekwa na hali fulani bila kuwa na uwezo na kujinasua. Ni wahusika waliojitenga miongoni mwao na kutoka kwa hadhira. Hadhira mara nyingine hushindwa kuwatambua au kuwalaumu wahusika hawa kutokana na vitendo vyao. Usawiri huu wa wahusika hudhamiria kubainisha hali duni na ya kukatisha tamaa ya binadamu ulimwenguni.

Kigezo cha wakati nacho husaidia kuendeleza hali ya ubwege. Wahusika huonekana kutojua vyema nyakati za vitendo vyao. Katika *Waiting for Godot*, Vladimir na Estragon hawawezi kukumbuka kama walikutana na Godot au la, na lini. Hawajui hata mahali walipo wala kutambua vizuri kinachoenlelea. Vitu vinatokea tu kama katika ndoto.

Kwa ujumla, drama ya kiubwege hudhamiria kusawiri na kudhihirisha bayana, hali duni ya maisha ya binadamu. Kwa muda mrefu, drama imetumiwa kufumba macho ya binadamu asiweze kuona ukweli wa unyonge wake ulimwenguni<sup>6</sup>. Drama ya kiubwege iliibuka kurekebisha hali hiyo kwa kuweka ukweli mbele ya binadamu.

#### **2.5.4 MIELEKEO YA DRAMA YA KIUBWEGE**

Drama ya kiubwege ni tapo mojawapo la matapo ya drama yanayotambulika hivi sasa. Aina hii ya drama inaweza kugawanywa katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni lile linalowakilishwa na Albert Camus na Jean-Paul Sartre. Hili ndilo kundi la awali zaidi katika drama ya kiubwege. Aina ya pili ni kundi linalojumuisha waandishi kama Eugene Ionesco na Samwel Beckett. Hili linawakilisha drama ya kiubwege ya kisasa ambayo hutambuliwa kama *Theatre of The Absurd*. Ni kundi ambalo limetia misingi imara na yenye uasili zaidi kuliko kundi la kwanza la Camus na Sartre.

Kundi la kwanza lilijikita zaidi katika matumizi ya yaliyomo katika tamthilia kudhihirisha dhana ya ubwege. Waandishi hawa, walitumia muundo wa kiakili kusawiri hali duni, ya kiubwege ya binadamu. Tamthilia zao hueleweka na hubainisha maana kupitia tendo la kufikiri. Kazi zao za awali hazibainishi ubwege kamili. Kwa mfano tamthilia *The Misunderstanding* na *Caligula* za Camus, zina ploti nzuri inayofululiza. Lakini kazi zake za baadaye kama *State of Siege* na *The Just Assassins* zina vipengele vingi vya kiubwege ambavyo vimeimarishwa. Kwa mfano, ukosefu wa muwala na umantiki katika ploti na usawiri wa wahusika ni bayana.

Waandishi wa kundi la pili hutofautiana na wa kwanza kwa vile tamthilia zao zimepevuka zaidi kiubwege. Kazi zao huonyesha picha halisi ya kukata tamaa kwa binadamu kutokana na hali duni na maisha yenye mateso katika ulimwengu katili usiomjali. Tamthilia za Beckett *Waiting for Godot* na *End game* pamoja na za Ionesco *The Lesson*, *The Chairs*, *Rhinoceros* na *The Killer* kwa mfano ni kazi ambazo zimeafiki sifa muhimu za ubwege, kama ambavyo tumekwisha zitaja na kuzifafanua. Tamthilia za kundi hili la pili hutumia vigezo vya yaliyomo na mtindo katika kupitisha maana. Hawategemei yaliyomo peke yake kama kundi la kwanza. Kuhusu hali hii, Esslin (1961:6) anasema:

... Sartre au Camus huelezea yaliyomo kwa  
kutumia kaida za kale lakini drama ya kiubwege  
ya kisasa hupiga hatua mbele katika jaribio la  
kupata muumano kati ya dhana zake za kimsingi  
na maumbo mbalimbali ambayo huelezea dhana hizi.  
(Tafsiri yetu)

Ingawa kuna haya makundi mawili, drama ya kiubwege kwa ujumla huongozwa na wazo la kuwoko kwa binadamu ulimwenguni, maisha yake duni na yasiyo na maana katika ulimwengu huo katili na wa kukatisha tamaa. Kitchin (1966:31) anathibitisha wazo hili anaposema kuwa haja kubwa ya drama ya kiubwege ni kuwoko kwa binadamu katika hali ya kukata tamaa na isiyo na maana ulimwenguni.

### 2.5.5 DRAMA YA KIUBWEGE BARANI AFRIKA

Uandishi wa drama ya kiubwege ni mpya katika eneo hili la Afrika hasa Afrika Mashariki. Hata hivyo, ni vyema kutaja kuwa sifa za ubwege zimekuweco katika fasihi hasa katika fasihi simulizi. Baadhi ya elementi zinazoendeleza ubwege kama wahusika wenye sifa za wanyama, motifu za kindoto na uchechele ambazo husaidia wahusika kujibadilisha mara kwa mara, zimekuweco kwa muda mrefu katika fasihi simulizi ya Kiafrika.

Kimaandishi, waandishi wa tamthilia za kiubwege Afrika Mashariki na hata Afrika nzima sio wengi. Hali hii inatokana na tofauti za kimazingira kati ya waandishi wa Kimagharibi na wale wa Kiafrika. Mazingira yaliyoendeleza hali ya ubwege kama vile Vita Vikuu vya Dunia, hayakuathiri Waafrika moja kwa moja kinyume na ilivyokuwa, kwa mfano Uropa. Hivyo basi, waandishi wa Kimagharibi mfano Sartre na Camus waliathiriwa mapema na kuandika tamthilia za kiubwege. Camus na Sartre walishiriki vita hivyo kama wanajeshi.

Baadhi ya waandishi wa tamthilia za kiubwege barani Afrika ni Athol Fugard ambaye amechapisha *Sizwe Bansi is Dead*, *The Island*, *Nongogo*, *The Coat*, *The Blood Knot*, *No Good Friday*, Robert Serumaga kupitia tamthilia kama *The Elephant* na *Majangwa and a Play*. Said Ahmed Mohamed naye ameandika *Amezidi*, tamthilia tunayoishughulikia.

### 2.6 HITIMISHO

Katika sura hii, tumeshughulikia historia ya drama, maendeleo ya tamthilia ya Kiswahili, na tanzu za drama. Tumetoa maelezo na mifano ya aina mbalimbali za drama zikiwemo tanzia na futuhi. Tumebainisha kwamba, ingawa tanzu hizi mbili ni kuu, kuna mikondo mingine ya drama ambayo ni muhimu pia. Drama ya kiubwege ni aina mojawapo ya zile ambazo zimeibuka miaka michache iliyopita na kuathiri uandishi wa fasihi. Tapo hili la uandishi wa drama, ubwege, ni ngeni na halijashughulikiwa ipasavyo katika uandishi na uhakiki wa fasihi. Tumeshughulikia drama ya kiubwege kwa mapana ili kusaidia wasomi na wapenda fasihi kuelewa vyema aina hii ya drama. Aidha, tumetoa mifano kadhaa ya waandishi wa Kiafrika na wa Kimagharibi wanaotambulika katika tanzu mbalimbali za drama. Uandishi wa tamthilia unaendelea kupanuka na hivyo kupata mielekeo mingi.



## TANBIHI

---

- <sup>1</sup> Bertoncini, E. Z. (1989) *Outline of Swahili Literature: Prose, Fiction and Drama*  
Leiden, E. J. Brill. Uk. Ix
- <sup>2</sup> Wafula, R. M. (1999) *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake.*  
Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi. Uk. 5
- <sup>3</sup> Camus Albert (1984) *The Myth of Sisyphus*  
Penguin, London uk. 3-4
- <sup>4</sup> CruickShank, J. (1958) *Albert Camus: The Literature of Revolt*  
Oxford University Press, London  
Uk. 40-43
- <sup>5</sup> Esslin Martin (1974) *The Theatre of the Absurd*  
Methuen, London. Uk. 3-4
- <sup>6</sup> Kama 3 hapo juu Uk. 5

### 3.0 SURA YA TATU

#### 3.1 UTANGULIZI

Katika sura hii tumedhamiria kuonyesha jinsi tamthilia ya *Amezidi* ilivyoathiriwa na mkabala wa uandishi wa kiubwege. Sura hii imejikita katika vipengele mbalimbali vya kimaudhui vikiwemo dhamira ya tamthilia, suala la Mungu, suala la historia, elimu na mkengeuko. Tumevihakiki na kuvichanganua vipengele hivi na vingine zaidi ili kubainisha kiwango cha ubwege katika tamthilia hii.

#### 3.2 DHAMIRA YA TAMTHILIA

Kimsingi, fasihi ya ubwege huwa na dhamira ya kuonyesha ubatili wa matendo ya binadamu ulimwenguni. Hususan, hutumia wahusika vibonzo ambao hukosa uwezo wa kujielewa na kufikiria licha ya kutekeleza yasiyo na maana. Binadamu husawiriwa kama kinyago kisicho na uwezo wa kubadilisha hali yake. Muhimu kwa binadamu ni kukaa na kusubiri kifo; kifo ambacho ndicho hatua ya mwisho ya maisha yake.

Dhamira ya Mohamed, katika *Amezidi* kwa maoni yetu haiafikiani kwa kiasi kikubwa na dhamira ya aina hii. Mwandishi huyu yaelekea anasukumwa na dhamira ya namna ambavyo bara la Afrika limenyonywa na kuathiriwa vibaya na mataifa ya Kimagharibi yaliyoendelea. Wafula (1999:75) anasema:

Tamthilia ya *Amezidi* inazungumzia ukosefu wa maendeleo barani Afrika. Mwandishi anadai kwamba mataifa ya kisasa barani Afrika yamejengwa kwa uigaji kikasuku wa teknolojia za Kimagharibi, ufisadi na unafiki.

Hali hii ni ya kiuhalisia zaidi na inapingana na mtazamo wa kiubwege. Madhumuni ya Mohamed, yaelekea ni kuzindua na kuhamasisha viongozi wa bara hili na raia wake kwa ujumla kuwa wazalendo kwa kulipenda bara lao na kujitolea kulifufua kimaendeleo. Nchi nyingi za bara la Afrika ziko huru lakini bado zinategemea misaada kutoka ng'ambo. Mtu au nchi huru ni ile inayoweza kujitegemea na aghalabu kukimu haja zake za kimsingi. Tunapooname na Zidi wakiomba vitu vingi chakula

kikiwemo, tunapata picha ya nchi maskini kabisa na inayoyumbayumba. Ni dhahiri kwamba, nchi nyingi za Kiafrika bado hazijimudu kwa mahitaji mengi na hivyo huwa zinategemea misaada na ruzuku za kigeni.

Ame na Zidi wanawakilisha viongozi wa Kiafrika katika nyadhifa mbalimbali. Tunawapata wakipokea hongo, paja la nyama ya ng'ombe, madawa na kadhalika. Tunaambiwa:

Ame: Umeshapeleka maombi ya msaada huko  
Umoja wa Mataifa? Au kuomba ruzuku  
nchi za Magharibi, yaani EC?

Zidi: Kwani kazi yangu kuomba mimi?  
Kwa nini unaniuliza mimi suala hilo?

Ame: Nimwulize nani basi?

Zidi: Unamjua.

Ame: Wewe... Mimi?

Zidi: Kwenda huko.....

Ame: Pengine tukiomba sisi, sasa tutapewa,  
Maana yeye ameomba mno! (uk. 9)

Inabainika hapa kuwa sio nchi moja tu inayoomba na kutegemea misaada, bali ni nchi nyingi. Upokeaji huu wa misaada hudhoofisha heshima na uhuru wa Mwafrika. Tunaona mtafaruku unaojiri kati ya Ame na Zidi kutokana na kupokea msaada wa paja la nyama ya ng'ombe kutoka EC. Hali hii ni dhihirisho kwamba, mataifa ya Ulaya hufurahia michafuko katika bara la Afrika. Mataifa hayo hutumia njama nyingi za kisiri ili kuendeleza uhasama baina ya nchi za Kiafrika ili kwa njia moja au nyingine waendeleo kuzitawala; kweli wanatenga na kutawala chambilecho wahenga. Katika bara la Afrika, mfano mzuri wa nchi hizi ni Somalia, Rwanda, Angola na Kongo.

Tamthilia katika onyesho la kwanza, inajaribu kueleza hali na uhusiano wa kiuchumi baina ya bara la Afrika na la Ulaya. Ame na Zidi wanajadiliana juu ya mihogo iliyovunda, isiyofaa na jinsi ya kuitayarisha ili iweze kulika. Baadaye tunawaona wakishindwa kuikata na kuichoma, na hivyo kulazimika kuila tu kinyama.

Maisha ya binadamu kulinganishwa na ya wanyama ni kigezo cha ubwege. Mwanadamu amepotea njia na kujitoma katika ulimwengu wa kinyama. Haya ni maisha mabaya, machafu mithili ya kiumbe wa kiubwege. Wanyama hawana uwezo wa kuboresha maisha yao sawa na Ame na Zidi ambao tunaambiwa hawana kisu wala kibiriti ambacho kingewasaidia kutayarisha chakula chao. (uk. 10-11)

Hata hivyo, hali hii ni fumbo kuhusu hali mbaya ya biashara kati ya mataifa ya Ulaya na ya Kiafrika. Waafrika, inabainika, wanahitaji vitu vingi zaidi kutoka Ulaya huku nchi za Kimagharibi zikisawiriwa kama zilizoendelea sana na kujitosheleza kimahitaji. Aidha, Waafrika wanasawiriwa kama watu wajinga ambao hawataki kufikiria na kujizatiti kuvumbua vitu vyao. Kwao, muhimu ni kulala, kuzembea kazi na kumtegemea Mzungu kwa yote. Zidi anasema:

Kwanza yanaumiza kichwa, pili, utafikiri kipi wewe  
Mwaafrika ambacho Wamarekani, Waingereza, Warusi,  
Wafaransa na Wajerumani hawajakifikiria? Tatu, si  
vipo tu vitu vyenyewe duniani vimeenea? Na sisi  
tunanunua tu. Huu ulimwengu wa biashara ati! (uk. 10)

Hii ni hali inayobainika bayana hata hapa nchini mwetu, ni hali ya kiuhalisia. Ubwege umo katika maisha ya Waafrika (Ame na Zidi). Wahusika hawa hawana uwezo wala nia ya kutekeleza wajibu wao wa kikazi licha ya kupatiwa mazingira yenye rutuba, na malighafi muhimu.

### 3.3 SUALA LA MUNGU

Kulingana na Biblia takatifu<sup>1</sup>, Mungu ndiye aliyetuumba sisi na vitu vyote vilivyomo ulimwenguni. Pia aliumba mbingu na ardhi, na nguvu zake hazina kifani. Suala la kuwepo kwa Mungu pamoja na uwezo wake hutiliwa shaka na tapo la ubwege. Kiudhanaishi, fikira za Mungu humjia mtu baada ya kushindwa kukabiliana na ugumu wa maisha yake.

Binadamu anaposhindwa kutekeleza wajibu wake ulimwenguni, huteseka na kukata tamaa ya kuishi. Hivyo basi, kwa kutarajia usaidizi, anaota na kufikiria juu ya nguvu fulani zenye uwezo wa kumwokoia, uwezo unaoshinda unyonge wake, Mungu.

Said Ahmed Mohamed, anamtambua Mungu katika tamthilia yake, *Amezidi*. Ubwege kikawaida, hautilii maanani suala la Mungu. Katika kianzio cha mwandishi- Wimbo wa Mzee, tunaambiwa:

...Nimeishi kusikia mengi, pia nimedanganywa  
kwa mengi. Mwanzo nilibeba dunia zito  
'kadhani ni mzigo alionipa Mungu. Nikawana  
kukidhi matakwa yake.

(uk. 2)

Usemi huu ni sawa na ujumbe tunaopata katika Biblia kuhusu watu wa Mungu kama Abrahamu, Jeremiah, na Musa ambao walitembelewa na Malaika wa Mungu na kupatiwa majukumu ya kutekeleza. Hivyo basi, Mzee huyu si mjumbe wa kidhanaishi.

Aidha, Ame na Zidi, hapa na pale wanakimbilia fikira za Mungu. Wanapokumbwa na haja ya kufanya kazi au mateso ya njaa, wanajaribu kukwepa kwa kusingizia msaada kutoka kwa Mungu. Katika onyesho la kwanza, tunaambiwa:

Zidi: Lakini haina haja kuomba,  
si tuna mhogo wetu?

Ame: Mhogo au riziki ya siku moja?

Zidi: Sikiliza bwana, kesho kuna Mungu!

Ame: Na bora tuanze kuula hasa,  
maana kesho kuna Mungu...

(uk. 9)

Tumaini la neema za Mungu linachomoza pia katika Wimbo wa Mtoto Asiyezaliwa. Mtunzi anatupa dhana inayopatikana katika vitabu vitakatifu na ambayo husisitizwa miongoni mwa Wakristo na Waislamu; dhana ya kupigwa kwa baragumu siku ya kiyama itakapofika. Siku hiyo ikifika, inasemekana, watu wote wataletwa mbele ya Maulana kujibu mashtaka. Tunaambiwa pia kuwa, hata wafu watafufuliwa na wagonjwa wataponywa ili kushuhudia siku hiyo. Ujumbe huu wa kibibilia umo katika kimalizio cha mwandishi. Anasema:

Huo mwisho ukifika maiti wote watafufuka  
vipofu wataona, viziwi watasikia  
mabubu watasema, vichaa watatengamaa  
wajinga 'tarevuka na wal'olala 'taamka  
Baragumu 'tapolia.

(uk. 86-87)

Mohamed kwa kutupatia hali hizi za kidini, yaelekea amekaidi kanuni za uandishi wa drama ya kiubwege. Wilson na Goldfarb (1991:402) wanasema:

Wana-udhanaishi wanaamini kuwa Mungu  
hayuko na hivyo binadamu yumo pekee  
katika ulimwengu katili. Kitendo muhimu  
ambacho binadamu anaweza kufanya ni  
kukubali mamlaka juu ya yale ayatendayo  
ulimwenguni.

(Tafsiri yetu)

Tamthilia ya *Amezidi* imekiuka kigezo hiki cha udhanaishi. Waandishi wa kiubwege hujaribu kushawishi binadamu kutomtegemea Mungu kwa vile hana chotote cha maana kwake. Wahusika katika tamthilia hii yabainika wana matumaini ya kupata wokovu kutoka kwa Mungu. Hali hii inachomoza katika onyesho la saba:

Zidi: Huyo! (Anafutuka na kukasirika)

Anarejea kule kwenye madda na shadda,

Kwenye varange na magumbe... vitendawili...

vitendawili... vitendawili kila siku...

Vitendawili vingi umevimepata wapi wewe

Mari mtu wa kawaida, hohe-hahe, bwege, muishi

madongoporomoka, mwanamke wa Mungu hapo ulipo!

Mari: Ulimwengu!

Zidi: Umefanyaje?

Mari: Umetufunza... sisi... sisi mabwege, sisi waishi

Madongoporomoka, sisi wanawake wa Mungu

(uk. 59)

Mwandishi anaelekea kutupa wazo kuwa, kwa vile Mari amekengeuka sana, anahitaji nguvu zinazoshinda uwezo wa Zidi kumbadilisha; nguvu hizo sio za kibinadamu bali ni za Mungu. Hali kama hii hujitokeza pia katika onyesho la kumi baada ya kifo cha Zidi. Tunapata mazungumzo yafuatayo:

Ame: Aaaa (Anakamata tumbo na kutoa macho)

Sauti: (Sauti ya Zidi) Nini?

Ame: Tumbo... tumbo... tumbo kama lile lako...

Yallah, Mungu wangu... (uk. 83)

Baada ya kukumbwa na shida na mateso ya ulimwengu, na kuathiriwa vibaya na uhitaji wa misaada, Ame anajuta. Mhusika huyu amegundua kwamba hawezi kujitoka katika tope la usumbufu ambamo amejilingiza. Hivyo basi anaomba Mungu amsaidie ili aweze kupata nafuu maishani.

Hata hivyo, yaelekea Mungu hasikii maombi ya waja wake. Maombi ya Ame hayakujibiwa kwa vile baadaye anaendelea kuteseka na hatimaye kufa. Tendo hili linaoana na imani ya kidhanaishi kuwa, binadamu ametupwa katika ulimwengu dhalimu unaomtesa na kumwangamiza bila huruma yoyote na Mungu hana uwezo wa kumwokoia binadamu.

Katika *Gamba la Nyoka*, tunapata hali kama hiyo tunapoambiwa:

Ndugu wanakijiji, wazee walisema  
'Mungu' anakulinda na wewe unajilinda.  
Kitendo ambacho tumekata shauri kutenda  
ni cha kishujaa lakini cha hatari. *Tusitegemee*  
*tu kirwa Mungu yupo. Tujiandae...*  
(msisitizo ni wetu) (uk. 19)

Kiubwege, dini ni chombo cha kumtuliza na kumliwaza binadamu anayeteswa na ulimwengu. Dini hutumiwa kumpa binadamu matumaini kuwa siku zijazo majonzi yake yataisha kwa kupata neema kutoka kwa Mungu.

Irungu (1999) <sup>2</sup> anadai kuwa binadamu hapaswi kuketi tu na kutegemea kuwa Mungu yupo bali bidii na kufikiri kutampeleka hatua mbele katika kutatua masuala yake. Kezilahabi, katika *Rosa Mistika* anaibeza dini. Rosa anasema:

Wokovu maana yake nini?  
Wokovu! Wokovu gani? Kama  
kuna moto basi nitakwenda. (uk. 59)

Ni dhahiri kuwa dini imeshindwa kutoa jawabu sahihi kwa maswali ya binadamu juu ya maisha yake. Ame alishindwa kupata usaidizi wa Mungu (uk. 83) na hivyo akaangamia. Naye msimulizi katika novela ya *Mzingile* anatuambia kuhusu padri Mzungu:



Katika ulevi wake alivunjavunja baadhi  
ya masanamu kanisani. Alisikika akipiga  
kelele. 'Mungu gani wewe!' Umeniaibisha  
mbele ya watu weusi. Alipoanza kuchanganya  
gongo na mvinyo, masista walimkimbia.

(uk. 20)

Beckett katika *Waiting for Godot* anaelekea kuunga mkono wazo la uhafifu wa Mungu katika maisha ya binadamu. Binadamu anatumia wakati wake mwingi kuomba na kutarajia baraka za Mungu bila mafanikio. Anawachora wahusika wake Vladimir na Estragon kama vibonzo wasiotenda lolote la maana, ila kumngojea Godot. Hali hii inabainika kutoka mwanzo hadi mwisho wa tamthilia. Godot, tunaweza kumchukulia kama Mungu wa aina fulani ambaye wahusika walikuwa na matumaini kwake ya wokovu. Kutofika kwa Godot, ni dhihirisho la mashaka yanayotiliwa kuwoko kwa Mungu na uwezo wake.

Roubiczek (1964:39) anaeleza kuwa, Nietzsche mara kwa mara alitoa kauli kama 'Mungu alikufa, tumemwua Mungu, Mungu amekufa'. Friedrich Nietzsche, ni mmoja wa watetezi wakuu wa nadharia ya udhanaishi. Alipinga utukufu uliopatiwa dini na Mungu. Aidha, aliandika<sup>3</sup> juu ya mwendawazimu ambaye siku moja mchana, aliwasha taa na kukimbia hadi sokoni huku akipiga kelele kuwa 'ninamtafuta Mungu'.... na watu waliokuwoko wakaangua kicheko.

Mawazo haya yanaunga mkono msimamo wa tapo la ubwege juu ya Mungu. Tamthilia ya *Amezidi* kwa kiasi kikubwa haijafuata mwelekeo huu. Mohamed kupitia wahusika wake inabainika anamtambua Mungu ingawa haamini juu ya uwezo wake wa kumwoko binadamu kutoka kwa usumbufu wa ulimwengu.

### 3.4 ELIMU NA MKENGEUKO

Wazo la mkengeuko ni kipengele muhimu katika nadharia ya udhanaishi. Wahusika katika tamthilia ya *Amezidi* wamesawiriwa kama wapotevu kutokana na athari ya elimu

ya kigeni. Mari amevaa wigi, ishara ya maigizo ya kigeni, mkengeuko. Hali hii pia inapatikana katika *Waiting for Godot*. Lucky amevaa kofia. Kiubwege, wigi na kofia ni vitu vinavyoashiria kichwa na fikira zake. Mawazo na nafsia ni vigezo maalum katika falsafa ya udhanaishi.

*Amezidi* ni kejeli kwa hali ya Mwafrika kujiwekea viwango vya ubora ambavyo vinaenda kwa misingi ya Kizungu. Ame anapokabiliwa na Mkaguzi (Zidi), anaandaa viburudisho vya kuonyesha ustaarabu wake. Hata lugha yake inaonyesha kuathiriwa kwake:

Ame: Ngoja nikuburudishe kidogo... hutaki

Burudani wewe?

Zidi: Burudani!

Ame: Entertainment yaani!

Zidi: Ala! Tumejia entertainment hapa?

Kazi tu...

Ame: Ngoja...

Zidi: Nini?

Ame: Whisky, Brandy, Vodka, Beer, Champagne?

Zidi: We lete tu.....

Ame: Vizuri...

(uk. 49)

★ Kiingereza ni lugha ambayo Waafrika wengi wanaipenda. Baada ya kujinyakulia uhuru, waliithamini na kujionyesha kwayo kwa madaha. Mwafrika aliathiriwa sana na tamaduni za Mzungu na hivyo kuiga matendo na tabia za Kizungu. Ame na Zidi ni mfano wa Waafrika wajinga wenye tamaa ya vitu vya Kizungu huku wakidharau vyao.

Mari naye hakuachwa nyuma. Licha ya kuvaa wigi, tunamwona akiwa amebadilika kilugha, kimavazi na hata kimwendo. Zidi anamwambia:

Sikutambui, Mari... umebadilika... siye  
tena Mari mtarambura msichana wa  
kijiji cha mjomba wangu; kile kijiji cha  
Mpashambi... siye tena Mari mwenye  
ngozi ya ganda la fuu na gome la mpingo...  
sasa ni Mari wa jijini na ngozi ya kukoboa!

(uk. 61)

Mari anapenda ya Kizungu, kwa vile ya Kiafrika ameshayashiba. Inabainika kuwa ngozi ya Mari imebadilika, amejipodoa. Hapendelei tena ngozi nyeusi ya Mwafrika, anataka kuonekena Mzungu. Ameichujua na kuichubua ngozi yake ili iwe kama ya Mzungu. Tukitazama usemi wake, ni dhahiri kuwa anaiga na kuthamini lugha ya kimombo:

Mari: (Kwa mapenzi) Mmmh!

Zidi: Moyo wangu...

Mari: (Kwa mapenzi zaidi) Yes!

Zidi: How do you do?

Mari: All right! (uk. 60)

Huu ni mkengeuko. Kupitia kwa Mari tunapata picha ya elimu inayokatisha tamaa. Amemsawiri kama mhusika aliyekengeushwa na mafunzo ya kikoloni. Ukengeushi wa Mari unaendelea kubainika anaporinga kuwa Zidi, mpenzi wake hana lolote la kumfurahisha. Tunaambiwa:

Mari: Na mapambo, mavazi na urembo wa  
Mwanamke kama mimi si ya hapa... si  
ya fedha za madafu; lazima yatoke States  
Canada, Japan, France, Italy au West Germany!

Zidi: (Kejeli) Alaaaa! Nimechelewa kutambua!

Mari: ...Unanichezesho kindumbwendumbwe charira,  
Kikojozi kakojoa na nguo kaitia moto!  
Ukanipa pasi kunipa vitu viliopo visivyokuwepo!

Zidi: (Tashtiti) Alaaa!

Mari: Enhe sasa nitazame, nimekuja makusudi unione! (uk. 60)

Usemi wa Mari ni usemi uliojaa kiburi na dharau kwa Zidi na Waafrika kwa ujumla. Ni mhusika ambaye kwake tamaduni za Kiafrika ni ujinga na hauna ustaarabu. Ni dhahiri kuwa kwake titi la mama si tamu. Aidha, Mari amemea mti msowera – mti ambao tunaambiwa humo moyoni mwake.

Zidi: Mti...

Mari: Mti... mti moyoni mwangu!

Zidi: Usiogope, kabisa usiogope...

Mari: Kwa nini?

Zidi: Kwa sababu mti wenyewe msowera. (uk. 57)

Huu ni mti wa ughaibu na ambao unamtenga Zidi, mpenziye. Ni mti wa kishetani, wa kupandwa na madaha, na mtu kupuuza wenzake. Kuathirika kwa Mari kunamwingilia Zidi baadaye, kwani naye tunaambiwa ameota mti huo huo.

Mari: Mti!

Zidi: Wapi?

Mari: Moyoni mwako!

Zidi: (Mshangao tena) Mti!

Mari: Usiogope.

Zidi: Kwa nini?

Mari: Kwa sababu mti wenyewe mjinga.

Zidi: Mjinga?

Mari: Mjinga enh, mjinga mwangamizi!

(uk. 58-59)

Ni wazi kuwa wote, yaani Mari na Zidi wamekengeuka. Hali hii inawafanya wasitambuane wala kuthaminiana. Inabainika pia kuwa uamuzi wao wa kutengana ni ishara kwamba wametambua kiini cha upotovu wao. Hii ni hali ya ubwege. Mwandishi anarudiarudia na kuisitiza jambo lilelile bila kubainisha umantiki wake.

Elimu katika ulimwengu wa mabwege hukosa misingi thabiti ya kijamii. Mara nyingi huwa ni elimu ya kuigwa na ambayo haisaidii binadamu kuboresha maisha yake, bali husaidia katika kumwagamiza zaidi.

Katika tamthilia ya *Amezidi*, Mwalimu na Wanafunzi wake wanalala darasani na kati yao, hakuna anayeweza kumwokoza mwenzake kutoka janga la kutojua. Ni hali ambayo inazidi kubomoa nchi ya Amezidi kwa kukosa viongozi wenye ujuzi wa kuleta maendeleo. Hali hii hukaribiana na tunayopata katika tamthilia ya Ionesco, *The Lesson*. Mhusika Pupil, anapatiwa elimu ambayo haisaidii kukua wala kuimarisha maisha yake, elimu anayopata inamnyooshea mkono wa maangamizo, kifo. Mwandishi anatupatia elimu isiyo na maana kwa jamii ndiposa Pupil, anauawa na Professor.

Katika onyesho la nne, tunaonyeshwa dhahiri matatizo yanayoikumba sekta ya elimu barani Afrika. Nchi ya Amezidi, inafuata mfumo wa elimu ya kigeni ambao haufungamani na mazingira yake. Tunaambiwa na Mwanafunzi.

Hivi... hivi baada ya kukariri  
mawazo ya Archimides kwa miaka mingi,  
kwa nini hatujaweza kuunda nyambizi?

(uk. 30)

Ni swali ambalo viongozi wa Kiafrika wanapaswa kujibu, lakini hata wao hawana mwelekeo, ni mabwege. Mwalimu hajui jibu lake ndiposa wanafunzi pamoja naye, wanalia na kucheka kuashiria mtafaruku wa mtazamo wa elimu hii. Hapa tunapatiwa Mwalimu ambaye tunatarajia amepata mafunzo ya kutosha kuelekeza wanafunzi, lakini anashindwa kutekeleza wajibu wake. Anafundisha mada ambayo haelewi na kushindwa kujibu maswali ya wanafunzi. Ni mwalimu asiyefuata maadili ya ualimu. Anasinzia darasani kuonyesha ubwete wake. Aidha, anaingia darasani na bakora ndefu. Labda bakora ni silaha yake ya kuogofya baadhi ya wanafunzi wasimwulize maswali na kumsumbua kichwa. Mazingira ya darasani yanachukiza:

Tendo limo fikirani... pangoni...  
tendo la shuleni. Zidi ni mwalimu,  
kaketi mbele ya meza ambayo haionekani.  
Pana ubao na chaki ambavyo pia havionekani.  
Ame (mwanafunzi) ameketi kwenye deski  
Lisiloonekana pia. Kuna wanafunzi wapatao  
sabini. Pia hawaonekani ila Ame tu!  
Mwalimu Zidi anasinzia huku darasa limejaa  
zogo la wanafunzi...kitambo...  
Kisha kengele inasikika kulia... mwalimu  
Zidi anashtuka kutoka usingizini.

(uk. 29)

Tazama darasa hili. Ni darasa la wanafunzi sabini watundu, wenye zogo. Pia ni darasa la somo la Fizikia lenye mwalimu anayesinzia na asiyejua wala kuelewa analofundisha. Ni darasa lisilo na mwelekeo wala matumaini ya kujifundisha mengi, ni mazingira ya kiubwege.

Elimu ya aina hii ni jazanda ya mifumo ya elimu ya bara la Afrika ambayo inaendelea kukuza njama za Mzungu. Nchi nyingi za Kiafrika bado zinaiga mielekeo ya elimu ya kigeni. Uchunguzi unabainisha kuwa takriban nchi zote za bara hili zinatumia lugha ya kigeni kama lugha rasmi au lugha ya taifa. Hali hii ni sawa na mkengeuko ambao Mari katika *Amezidi* anasawiri. Bado wananchi wengi wa Afrika wanazionea fahari lugha za kigeni kama Kiingereza, Kifaransa na Kijerumani sawa na afanyavyo mhusika Mari:

Mari: Yes!

Zidi: How do you do?

Mari: All right! (uk. 60)

Hizi ni lugha ambazo zinaendeleza ukoloni na tamaduni za Kimagharibi. Tunaambiwa na Mwalimu:

Vizuri... vizuri... bas... bas... vizuri,  
unaijua, unaijua – (Anaandika kwenye  
ubao usiokuwepo. Anaandika kama  
Kichina au Kijapani kutoka juu kuja chini). (uk. 29)

Kwa nini mwalimu anaandika kama Kichina au Kijapani na sio kama Kiafrika? Ni kwa sababu elimu inayopitishwa haina manufaa kwa Mwafrika, ni elimu inayotetea matakwa ya kigeni, ni elimu inayoiga mambo ya kigeni mfano bara la Asia. Ni elimu ya mkengeuko.

Ubwege wa elimu ya bara hili unaendelezwa zaidi tunapowapata Mwalimu na Wanafunzi wake wakibadilisha somo la Fizikia kuwa la muziki. Baada ya kuzozana juu ya maana ya Archimides' principle, na suala la nyambizi, wanageukia wimbo. Wanaimba:

Tajiri kasimama  
kasimama kwa maguu yake  
Hana anacho!  
kope si zake  
kope ni zake  
Kasimama kwa maguu yake  
Kwenye mgongo wake mwenyewe  
(uk. 33)

Ni wimbo ambao unakejeli Mwafrika kwa kujigamba kuwa yu huru na tajiri huku akiendelea kumtegemea mkoloni mkongwe. Tajiri ni mtu anayejisimamia kifedha na kimawazo. Kufuata na kuendeleza elimu ya kigeni si utajiri bali ni utumwa. Utajiri utapatikanaje ikiwa Mwafrika ameshindwa kuidhibiti elimu yake ili aweze kujipatia maarifa yanayofaa ya uongozi? Ni ndoto tu, ni ubwege wa Kiafrika, wa kujidanganya badala ya kuzinduka na kurekebisha mwelekeo wa mambo.

Kuchanganyikiwa kwa mfumo wa elimu ya Kiafrika unabainika zaidi, tunapopatiwa sauti ya redio. Mazingira ya darasani, ghafla yanabadilika na tunasikia redio ikitoa matangazo. Sauti hii ya redio inaashiria utupu wa nchi ya Amezidi. Mtunzi anaitumia kuikejeli zaidi elimu ya bara la Afrika. Nchi nyingi, redio inasema, bado zinaendelea kuhitaji na kupokea misaada kutoka ng'ambo, misaada ambayo haifai. Nchi hizi zina wasomi wengi, na inashangaza kuwa zinatumia misaada na ruzuku zisizofaa. Ni dhihirisho la uduni wa elimu ya nchi hizi, ni elimu inayokatisha tamaa kwa vile haisaidii viongozi na raia kutambua kwamba bado wananyanyaswa na nchi za Kimagharibi. Afrika imekuwa ghala la kutupia uchafu wa Kimagharibi kama madawa yasiyohitajika, mitumba, na nyama mbovu.

Ubwege unaendelezwa zaidi tunapopata mwalimu na wanafunzi wamelala huku redio ikitoa taarifa. Mwalimu anasema:

Barabara. *anatabasamu* Dakika tano za  
kulala... tunza yenu! (*Wanalala na  
mwalimu wao juu ya meza zisizokuwepo*).  
(uk. 35)

Nani anapatiwa ujumbe huu wa redio? Ni dhahiri kuwa wasomi wamefumba macho yao na kuziba masikio yao ili wasisikie na kugundua uozo wao; wametafuta njia za kukwepa lawama. Camus (1953:11) anaeleza:

Tunaishi katika kipindi chenye uhalifu  
mwingi. Wahalifu tunaoshuhudia sasa  
si watoto dhaifu bali ni watu wazima  
ambao wamepata njia ya kujitoa lawama  
kwa kutumia ujanja. Wanatumia falsafa,  
ambayo pia inaweza kutumiwa kwa lolote,  
hata kugeuza wauaji kuwa mahakimu (Tafsiri yetu)



Redio inatangaza kuwa kijiji cha Fujo kimekumbwa na ukame na njaa. Kupitia tangazo hili, mwandishi anadhamiria kuonyesha kwamba ukame wa kimazingira ni kielelezo cha ukame wa kimawazo miongoni mwa wahusika wa tamthilia hii. Kupitia tendo la kulala kwa mwalimu na wanafunzi darasani, mtunzi pia anaonyesha udhahania wa wahusika, wahusika ambao hawahisi wala kujaribu kutatua shida za ulimwengu wanamoishi.

Mwalimu tunayekumbana naye katika tamthilia hii ni mfano wa Waafrika ambao licha ya kuelimishwa na serikali, bado wamebaki nyuma kifalsafa na kuendelea kuishi pangoni. Badala ya kutumia mbinu zinazofaa kufundisha somo la Fizikia, anawashirikisha wanafunzi katika kuikariri nadharia ya mwanasayansi Archimides, ambayo haina umuhimu wowote katika mazingira yao, na ulimwengu unaowazunguka. Nchi changa za Kiafrika ambazo zimepata uhuru, zinahitaji elimu ya kusukuma mbele sera zao za maendeleo na usawa. Kinyume na matarajio hayo, *Amezidi* inasawiri elimu inayotengana na mahitaji ya nchi. Nchi za Kimagharibi zingali zinaendeleza njama za kutawala bara la Afrika kisirisiri. Hivyo basi, wanahimiza mifumo ya elimu ambayo huendeleza mahitaji yao katika bara la Afrika. Marx (1959:328) anasema:

Historia ya mawazo na fikira inathibitisha  
kuwa mawazo yanayotolewa wakati wowote  
ule yanaambatana na mfumo uliopo. Mawazo  
ya kipindi chochote kile yamekuwa ni mawazo  
ya utawala wa wakati huo.

(Tafsiri yetu)

Afrika bado inaongozwa na mawazo ya kigeni. Viongozi wa Afrika wameshindwa kukuza mawazo yao asilia. Ame na Zidi wanategemea nchi za Kimagharibi kwa mahitaji yao yote, yakiwemo elimu na teknolojia. Elimu muhimu ni ile ambayo hunufaisha jamii kulingana na wakati. Mada ya Archimides' principle ambayo hufafanua juu ya ueleaji wa vyombo kama nyambizi baharini, haina uhusiano wa moja kwa moja na matatizo yanayoikumba jamii ya Amezidi. Ni elimu inayokatisha tamaa, kwa vile haina matumaini kwa raia.

Nyerere (1967:1) anasema kuwa, elimu ya aina hii ni ya kikoloni na haikupangwa na Wakoloni ili kuwaandaa vijana kulitumikia taifa lao bali ni kutimiza haja ya kuingiza tamaduni za kikoloni katika bara la Afrika na kuwafunza watu waendeleo kuwatumikia wakoloni wao wakongwe.

Mawazo ya Nyerere yanakaribiana na ya Rodney (1982:239) ambaye anasema kwamba, kulikuwa na utata kuhusu elimu iliyotolewa na utawala wa kikoloni. Ilibainika kuwa, nia yao kwa kweli haikuwa kudumisha mfumo wa jamii iliyokuwepo wala kuleta mabadiliko kwa wenyeji. Nia yao kuu ilikuwa ni kuwatayarisha baadhi ya Waafrika ambao wangesaidia kutoa huduma za usaidizi katika nyadhifa mbalimbali za utawala wa nchi zikiwemo ukarani, unyampala, na uakida.

Mohamed pia amezungumzia hali hii ya elimu ya mkengeuko katika tamthilia yake nyingine, *Kivuli Kinaishi* kupitia mhusika mtolewa. Elimu hii pia imetiliwa maanani na Kezilahabi katika *Dunia Uwanja wa Fujo*, na *Kichwamaji*.

### 3.5 SUALA LA HISTORIA

Katika mtazamo wa kiubwege, binadamu hapatwi historia. Binadamu anaishi katika ulimwengu katili, wenye fujo na ambao hauna historia. Hali hii ndiyo hubainika katika tamthilia za Beckett na Ionesco. Katika *The Lesson*, mtunzi hatupi historia ya wahusika wake; Pupil na Professor. Tunawapata tu hapo kama vibonzo vya kutumiwa na kuachiliwa. Katika *Waiting for Godot*, Beckett anapuuza historia ya Vladimir, Estragon, Lucky na Pozzo. Wahusika wengine wanatajwa tu bila hata kujitokeza jukwaani, mfano Godot. Hali sawa na hii inajitokeza katika kazi za Athol Fugard kama *The Blood Knot*, *The Coat*, na *No Good Friday*.

Katika *Amezidi*, mwandishi amejaribu kuwapa wahusika wake historia. Mzee anatupatia hali ya kuweza kukizia umri wake. Anasema:

Nimeishi si haba

Nimeishi kuona mengi

Pia nimedanganywa kwa mengi

Mwanzo nilibeba dunia nzito...

(uk. 2)

Anaendelea kutuambia:

Jana nilijua imepita na majuto

Leo najua haipo

Kesho haijazaliwa kamwe...

(uk. 3)

Huyu Mzee si kiumbe wa kidhanaishi. Ni binadamu wa kihalisia kwa vile ana uwezo wa kuorodhesha au kupanga matukio ya maisha yake kulingana na mpito wa wakati. Ame na Zidi nao wamepatiwa chembechembe za historia. Kupitia wimbo, mwandishi anatuambia:

Miaka mia tulikuwa vile vile

Leo tuko hivi hivi

Tu papo au tumeendelea

Tu macho tumelala

Au tumelala tu macho.

(uk. 68)

Hapa mwandishi anaashiria mpito wa wakati kuanzia kipindi kabla ya ukoloni, kipindi cha ukoloni na baada ya ukoloni, yaani kipindi cha uhuru. Miaka mia ni sawa na karne moja ya matukio barani Afrika, matukio ambayo ni ya kihalisia, si ya kiubwege.

Aidha, suala la historia linachomoza katika onyesho la saba tunapompata Zidi akikumbana na Mari. Wakati umembadilisha Mari kiasi cha Zidi kutomtambua. Zidi anasema:

Sikutambui, Mari...umebadilika...siye

tena Mari Mtarambura msichana wa

kijiji cha mjomba wangu: kile kijiji cha

Mpashambi...siye tena Mari mwenye

ngozi ya ganda la fuu na gome la mpingo...

Sasa ni Mari wa jijini na ngozi ya kukoboa!

(uk. 61)

Mtu habadiliki kiasi hiki kwa siku moja. Bila shaka Mari ameonja ya ulimwengu tangu aondoke kijiji chao, kijiji cha akina Zidi. Ni mfano wa historia fupi ya Mari na Zidi; historia ambayo inapingana na tapo la ubwege.

Kupitia Ame, mwandishi anajaribu kutupatia historia ya viongozi wa bara la Afrika. Wazo lake ni kuwa, viongozi kwa ujumla – wawe Wakoloni au Waafrika,, hawajalifanyia haki bara la Afrika. Mwandishi anawasuta viongozi hao kwa kupenda kusema tu pasi na kuchukua hatua zifaazo kutatua matatizo chungu nzima yanayowakumba raia wa kawaida wa bara hili. Anawakebehi kwa njama zao za kutoa hotuba zenye ufasaha wa maneno bila matendo. Ame anasema:

Wewe, lazima umeshapoteza mzee, ndugu,  
Rafiki, mwenzi, mpenzi au muhisani  
kama mimi nilivyompoteza Zidi...lakini  
tunacheka na kuchekelea kama vile  
mazigazi yatawarejesha... tunafurahi... na  
mbele yetu mazigazi...mazigazi... mazigazi...  
nini basi kama si ndoto na kujidanganya tu?  
Maneno makubwa makubwa, manene  
manene, lakini hayazuii roho kupotea...  
Na kesho ndugu yangu...ni siku yangu  
na yako...kesho tutakufa. (uk. 83)

Ni bayana kuwa maneno hayawezi kuzuia kifo. Jitihada za kuzuia roho kupotea au kukwepa kifo si ashiki ya kiubwege. Kiubwege kifo hushangiliwa na ndicho hatua ya mwisho ya binadamu ulimwenguni, kikomo cha historia yake duni.

### 3.6 HITIMISHO

Katika sura hii, tumechunguza jinsi tamthilia ya *Amezidi* imeshughulikia vipengele mbalimbali vya usanii hasa vya kimaudhui na kuonyesha mkabala wake kuhusiana na mtazamo wa kiuhalisia na kiubwege.

Tumbainisha kuwa, Mohamed ameathiriwa na waandishi wa tapo la ubwege kama Samuel Beckett, Eugene Ionesco na Athol Fugard. Hawa ni waandishi waliobobea kimawazo kuafikiana na tapo lao. Tamthilia ya *Amezidi* kwa kiasi haijaafikiana na vipengele pamoja na mielekeo ya kiubwege.

Mohamed anaelekea kukubali kuwa maisha ya binadamu ulimwenguni ni duni. Hata hivyo haamini kwa dhati kuwa binadamu amepotea kabisa. Kwake bado kuna matumaini ya kuboresha hali ya binadamu ulimwenguni. Amewapatia wahusika wake suluhisho la shida zao – kuacha uzembe na kujitolea kutenda kulingana na mahitaji ya nchi yao. Ingawa hivyo Ame na Zidi wanakatisha tamaa.

## TANBIHI

<sup>1</sup> International Bible Society (1973) *Holy Bible*.

New International Version.

Kitabu cha Ufunuo.

<sup>2</sup> Irungu, C. M. (1999) *Dhana ya Maisha Katika Novela Mbili za*

*Euphrase Kezilahabi: Nagona na Mzingile*.

Tasnifu ya M. A, haijachapishwa.

Uk. 32-33

<sup>3</sup> Taz. Roubiczek, P. (1964) *Existentialism For and Against*.

Cambridge University Press, London.

Uk. 39-40

---

## 4.0 SURA YA NNE

### 4.1 UTANGULIZI

Maswala muhimu yatakayoshughulikiwa katika sura hii yanajikita katika kipengele cha fani. Haya ni pamoja na uhusika, mazingira, ploti, nyimbo, lugha na mawasiliano. Tumeyachanganua kwa kusudi la kudhihirisha athari ya ubwege katika tamthilia hii.

### 4.2 UHUSIKA

Dhana ya uhusika imefafanuliwa na *Kamusi ya Fasihi* (2001:96) kuwa:

Utaratibu wa kuwaumba wahusika pamoja na kunga zinazokwenda na utaratibu huo, hasa utofautishaji na ukuzaji wao.

Katika tamthilia ya *Amezidi*, mwandishi anasawiri wahusika wawili wakuu ambao ni Ame na Zidi. Wahusika hawa ni raia wa nchi ya *Amezidi*, nchi ambayo kulingana na tamthilia inaweza kuwa yoyote katika bara la Afrika. Sauti ya redio, katika onyesho la nne, inathibitisha dai hili:

Hii ni sauti ya *Amezidi*... Taarifa tuliyoipata punde hivi inasema kwamba katika kijiji cha Fujo, maelfu kwa maelfu ya watu wanakufa kwa njaa kila siku... sababu ya ukame. Mvua hazijanyesha miaka mingi... Umoja wa Mataifa unaandaa misaada...  
(uk. 35)

*Amezidi* inaweza kuwa nchi ya Ethiopia, Somalia au Rwanda nchi ambazo kwa kiasi kikubwa zinabainisha mazingira yanayosawiriwa kupitia kwa sauti ya redio.

Suala la wahusika wachache katika tamthilia za kibwege ni dhahiri. Wahusika katika tamthilia hii kama ambavyo tumetaja ni wawili lakini wanachukua nafasi tofauti tofauti

za kikazi katika nchi hii ya Amezidi. Hali hii ni sawa na ya tamthilia za Beckett, Ionesco, na Fugard. Katika tamthilia ya *Waiting for Godot*, tunapata wahusika wawili wakuu, Vladimir na Estragon. Wahusika wengine kama Pozzo na Lucky wanajitokeza kama vijenzi vya wahusika wakuu.

Katika *The Blood Knot*, Fugard anasawiri wahusika wawili tu, Morris na Zachariah, naye Ionesco katika *The Lesson*, anajikita katika wahusika, Pupil, na Professor.

Tamthilia za kibwege hukosa wahusika wa kihalisia. Njogu na Chimerah (1999:75) wanasema:

Wahusika wa tamthilia za kibwege, si wa kihalisia  
wanaoweza kutambulikana na kuonekana katika  
mazingira yetu, bali wamebuniwa akilini mwa  
mwandishi ili kuendeleza mawazo yake.

Wahusika katika tamthilia ya *Amezidi* si wa kihalisia. Mwandishi amewaumba kidhahanifu huku matendo na mazungumzo yao yakikiuka hali za kawaida. Tunasoma:

Tendo linatokea mawazoni na uhalisini...  
Pangoni. (uk 4)

Aidha, katika onyesho la pili, tuwaelezwa:

Tendo hili lote linatokea ndotoni mwa  
Ame na Zidi. (uk 12)

Tamthilia za kibwege hujikita katika mawazo, na mambo ya kufikirika tu, ya kidhahania. Mohamed anajaribu kuafikiana na mkabala huu anapoanza maonyesho yake kwa mawazo na ndoto nyingi.



Ukosefu wa uhalisia, hufanya wahusika wa kibwege waamini na kusisitiza vitu visivyokuwepo. Katika tamthilia ya *Amezidi*, Ame na Zidi wanaamini kuwa makazi yao ni yenye utajiri, kasri kubwa ambalo limejaa marembo na mapambo. Zaidi ya hayo, kasri hili lina watumishi, na furaha. Ukweli wa mambo hata hivyo ni kuwa hawa wanaota, na vitu ambavyo wanazungumzia ni mazingaombwe tu. Nyumba yao ni pango, yaani mahali penye umaskini na uhitaji mwingi ndiposa wanalazimika kuomba na kutegemea misaada kutoka nje. Baadhi ya yale wanayoamini ni vyeo vikubwa kazini, na utajiri mwingi. Onyesho la tano linaanza hivi:

Tendo limo fikirani... pango linageuka ofisi!  
Ame ni bosu, na Zidi, msaidizi wake. Ame ameketi  
nyuma ya meza yenye simu isiyokuwepo... kwa  
kweli ameketi chini sakafuni... Matendo yanatokea  
ndotoni mwao. (uk. 40)

Hali hii ya kuota na kufikiria yasiyokuwepo inabainika pia tunapompata mhusika Bosu. Anatueleza:

Anatoa orodha ndefu kwenye mtoto wa meza  
isiyokuwepo. Anampa msaidizi wake aisome  
orodha yenyewe nayo haionekani. (uk. 42-43)

Orodha inayotajwa ni ya vitu ambavyo Bosu na msaidizi wake wanahitaji ofisini mwao na ambavyo wafanyikazi wote walipaswa kuvihitimisha. Vitu vyenyewe ni vya kuagizwa kutoka ng'ambo kama vile fenicha, zulia, mapankaboi, simu, na meza ya Executive.

Mwandishi anaelekea kuwakejeli raia na viongozi wa *Amezidi*. Ni watu ambao ni maskini hohehahe, wanaotegemea misaada ya kigeni, lakini hapa wanaonyesha uwezo wa kifedha wa kuagiza vitu ghali kadha wa kadha kutoka Ulaya. Ni hali isiyoaminika, ya kuota na kufikirika tu, ubwege.

Wahusika wa kiubwege hukosa historia. Katika tamthilia ya *Amezidi*, wahusika tunaopewa hawana ukuaji unaofuata misingi ya kiuhalisia. Ingawa kuna chembechembe za historia hasa kupitia mzee na wimbo wake, wahusika wakuu Ame na Zidi wanajitokeza tu kama mapacha, vibonzo wa kutumika kutekeleza majukumu fulani tu. Zaidi ya hayo, hatuonyeshwi asili yao, umri wao wala kazi zao kikamilifu.

Kuhusu suala la utendaji, wahusika wa kibwege hawapatiwi nafasi ya kutenda au kutekeleza mambo ya maana. Njogu na Chimerah (1999:75) wanaeleza kuwa:

Wahusika wa kibwege hujiepusha na kutenda,  
na badala yake huketi na kuzungumza tu.

Ame na Zidi hawafanyi lolote la maana kujinufaisha au kuboresha hali yao duni. Ni wahusika waliokwama kwenye shida nyingi zikiwemo umaskini, ukosefu wa ujuzi na elimu, na magonjwa mabaya, lakini hatuwaoni wakijaribu kujinasua kutoka kwa minyororo ya uduni inayowazunguka. Wanalofanya aghalabu ni kulala tu. Tunasoma:

Ame: Na kwa nini mtu apende kazi? Mungu yupo na ardhi  
ipo... na ardhi yenyewe bikra... ikidondoka mbegu  
tu imeshaota! Ukiatika kambu za migomba kesho  
utakula ndizi: na hata mwaka mzima ardhi inakubali  
tu, haichoki... Wewe kula tu na kulala! Ah, hata  
Mungu alifanya kazi siku saba, kisha akapumzika...  
na wewe ulilala siku ngapi vile?

Zidi: Siku tisa kama wewe!

(uk. 7)

Wahusika wa namna hii, ambao hawatendi lolote la maana ni sawa na binadamu wa kidhanaishi anayeishi tu huku akisubiri kifo.

Badala ya Ame na Zidi kufanya kazi, wanatumia wakati wao mwingi kulala na kuzungumza. Suala hili la mazungumzo ni muhimu katika fasihi ya kiubwege. Wahusika wa kiubwege mara nyingi hujiingiza katika mazungumzo ambayo aghalabu yanazuia uelewano na badala yake kuzua ubishi usio na maana yoyote. Hali ya mwandishi kusawiri wahusika hafifu wasioelewana kwa mambo madogo madogo na ambayo hukosa mantiki ya mazungumzo, ni kigezo muhimu kinachoendeleza hali ya ubwege na hivyo hivyo kukuza imani ya kidhanaishi kuwa maisha ni fujo na hayana maana yoyote. Ame na Zidi katika onyesho la kwanza wanabishana kuhusu masuala ya kikawaida kama kuamka, kulala, hali ya kuwa kumekucha, hali ya suruali iliyoraruka makalioni, na hali ya mhogo uliovunda. (uk. 4-5)

Aidha wahusika hawa hutatiza mawasiliano kwa kuingiza hoja ambazo hazina uhusiano wowote na yale yanayokithiri. Mfano suala la suruali kuliwa na panya, au panya kuliwa na suruali, halina umantiki wala maana ya moja kwa moja kulingana na muktadha wa mazungumzo ya wahusika. (uk. 5). Hili ni suala la ubwege.

Wahusika hawa ni wazembe na wajinga. Ame na Zidi wanajikuta katika hali ya uhitaji mwingi ambayo inawalazimisha kukubali usaidizi usiofaa. Misaada wanayopewa haina thamani. Mihogo iliyovunda tunaambiwa imetoka nje. Nje hapa panaweza kumaanisha nje ya bara la Afrika; ni jazanda ya misaada mibaya na yenye vikwazo ambayo Wazungu hutunukia Waafrika. Tamthilia inaendeleza wazo hili kupitia Ame na Zidi:

Zidi: Ujue cha kuliwa .....

Ame: Kinacholiwa.

Zidi: Mhogo wa kuvunda...

Ame: Mpe paka.

Zidi: Hataula

Ame: Mpe mbwa.

Zidi: Ataunusa tu 'ende zake...

Ame: Mpe mbuzi.

Zidi: Labda... labda mbuzi aliyekosa majani! (uk. 6)

Mbuzi aliyekosa majani ni jazanda ya Waafrika wanaokufa kwa njaa kwa sababu ya ukame na vita vya wenyewe kwa wenyewe. Kwa kukosa njia bora ya kujisaidia (majani), hupokea misaada yoyote hata yenye kasoro nyingi na kuifurahia. Hali hii ya wahusika kufurahia vitu vibaya huendeleza imani ya kidhanaishi kuwa ulimwengu hauna wema na binadamu hawezi kupata furaha ya kudumu maishani mwake.

Hali hii inaendelezwa vyema kupitia sauti ya redio inayoeleza kuwa:

...Umoja wa Mataifa unaandaa misaada. Marekani ishapeleka misaada ya magunia milioni ya sembe na dona... Uingereza imepeleka mitumba na nyama ya kukausha... Ufaransa imetoa madawa ambayo huko hayahitajiki tena. (uk. 35).

Kupokea misaada si tendo baya, lakini kutegemea misaada kila wakati ni ulitima unaochukiza. Ikumbukwe kuwa, Ame na Zidi wana kazi, nchi yao ina rutuba, madini na malighafi nyingine chungu nzima, lakini hawafanyi lolote la maana kurekebisha hali yao ya maisha. Mali yao inapotea tu, wameipoteza kwa ujinga wao. Tunaambiwa kuwa kasri lao halina maji, hata tone moja:

Ame: Tumekuwa tukijidanganya, Zidi.

Zidi: Hivi kweli kasri hili lote halina maji?

Ame: Enh, hamna maji hata tone moja!

Zidi: Tumekuwa tukijidanganya, Ame!

Ame: Hapana; sikudanganya, Zidi.

Zidi: Aaaaaa, hunifahamu ... ka... hamkuwa na lolote ila mlitawaliwa na ujinga, uvivu, mapuuza, unafiki, wivu, choyo... humu katika kasri letu...

Ame: Hapana. Mlikuwa na maji na kila kitu humu; ela vimehama...

Zidi: Labda tulivihamisha mimi na wewe  
au tuseme tulivihamisha kwa kuvibadilisha  
kwa nyama mbovu – aaa, tumboo, Ame;  
linanikeketa... aaa, naona linaanza tena  
kuniendesha. (uk. 77)

Nyama mbovu inayorejelewa hapa ni lile paja la nyama ya ng'ombe lililoangushwa na EC. (uk. 69-70). Paja hilo lilikuwa na maandishi EC, na ni msaada uliotolewa kuwaokoa raia wa Amezidi kutoka kwa tisho la kifo kutokana na ukosefu wa chakula.

Kejeli ni kwamba, badala ya paja hilo kuwaokoa wapokeaji, linawaleta ugonjwa mbaya na kusababisha kifo chao. Kifo cha Ame na Zidi kinathibitisha imani ya kidhanaishi kuwa, binadamu hana uwezo wa kuzuia kifo, kifo ndicho hatua ya mwisho ambayo binadamu anangojea ulimwenguni.

Wahusika wanaokaa na kulala huku wakisubiri kuokolewa ni wa kiubwege. Katika *Waiting for Godot*, tunapata Vladimir na Estragon katika hali duni na ya uhitaji lakini hawatendi lolote la kuwanufaisha ila kumngojea Godot, ambaye tunaweza kumchukulia kuwa mwokozi au Mungu wao. Matumaini ya wahusika hawa yanatumbukia nyongo kwa vile Godot hatokei na uduni wao kunata zaidi.

Hali hii ya kutotenda la maana ila kutegemea misaada na wokovu, inaendeleza imani ya kidhanaishi kuwa maisha ni majaaliwa na binadamu huishi kibahati. Kezilahabi, mmoja wa waandishi tajika wa kidhanaishi barani Afrika anasema:<sup>1</sup>

Maisha ni mkondo, hakuna kurudi nyuma.  
Kama maji katika mteremko,  
Maisha ya mwanadamu huenda mbele  
kwa kasi sana.

Wahusika wa kiubwege, hukosa umantiki wa mawasiliano. Mazungumzo yao yanabainisha utengano mwingi na hayana umuhimu. Mhakiki wa drama ya kiubwege, Esslin Martin (1974:4) anasema:

Kawaida, tamthilia huwa na umantiki wa mazungumzo kati ya wahusika, ilhali tamthilia za kibwege hubainisha utengano, upweke wa mazungumzo. (Tafsiri yetu)

Hali hii ndiyo inayodhihirika katika *Amezidi*. Wahusika wakati mwingi hujiingiza katika mazungumzo yenye ubatili, yasiyo na umuhimu wowote. Katika onyesho la nne, tunapata Mwalimu (Zidi) na Mwanafunzi (Ame) wakiwa katika mazungumzo yasiyokuwa na nia maalum ila kupoteza wakati na kuendeleza ubwege wao.

Mwanafunzi: Suala?

Mwalimu: Jibu.

Mwanafunzi: Suala.

Mwalimu: Jibu.

Mwanafunzi: Jibu.

Mwalimu: Suala.

Mwanafunzi: Sawa

Mwalimu: Sawa nini?

Mwanafunzi: Sawa sawa.

Mwalimu: Sawa.

(uk. 30)

Kutatizika huku kwa mawasiliano kunapatikana kote katika tamthilia. Katika uk. 47, Ame na Zidi, wanabishana juu ya 'nje' na 'ndani' kiasi ambacho kinawasawiri kama wahusika waliopotea na wasiojua kinachoendelea.

Haya si mazungumzo yanayoweza kutarajiwa kutoka kwenye vinywa vya wahusika wa kihalisia, ni mawasiliano ya vibonzo, wahusika wa kiubwege.

Beckett katika *Waiting for Godot* anatuchorea hali sawa ya wahusika:

Estragon: Tufanye nini sasa?

Vladimir: Huku yuingoja.

Estragon: Huku tuingoja (kimya)

Vladimir: Tunaweza kunyosha viuongo.

Estragon: Matembezi yetu.

Vladimir: Kujiinua kwetu.

Vladimir: Kupumzika kwetu.

Estragon: Kupumzika kwetu.

Vladimir: Kujitayarisha kwetu

Estragon: Ili tuweze kutulia..

(Tafsiri yetu) (uk. 76)

Ukosefu wa mtiririko katika mazungumzo ya wahusika wa kibwege ni thibitisho la imani ya kidhanaishi kuwa, maisha ya binadamu ulimwenguni ni kama ajali. Matukio hutokea tu bila visababishi wala mpango wowote.

Suala la maisha kuwa usumbufu, mateso, pia ni dhahiri miongoni mwa wahusika wa kibwege. Waandishi wa kibwege husawiri wahusika wenye majonzi na mitafaruku mingi katika maisha. Tamthilia ya *Amezidi* inasheheni wahusika ambao wanakumbwa na visa vingi visivyopendeza. Ni wahusika maskini, na wahitaji wa kiwango kikubwa. Tunawapata katika hali ya ukosefu wa chakula cha kutosha, hawana mavazi ya kiheshima, wamejaa uzembe na wanakumbwa na maradhi mabaya. Ni wahusika ambao wamezama kwenye matope ya shida na hivyo basi kulazimika kuomba misaada kutoka nje, misaada isiyofaa na ambayo inawaangamiza zaidi. Tunaambiwa:

... anageuka na Ame anatazama suruali ya Zidi  
imechanika makalioni!!! (uk. 5)

Ni wahusika wanaoalia matambara licha ya kuwa na mazingira yenye mbolea na malighafi chungu nzima. Kuhusu uzembe wao, Ame anasema:

eee, na hiyo imenikumbusha ... wajua wewe  
hujapiga simu kazini kwako wala mimi sijapiga  
kazini kwangu kuwaeleza mabosi wetu kwamba  
hatujaenda kazini wiki ya pili... Yaani kwa nini ...(uk. 15)

Ame na Zidi, sawa na Waafrika, ni wahusika wenye nguvu na ambao wana kazi za kuajiriwa. Ingawa wana wajibu wa kujizatiti, na jukumu la kufanikisha maendeleo ya nchi yao, wanazembea kazi. Ni wahusika wa kukatisha tamaa kwa mwandishi na hadhira.

Tamthilia inaelekea kuwacheka viongozi wa Kiafrika kwa ubwete na ujinga wao. Licha ya kustarehe kwa kulala na kutoenda kazini, wahusika hawa hawapati furaha ya kudumu. Wanasumbuliwa na mbu ambao wanasambaza ugonjwa wa Malaria. Katika onyesho la nane, tunaambiwa:

Zidi: Mbu ...

Ame: Mbu ...

Zidi: Huyu! (Anakwenda kulia)

Ame: Huyu! (Anakwenda kushoto)

Zidi: Huyu (Anapigapiga makofi, lakini mbu hampati)

Ame: Huyu! (Anarusha mikono ovyo. Wanamwinda  
kwa muda mrefu)

(uk. 65)

Mbu ni mdudu mbaya na madhara yake kwa binadamu hayawezi kupuuzwa. Mbu hapa ni sitiari ya wakoloni, na Malaria husimamia madhara au athari ya ukoloni kwa Mwafrika. Ame na Zidi, wanateseka lakini hawana njia ya kujiepusha au kukwepa mateso hayo. Tunaambiwa hawana madawa ya kutibu Malaria hiyo:



Zidi: Madawa tununue? Kwa nini hatufanyi yetu?

Ame: Si mpaka tuvumbue kwini!

Zidi: Kwa nini hatuvumbui?

Ame: Tununue tu.

Zidi: Kwa nini

Ame: Ndiyo raha, ndiyo kuendelea... (uk. 66)

Madawa kama kwini ni sawa na mbinu za kukabiliana na ukoloni. Waafrika wametekwa na njama za Wazungu na hawana njia (madawa) za kuwakwepa wakoloni hao. Ukweli huu unaendelezwa zaidi mbeleni, tunapowakuta Ame na Zidi wakilia na kuangamia kwa kipindupindu, ugonjwa uliosambazwa kupitia msaada wa paja la nyama ya ng'ombe kutoka EC. Wahusika hawa wanasemezana:

Ame: Na kipindupindu pia na kwa msaada wa nyama ya EC.

Zidi: Na mimi nakwenda huko huko.

Ame: Si kwa ukame lakini ...

Zidi: Kwa nyama mbovu! Mtume! Nakufa mimi, Ame! ...

Zidi: Usinikumbatie ... usiniguse... usisahau kwamba

Nina kipindupindu mimi...

Ame: Haidhuru!

Zidi: Kwaheri basi, Ame!

(uk. 79)

Kigezo cha wahusika wenye majonzi kinabainika pia katika kazi za Kezilahabi, mmoja wa waandishi stadi wa tapo la udhanaishi. Anaamini kwamba maisha hayana furaha, ni mateso, ni huzuni tupu. Kwake, furaha ni neno jingine la adhabu. Anaendeleza wazo kwamba, kupata furaha ulimwenguni ni jambo lisilowezezana na hata furaha ikipatikana, ni ya muda mfupi tu. Kazimoto<sup>2</sup> anasema:

Mwanadamu ni kiumbe ambaye amejaribu kutafuta njia nyingi zitakazomwezesha kupata furaha. Kwa kuwa ameshindwa kupata furaha duniani amejenga kichwani mwake kitu kama mbingu, yaani mahali anapotegemea kupata furaha baada ya kufa.

Mohamed anatumia mbinu ya mhusika ndani ya mhusika katika tamthilia ya *Amezidi*. Ame na Zidi wanabadilikabadilika na kuchukua nyadhifa mbalimbali kulingana na mahitaji ya mtunzi. Kwa mfano Ame anakuwa Mari katika onyesho la tatu, Mwanafunzi katika onyesho la nne huku Zidi akiwa Mwalimu wake. Katika onyesho la tano, Ame ni boshi na Zidi ni msaidizi wake. Hali hii hubainika katika kazi za kiubwege chambilecho Anderson (1972:2) anayesema:

Wakati mwingine wahusika hawa hubadilika  
hali zao, mazungumzo yao yamejaa ukinzano;  
hukataa kuamini yaliyomo ulimwenguni na  
badala yake kukubali matukio ya kidhahania.  
Maelezo yao juu ya hali na dhana mbalimbali  
hukosa maana.

(Tafsiri yetu)

Kigezo cha kutozingatia yaliyomo na kuamini ya kufikirika kinadhihirika wazi katika *Amezidi*. Ame na Zidi wanaishi katika ulimwengu wa kindoto. Badala ya kukubali hali yao duni ndani ya pango, wanaota na kuamini juu ya kasri lenye fahari. Hii ni hali ya wigo bubu, mbinu inayoendeleza ubwege wa wahusika hawa.

Kwingineko, Ionesco katika *The Chairs*, *The Lesson*, na *Rhinoceros* anasawiri wahusika wanaobadilika badilika na ambao wanaamini vitu na mambo ya kidhahania, sawa na wenzao katika *Amezidi*.

Aidha, katika *Amezidi*, tunakumbana na wahusika ambao hawajui watokako wala wanakoelekea. Wanajigamba kuwa wao ni matajiri huku wakiendelea kuhitaji na kupokea misaada. Ame na Zidi wanajua kwamba misaada wanayopata ni mibaya, imevunda lakini bado wanaipokea na kuitumia. Hawa ni wahusika wapumbavu waliochanganyikiwa na wanaofurahia uvundo. Ni wahusika wa kibwege.

Mohamed ameibua wahusika walioathirika kiubwege. Kupitia uhusiano wao, pamoja na matendo yao, Ame na Zidi wanathibitisha kuathiriwa kwa mwandishi na tapo la uandishi wa drama ya kiubwege. Ame na Zidi ni wahusika wenye nafsi moja, wana imani zinazofanana, tabia zinazoshabihiana, mielekeo sawa ya kimaisha, mazungumzo yao ni ya mkabala mmoja na kifo chao kinatokea kwa namna moja. Kwa hakika, hawa si wahusika wa kihalisia, ni wa kiubwege ambao wamebuniwa katika akili ya mwandishi ili kusaidia kuendeleza mawazo yake juu ya uduni, ubwege wa bara la Afrika.

Huu ni ubwege ambao umechochewa na uzembe pamoja na ujinga wa Mwafrika. Mwafrika, kwa kumruhusu tena Mzungu kuingilia maisha yake, amedhoofika kiuchumi, kisiasa na kitamaduni na hivyo kubaki akiishi kinyama, kiubwege.

Ame na Zidi ni wahusika ambao hawajijui wala hawajitambui. Mara kwa mara husahau mambo mengi. Tunawaona wakisahau siku ya kuzaliwa kwao, siku ambayo ni muhimu katika maisha na maendeleo yao. Mwandishi anawakejeli kwa kusherehekea siku ambayo hawaikumbuki. Wanatumia pesa nyingi kuandaa sherehe za siku wasiyoitambua umuhimu wake, ni ishara ya uongozi duni na ambao hauna mwelekeo. Wanasahau pia kuwa Mzungu ni adui na hivyo kuendelea kuhusiana naye kidugu. Uhusiano huu unachangia maangamizo yao.

Wahusika wa kihalisia hujaribu kutenda na kufikiria jinsi ya kuboresha hali zao za kimaisha. Ame na Zidi kutoka mwanzo hadi mwisho wa tamthilia wamesawiriwa kama vibonzo. Hawatendi wala hawafikirii lolote la maana. Wakati wao mwingi wanatumia kuota na kufurahia uduni na maangamizo yao. Hawana haja ya kusafisha uchafu wao; kwao, maisha ni usumbufu na binadamu anapaswa kuyaishi jinsi yalivyo. Hawa kwa kweli ni wahusika wa kiubwege.

### 4.3 MAZINGIRA

Dhana ya mazingira inaelezewa na *Kamusi ya Fasihi* (2001:44) kuwa:

Mahali, wakati na muktadha wa kijamii  
ambamo matukio ya kazi ya kifasihi hutokea.

Tamthilia ya *Amezidi* inabainisha mazingira ya kibunilizi yenye ishara mbalimbali za kiuasilia. Onyesho la kwanza linaeleza:

Tendo linatokea mawazoni na uhalisini.....

Pangoni.... spotilaiti inafuata wahusika.

(Uk. 4)

Tunaambiwa kuwa Ame na Zidi wanaishi pangoni. Mazingira ya pango ni machafu na ya kinyama. Hali ya binadamu kuishi pangoni badala ya nyumbani ni dhana ya kiubwege. Binadamu husawiriwa kama kiumbe duni na anayestahili kuishi katika mazingira machafu na yanayokatisha tamaa. Katika onyesho la pili, tunaenezwa:

Zidi: Umeniamshia nini?

Ame: Kukuuliza.

Zidi: Nini?

Ame: Kama umepata kuikagua kwa macho nyumba hii yetu...

Zidi: Humu pangoni?

Ame: Pangoni, au kasrini mwetu?

Zidi: Ah, kasri ndiyo, kwani lina nini?

(uk. 12)

Wahusika hawa wanaishi katika mazingira ya kuchukiza, pangoni, lakini wanafurahia hali hiyo. Kwao, pango ni kasri, ni makao mazuri ya kuishi. Kuishi na kufurahia uduni wa maisha ni suala la kiubwege ambalo huendeleza imani ya kidhanaishi kuwa maisha hayana maana, hayana furaha ila huzuni tupu.

Hali hii katika *Amezidi* inakaribiana na ile inayosawiriwa katika *Waiting for Godot*. Vladimir na Estragon wanatumia kichunguu kama kiti, na mchezo unafanyika barabarani. Kichunguu sawa na pango ni vitu vyenye uasilia. Matumizi ya vitu au vifaa vya kiasili licha ya kuwoko kwa vile vya kisasa kama viti na nyumba, ni kipengele cha ubwege. Barabarani ni mahali pachafu; ni mazingira yanayozua taswira ya vumbi wakati wa kiangazi na matope wakati wa mvua. Beckett anapotumia barabara ya mashambani, badala ya barabara ya kisasa, ya kimji, anaendeleza hali ya kutobadilika kwa binadamu. Binadamu bado anaendelea kuishi kinyama katika maisha yenye usumbufu na yanayokatisha tamaa.

Katika onyesho la nane, Ame na Zidi wanakubali kuwa mazingira ya maisha yao ni duni lakini kwa vile wameyazoea, yamekuwa kama kasri. Kwao harufu mbaya ni uturi. Wanasemezana:

Zidi: (Anaziba pua) Mmmff.

Ame: Nini?

Zidi: Harufu! (Anaziba pua)

Ame: Nini?

Zidi: Uvundo! (Anaziba pua)

.....

Ame: La, pana uturi hapa?

Zidi: Uturi – mzoga!

Ame: La, mzoga-uturi.

(uk. 64)

Mohamed, katika *Amezidi* pia amewapatia wahusika wake vifaa duni kama kibenza na vijiti (uk. 10); kupekecha moto badala ya kutumia kibiriti (uk. 11), kiserema, mavi ya ng'ombe na samadi (uk. 38) na kadhalika. Vifaa na hali hizi huchora mazingira ya kuchukiza yasiyomsaidia binadamu kuishi katika furaha, bali huendelea kumdhoofisha kifikira na kimaisha.

Kuna matumizi ya mandhari na dhana zinazosheheni ishara za giza na mwangaza. Giza ni ishara ya woga. Mazingira yenye giza huogofya na hukatisha tamaa kwa binadamu anayetaka kuona mbele. Hali hii husaidia kufafanua maisha ya binadamu ulimwenguni. Binadamu amegubikwa na giza totoro na ni sharti atafute mwangaza ili aweze kugundua ukweli wa kuweco kwake ulimwenguni. Mohamed ametumia neno GIZA kama kimalizio cha maonyesho yake. Amedhamiria kubainisha utata wa maisha ya binadamu, maisha ambayo hayana mwelekeo na yanayoendelea kudidimia.

Katika onyesho la kwanza, tunaambiwa:

Spotilaiti inafuata wahusika

(uk. 4)

Spotilaiti, kawaida hutumika mahali pasipo na mwangaza, penye giza. Spotilaiti hapa yaelekea kusimamia jitihada za binadamu kutafuta ukweli juu ya maisha yake. Giza linaweza kuwa jazanda ya hali ya binadamu ya kutojifahamu na kutoelewa ulimwengu anamoishi. Binadamu anadanganyika kuwa anaishi vizuri kwa furaha. Ameshindwa kutambua ukweli wa mambo kuwa maisha ni duni na ni adhabu kali. Hii ndiyo sababu waandishi wa kiubwege hutumia mazingira hafifu na ya kukatisha tamaa kama pango, mahali palipoinukia – kichunguu, ili kuashiria uozo wa maisha ulimwenguni. Vichunguu (*Waiting for Godot*) na mapango (*Amezidi*), ni makazi ya wanyama wa mwituni si makao ya binadamu kamwe. Binadamu na maisha yake, ni sawa na wanyama wa mwituni katika mkabala wa uandishi wa drama ya kiubwege.

Kuna matumizi ya mti katika *Amezidi* na kazi zingine za kibwege. Mti hutumiwa kudhihirisha maisha yasiyobadilika, kiumbe kisicho na uwezo wa kutembea au hiari ya kubadilisha hali yake ila kutegemea majaaliwa. Katika onyesho la kwanza, tunapata matumizi ya vijiti (uk. 10), ambavyo ni sehemu ya mti. Aidha, mwalimu katika onyesho la nne, anaingia darasani na bakora ndefu. Anasema:

Na...na.....nani atata... taja  
Archimedes' principle .. mikono juu .. enhe.  
(Kwa Mwanafunzi wake Ame). Wewe, Ame!  
(sasa Mwalimu anasimama na bakora inayoonekana.  
Bakora ndefu)  
(uk. 29)

Katika *Waiting for Godot*, tunapata pia ishara ya mti katika maelezo ya tendo la kwanza. Kiubwege, mti ni sitiari ya binadamu asiyekuwa na uwezo katika ulimwengu katili unaomtesa. Ni hali ya upweke, utengano wa maisha. David Cante<sup>3</sup>, anasema:

Ole wangu niwe kama mti

Mohamed amefuata mtindo wa watunzi wa drama ya kiubwege. Hawa huchora wahusika, wanaosawiri na kuendeleza mazingira ya maisha ya kinyama. Wahusika wao kwa kiwango kikubwa hushabihiana na wanyama kitabia na kivitendo. Katika *Amezidi*, Ame na Zidi hula mihogo iliyovunda na mibichi kama wanyama. Tunawaona wakitumia kucha zao kuumenya mhogo:

Ame: Kwani kucha huna? Tumia kucha bwana....

Zidi: Haya (anamwendea na kumpa ile mihogo miwili),  
imenye kwa kucha basi...

Ame: Aaaa, hata kumenya kwa kucha zako umeshindwa....

(anamenya mhogo kwa kucha na kisha...).

Huu mmoja niliokwisha umenya unatosha...

Menya huo wako sasa!

(uk. 11)

Aidha, wahusika hawa hula nyama mbichi na iliyooza mithili ya wanyama wa mwituni:

Zidi: Njaa!

Ame: Njaa!

Zidi: Una meno?

Ame: N'na meno!

Zidi: Tuwe simba basi.

(wanalitafuna paja la nyama mbichi iliyooza!)

(uk. 72)

Haya ni mazingira ya kiuhayawani, na yenye nia ya kubainisha uduni wa maisha ya binadamu. Tofauti kati ya binadamu na wanyama katika mtazamo wa kiubwege ni nyembamba mno. Hali hii hupingana na madai ya kuwoko kwa jamii ya binadamu yenye ustaarabu wa kimaisha kutokana na maendeleo ya kiviwanda.

Beckett, katika *Waiting for Godot* kwa mfano, anachora wahusika waliozama ndani ya mazingira ya kinyama na ambayo huchukiza. Lucky, amebeba mzigo mzito mgongoni mwake (uk. 21), na anafurutwa kwa kamba kama mnyama. Zaidi ya hayo, Pozzo anampiga mijeledi na kumwumiza kinyama. Mzigo wa Lucky ni jazanda ya maisha ya binadamu, maisha yenye usumbufu na ambayo sio rahisi kuyaishi.

Tamthilia ya *Amezidi* pia husawiri mazingira ya ukame. Mwandishi amechora mazingira ya ukavu, mazingira yasiyopendeza na yaliyojaa mizoga, wafu, wakondefu na vumbi (uk. 35) Haya ni mazingira yanayomulika bara la Afrika kiuchumi, kisiasa na kitamaduni, hasa baada ya uhuru. Ni mazingira ambayo ni ya kihistoria na hivyo yanakiuka muktadha wa kiubwege. Historia ya jamii ni suala la uhalisia na kwa kujaribu kubainisha mazingira hayo, Mohamed amekiuka kanuni za tapo la ubwege.

Mazingira tunayopata katika tamthilia hii, hayaifungi katika taifa moja, bali ni mazingira wazi, yanayoweza kutambulikana katika maeneo mengi. Ame na Zidi ni raia wa *Amezidi*, nchi ambayo inaweza kuwa yoyote miongoni mwa nchi za bara la Afrika au hata nje ya bara hili. Mazingira yanayovuka mipaka, yanayoweza kubainika katika nchi nyingi, huendeleza sifa ya utafa na umataifa ambayo ni kipengele muhimu cha tapo la usasa na usasaleo.

Mazingira ya kazi za kiubwege pia hubainisha utupu. Katika jukwaa, tamthilia za kiubwege huwa na vifaa vichache sana, na suala la mapambo halitiliwi maanani. *Amezidi* inaafikiana na kigezo hiki. Mwandishi anatumia jukwaa tu linalosheheni wahusika vibonzo wasiotenda la maana ila kuota tu. Madhumuni ni kuonyesha au kurejelea utupu wa maisha ya binadamu ulimwenguni.

Suala la ukosefu wa matumaini maishani nalo hupitishwa kwa kutumia mazingira. Mazingira ya kiubwege hukosa matumaini na huonyesha uchafu na usumbufu. Mandhari ya mchezo wa *Amezidi* kwa kiasi kikubwa huchukiza kwa vile hufanyika pangoni. Haya ni mazingira yanayokiuka ustaarabu unaokusudiwa binadamu, ni ubwege. Mahali pachafu na pasipokalika kwa sababu ya ukosefu wa vifaa na vitu muhimu na vya kimsingi kama chakula, mavazi, na maji, ni dhahirisho la maisha yasiyo na maana na ya kukatisha tamaa – maisha ya binadamu wa kiudhanaishi.



Usumbufu wa maisha katika tamthilia ya *Amezidi* unatiliwa mbolea, tunapoambiwa kuwa humo pangoni mna mbu – mdudu hatari kwa kueneza ugonjwa wa Malaria. Aidha, kuna mafunza ambao wametapakaa kote pangoni. Tunaambiwa:

Ame: Tulikuwa tukiukimbia ukweli

Zidi: Na sasa?

Ame: Haukimbiliki.

Zidi: Umefika wakati wa kutoweza kukimbia  
ukweli... ah, mafunza! Naona kinyenye...  
naona kichefuchefu...

(uk. 78)

Mazingira yaliyojaa usumbufu wa mbu na mafunza yanaudhi. Ame anasumbuliwa na kuwoko kwa mafunza na hivyo kukosa utulivu. Anasema kuwa ameshakaribia. Anatoa macho zaidi huku akitazama chini. Anauliza juu ya mafunza. Mafunza, mafunza... wamesomba sakafu yote, wamo kutani, darini wananing'inia... mafunza. Anaona kinyenyevu... anajaribu kufumba macho kwa mikono yake na kisha anaiondoa. Anauliza kama bado wapo. Mnawaona na nyinyi jamani? Mafunza... mafunza... mafunza kila pahala! mtume! Wananiingia, Wananiingia mdomoni... wananiingia masikioni kila pahala wananiingia... kila penye tundu wananiingia... mafunza... mafunza. (uk. 84)

Wadudu kama mbu hufyonza damu ya binadamu na kuathiri afya yake. Wadudu hawa wanaweza kuwa jazanda ya Wakoloni ambao waliathiri na kudhoofisha Waafrika kiuchumi, kisiasa, na kitamaduni. Jinsi ambavyo mbu hutapakaa kote pangoni na kueneza Malaria, ndivyo ambavyo Wakoloni walilizingira bara la Afrika na kueneza sera zao huku wakipuuza mahitaji na haki za Waafrika. Waafrika walitekwa na kunyonywa na Wakoloni mithili ya mbu kufyonza damu ya binadamu.

Hali hizi, hujenga na kuendeleza picha ya mazingira ya kiubwege, yaani ulimwengu unaomtesa binadamu, wenye fujo, na unaokatisha tamaa.

Licha ya tamthilia kutuchorea mazingira ya kiuchafu na ya kuchukiza, kawaida ya drama ya kiubwege, hapa na pale hutuonyesha hali ambazo zinapendeza na kuvutia. Katika onyesho la pili, pango ambalo Ame na Zidi wanalitazama kama kasri, kwa kiasi kikubwa linatupatia picha ya kuamini kuwa ni kasri kweli. Mawazo ya mazingira yenye uchafu, mbu, mafunza na giza yanatoweka. Mtunzi pia analipamba kasri vilivyo. Ndani mule kuna zulia kutoka Iran, meza ya kahawa, makabati ya vitabu, mabakuli ya fedha, TV na video, simu ya rangi ya maziwa, na kadhalika.

Aidha, mwandishi amerembesha pango hili kwa kuwapa wahusika wake fikira za umilikaji wa magari ya fahari kama Benz na BMW. Zidi anamwambia Mari:

Gari lipo nje ..hukuliona hapo ulipopita?

Na vitu vyako vyote vimo ndani ya

mabegi , ngoja nikakutolee.

(uk.23)

Zaidi ya gari, kuna watumishi, vyakula vizuri na vinywaji vya kizungu kama Champagne, Beer, Vodka, Whisky na Brandy. Mazingira kama haya hukiuka misingi ya kiubwege.

#### 4.3.1 PANGO

Sehemu kubwa ya mchezo wa tamthilia ya *Amezidi* inaigizwa pangoni. Pango ni taswira muhimu ambayo mwandishi ametumia kuendeleza madhumuni yake. Mohamed ametumia pango kama mandhari ya mchezo wake katika maonyesho manane.

Matumizi ya pango katika kazi za kifasihi hayakuanza leo. Waandishi kadhaa wamewahi kutumia dhana ya pango kuonyesha mandhari ya kazi zao. Katika tamthilia ya *Mashetani*, Hussein ametumia pango kuwamba maudhui ya saikologia ya ukoloni na pia ukoloni mamboleo.

Aidha, inabainika kuwa hadithi ya watu wanaoishi katika ulimwengu wa kidhahania wa kufikirika tu inafanana na ngano ya pango la Plato<sup>4</sup>. Kwa mujibu wa Ayi Kwei Armah, ngano ya pango la Plato inatamba hadithi ya watu waliofungwa na minyororo na kuishi katika kiza cha pango katika kipindi cha maisha yao yote. Ilitokea kuwa, mfungwa mmoja alipata nafasi ya kutoka nje ya pango na akawahi kujionea uzuri na utamu wa jua. Mfungwa huyo aliporudi pangoni, aliwaelezea wenzake juu ya mwangaza na ubora wake lakini hakuna aliyemwamini. Mwenye kuona mwangaza alidharauliwa na kuitwa mzushi na mwehu.

Ngano hii imetolewa kufundisha jamaa kuwa watu wanaoishi katika mazingira na hali tofauti za kilimwengu huwa na maono tofauti. Wale wanaoishi katika ulimwengu finyu kimawazo hawana uwezo wa kufikiria na kuona mambo yaliyoko nje ya duara lao finyu.

Hali hii ndiyo hubainika katika tamthilia ya *Amezidi*. Wakazi wa nchi ya Amezidi wamekubali ulimwengu wao duni na kuukabidhi maana za kipekee na ambazo hazieleweki nje ya muktadha wao. Pango, kwao ni kasri zuri lililosheheni ubora wa kisasa. Katika tamthilia hii, pango linapatiwa maana za aina yake. Kadhia nyingi zinazohusu maisha ya raia wa Amezidi zinaigizwa pangoni. Mazingira haya ni ya kuchukiza na yana nia ya kuashiria uduni, uchafu na maisha yasiyokuwa na thamani- maisha ya Mwafrika.

Mohamed anabadilisha badilisha pango lake na kulipa mandhari tofauti ya kimawazo. Taswira ya pango machoni mwa wasomaji hugeukageuka kutegemea madhumuni ya mwandishi. Onyesho la kwanza na la pili kwa mfano huashiria uasili wa Mwafrika. Pango linaashiria hali isiyobadilika ya maisha ya bara la Afrika. Ni bara ambalo halijaendelea kiteknolojia wala kurutubisha historia ya wakazi wake. Tunaambiwa :

Tendo hili lote linatokea ndotoni mwa Ame  
na zidi ... pahala ni palepale pangoni!

Aidha, tunaambiwa kuwa ,

*(kaketi chini kwenye majani ambayo ni godoro  
lake. Anamtikisha zidi.)* Amka bwana... siku ngapi zimepita?

(uk 12)

Hili ni pango linalokatisha tamaa. Wakazi wake ni maskini sana kiasi cha kukosa malazi mema. Wanalalia majani ambayo ndiyo godoro lao. Mwandishi anatuambia kwamba licha ya uduni huu wa kimaisha , wakazi hawa wanafurahia hali na mazingira yao na ndiposa tunamkuta Zidi amelala usingizi wa pono , usingizi anaoupenda bila shaka.

Mohamed ana wazo kuwa, tangu Mwafrika aanze kuishi ulimwenguni, hajabadilisha nyumba yake Bado anaendelea kuishi na kusherehekea pango lake. Licha ya kuwa maisha yao ni sawa na ya mnyama , Ame na Zidi , hawafanyi lolote kujikwamua kimaisha. Wanabaki wakizembea kazi na kutegemea misaada ya kigeni. Kejeli ni kwamba, hata misaada hiyo ni duni na haina manufaa ila kuendeleza uduni wao katika pango.

Pango pia linageuka na kuwa ofisi, na hata darasa. Mabadiliko haya ni ya kimawazo tu, si ya kihalisia, kwa vile pango ni lile lile lenye mazingira ya kuchukiza.

Katika onyesho la nne tunaambiwa:

Tendo limo fikirani... pangoni ...Tendo  
la shuleni.Zidi ni mwalimu , kaketi  
mbele ya meza ambayo haionekani.Pana  
ubao na chaki ambavyo havionekani.Ame  
(mwanafunzi) ameketi kwenye deski  
lisiloonekana pia.Kuna wanafunzi wapatao  
sabini.Pia hawaonekani ila Ame tu! Mwalimu.  
Zidi anasinzia huku darasa limejaa  
zogo la wanafunzi...kitambo ...kisha kengele  
inasikika kulia ...Mwalimu Zidi anashtuka  
kutoka usingizini...)

(uk.29)

Hili ni pango linalokaribiana sana na pango tulilopatiwa awali. Ingawa mwandishi amelibadilisha kuwa darasa, bado hali ya uduni na utupu inaendelea kubainika. Mandhari ya shule yanafaa kuwa na vifaa muhimu vya kimasomo, mwalimu mwenye ujuzi na uwezo wa kumiliki darasa, pamoja na wanafunzi watiifu. Hali inayosawiriwa ni kinyume kabisa na matarajio hayo. Hamna ubao, deski na chaki ila zile za kimawazo tu! Mwalimu mwenyewe hatambui wajibu wake, amelala. Kulala kwake ni sawa na kule kwa Zidi katika onyesho la pili. Tabia ya kulala haijabadilika. Zidi katika onyesho la pili anaamshwa na Ame, na Mwalimu anaamshwa na mlio wa kengele. Kwa upande wao, wanafunzi ni zogo si watiifu na hawatambui kuwa wamo darasani. Tena ni wanafunzi wengi sana, sabini, idadi ambayo ni kubwa na ngumu kwa mwalimu mmoja wa somo la fizikia. Haya ni mazingira yasiyopendeza na yanayosheheni sifa za kiubwege.

Labda mwandishi amepuuza tendo la kuyafanya mandhari haya yatangamane na hali na muktadha wa kidarasa ili kukejeli maendeleo ambayo Waafrika wanajivunia. Nchi nyingi za bara hili zimesahau wajibu wao wa kusanifu maendeleo, na hivyo kubaki zikitegemea misaada kutoka mashirika ya kigeni. Katika onyesho la nane, Ame na Zidi, wanasemezana:

Ame: Tumelala au tu macho?

Zidi: Sijui.

Ame: Ndiyo ujue tu !

Zidi: Madawa tununue? kwa nini hatufanyi yetu?

Ame: Si mpaka tuvumbue kwini!

Zidi: Kwa nini hatuvumbui ?

Ame: Tununue tu!

Zidi: Kwa nini?

Ame: Ndiyo raha, ndiyo kuendelea.

Utafiti wa nini? Uvumbuzi wa nini?

Si tununue tu , tuna fedha bwana !

(uk.66)

Mazingira ya pango ni ya uasilia na huwa hayatoi fursa kwa wakazi wake kujielewa na kutafuta mbinu za kuboresha maisha yao. Tunawakuta Ame na Zidi katika hali ya kutojali. Wahusika hawa hawana haja ya kuufahamu ulimwengu kwa mujibu wa tajriba zao na ujuzi wao. Kwao, hakuna haja ya kujitia katika tendo la kufikiri ili angalau wapate unafuu wa maisha.

Uasilia wao unabainika pia, pale ambapo tunawakuta wakipokea misaada na kuitumia tu vile ilivyo bila kuisafisha wala kuiandaa. Isitoshe, katika pango lao, hamna kisu, kibiriti, mbolea, wala trekta. Elimu ya nchi hii haijasaidia wananchi kuvumbua vifaa muhimu vya kurahisisha maisha ya binadamu:

Mwanafunzi: Nikalime.

Mwalimu: Ukalime.

Mwanafunzi: Ardhi i wapi?

Mwalimu: Ardhi halia – ardhi tupu ipo inakungojea!

Mwanafunzi: Trekta?

Mwalimu: Kiserema.

Mwanafunzi: Mbolea?

Mwalimu: Mavi ya ng'ombe na samadi!

Mwanafunzi: Ng'ombe wamekufa kwa ukame.

(uk. 38)

Inasikitisha kwamba, mazingira yanayozunguka maisha ya wahusika hawa ni duni zaidi kuliko hata hali walizopitia mababu zetu. Kama mababu zetu waliishi katika pango, basi inabainika, pango lao lilikuwa nafuu kidogo ukililinganisha na lile la akina Ame na Zidi. Pango la Mwafrika, linaendelea kufifia kiubora na kuwa baya zaidi.

Kutokana na matukio yanayosawiriwa katika tamthilia ya *Amezidi* na riwaya ya *Wema Hawajazaliwa*, inadhihirika wazi kuwa watunzi hawa wa fasihi, wanaelekea kukata tamaa. Uozo wa bara la Afrika unawapa kero.

Ubwege husawiri uozo *Amezidi* inazungumzia uozo wa kimawazo, kifikira, ambao ni shida kubwa inayoikabili bara letu la Afrika. Kwa upande wake, *Wema Hawajazaliwa* imejikita katika uozo unaotokana na ufisadi na matumizi mabaya ya mamlaka. Ni dhahiri kuwa, bara la Afrika limepoteza heshima yake kutokana na uozo huu wa viongozi dhalimu, viongozi ambao wanaiga kikasuku mambo na vitu vya kigeni.

#### 4.3.2 UTUPU

Dhana ya utupu huashiria uduni wa maisha katika tapo la ubwege. Mohamed katika tamthilia ya *Amezidi* anasukumwa na nia ya kuonyesha kuwa Waafrika wanaishi na wamekwama katika maisha duni yanayokatisha tamaa. Bara la Afrika hukosa uasilia wa teknolojia, uvumbuzi wa kimsingi, na mawazo halisi ya kimaendeleo. Mwandishi anatupatia jukwaa lililo tupu kuashiria hali hii ya utupu wa maisha ya Mwafrika.

Tamthilia ya *Amezidi* imejikita sana katika misingi ya kidhahania. Licha ya kusawiri utupu wa kijukwaa, mtunzi anatupatia wahusika wawili Ame na Zidi. Ni wahusika ambao hawatendi lolote la maana ila kusemezana wao kwa wao. Mandhari ya kuigizia kwa kiasi kikubwa yanafanana kutoka mwanzo hadi mwisho wa tamthilia. Mwandishi habadilishi mandhari ya tamthilia yake kinyume na tamthilia za kihalisia.

Tunaweza kusema na kuamini kuwa, lengo la tamthilia la kuonyesha uduni na utupu wa maisha katika nchi ya *Amezidi*, Afrika, limemfanya asiwakuze wahusika wake. Hata hivyo, mwandishi amewapa nafasi ya kuigiza kama wakuu katika asasi mbalimbali za uongozi hususan ofisini, shuleni na serikalini. Hali ya Ame na Zidi haibadiliki na ni sawa na vibonzo. Maisha kwao ni mchezo na hivyo kama vinyago wanakaa tu na kusubiri majaaliwa. Hawana uwezo wa kufikiri wala kuvumbua, ndiposa hali yao tunapowakuta na tunavyowaona mwanzoni mwa tamthilia ni karibu sawa na walivyo wakati mchezo unapoisha. Badiliko la maana kwao, ni kuwa wanakufa hatimaye na vifo vyao vinafanana.

Baada ya kufa, Zidi anaendelea kuishi kwa vile tamthilia inatupatia sauti yake. Hali hii huashiria utupu wa maisha – maisha si kitu cha maana bali ni sauti tu! Sauti hii inatupa hisia za kuathiriwa kikweli kwa Waafrika kutokana na njama za mkoloni. Inaashiria

kuenea kwa mawazo ya kijinga ya Mwafrika hata baada ya kifo cha viongozi wao. Mwandishi hapa anadunisha fikira na mielekeo ya viongozi wa Kiafrika.

Dhana ya utupu pia inabainika kupitia mazungumzo ya wahusika Ame na Zidi. Mara kwa mara wanajiingiza katika maongezi yasiyokuwa na maana. Maneno yao hayana mashiko na yanaendeleza kuchanganyikiwa kwao. Hii ndiyo sababu wanashindwa kutofautisha kati ya dhana za vinyume mfano swali na jibu, vicheko na vilio, kifo na uhai, kulala na kuamka, na kadhalika. Mazungumzo ya bosu na msaidizi wake ni mfano wa utupu na kuchanganyikiwa:

Msaidizi: Naam, Bosu... nipo kwa ajili yako!

Bosu: Kwa ajili yetu.

Msaidizi: Yako.

Bosu: Yetu.

Msaidizi: Yako.

Bosu: Yetu.

Msaidizi: Yetu.

Bosu: Sawa.

Msaidizi: Sawa.

(uk 40)

Mazungumzo yasiyoandamana na vitendo vya maana, ni utupu wa hali ya juu. Hawa ni wahusika ambao kihalisia tungetarajia wajikaze na kujitolea muhanga kuendeleza sera na matakwa ya nchi yao. Kinyume na matarajio yetu, mwandishi anawasawiri kama watu wazembe wenye ufisadi uliokithiri na ambao hawafikirii la maana ila kukaa tu na kupiga domo, huku wakisubiri vya bule. Hawa ni wahusika wa kiubwege, wanaoishi katika nchi yenye ukame. kavu, utupu.



#### 4.4 MATUMIZI YA NYIMBO

Nyimbo sawa na ushairi ni kipengele cha fani ambacho Mohamed ametumia kuendeleza maudhui yake. Takriban nyimbo zote ambazo mwandishi ametumia katika tamthilia ya *Amezidi* zinapingana na mtazamo wa kiubwege. Mchezo unaanza kwa dondoo la kishairi kutoka tamthilia ya *Kilio cha Haki* yake Alamin Mazrui.

Kwa nini ewe bara la Afrika, ewe nchi  
uliyejipamba kwa weusi, ewe roho ya  
kizazi chetu. Tukutiliaye mbolea siku  
baada ya siku kwa kutaraji utatuzaliya  
matunda ya umoja wetu

Niambiye –

Kwa nini ungali moyoni mwangu

Kwa nini ungali mpenzi wangu

Katika saa hii ya huzuni?

Ni hii njaa ya fisadi iliyotuzunguka?

*Kilio cha Haki* (uk. 5)

Hiki ni kifungu ambacho kinasheheni uhalisia wa harakati za kujikomboa na kuleta haki, usawa na maendeleo ya kiuchumi katika jamii. Ni dondoo ambalo hubeba maudhui mazito ya kiukombozi kulingana na mtazamo wa Umarx. Shairi hili linatupa mwangaza wa uwezekano wa bara hili kupata maendeleo ikiwa viongozi watajitolea kutekeleza wajibu wao ipasavyo. Hili ni wazo la kihalisia, la matumaini, wazo ambalo linapingana na mwelekeo wa tapo la ubwege. Ki-marx, binadamu anayeteseka na anayedhulumiwa, hupatiwa matumaini ya mafanikio ikiwa atajikaza na kutetea haki yake. Matajiri wanaomiliki mali na nafasi za juu za uongozi huzozana na wafanyakazi, wachochole, ambao ni wanyonge wasiokuwa na chao. Hali hii ya utabaka inabainishwa kupitia dondoo hili. Ubwege humtazama binadamu kama kiumbe duni ambacho kimetupwa ulimwenguni kuteseka bila matumaini ya kuokolewa ila kukaa tu na kusubiri lisiloepukika, kifo chake.

Aidha, tunapata ‘Wimbo wa Mzee’, wimbo ambao sawa na dondoo kutoka *Kilio cha Haki*, unapitisha haja ya kutumainia mema siku zijazo. Mzee anatuambia kwamba, makosa yalifanywa na kizazi chake, ni kama anatubu dhambi zake. Hata hivyo hajakata tamaa. Kwake bado kuna matumaini ya chembechembe za furaha kwa vile ameacha vijana – kizazi kipya ambacho anatarajia kitaleta maendeleo yanayohitajika. Anaimba:

Jana nilijua imepita na majuto

Leo najua haipo

Kesho haijazaliwa kamwe

Kesho nitapoonaa ardhi hii

matunda mema inazaa.

Kuneemesha kila mtoto wake

Na ule mzigo mpya n’lojitwika mwenyewe

kwa hiari n’lojitwika

Mwepesi umekuwa.

(uk. 3)

Mzigo wa Mzee umekuwa mwepesi kwa kufikiria mafanikio yatakayojiri barani Afrika wakati kizazi kipya kitakapochukua hatamu za kuongoza. Hata hivyo, ni matumaini ambayo hadi mwisho wa tamthilia hayabainiki.

Ubwege hupingana na suala la matatizo, mzigo wa binadamu kupungua kiuzito na kuwa mwepesi wa kubebeka. Badala yake, mzigo huo huendelea kuzidi kiuzito na baadaye kumwangamiza binadamu kwa vile maisha ni kufa pole pole. Aidha, wazo la kufikiri kuwa siku moja wenye njaa watapata shibe kutokana na ardhi kuzaa matunda mema linakaidi teneti za kiubwege. Wimbo wa mzee kwa ujumla, ingawa una chembechembe za mateso, huzuni na kujuta, kwa kiasi kikubwa huendeleza kigezo cha matumaini kinyume na mwelekeo wa kazi za kiubwege.

Wimbo wanaoimba Ame na Zidi katika onyesho la tatu unaendeleza majivuno ya Waafrika. Rangi nyeusi inaonewa fahari na wahusika hawa ingawa umuhimu wake haudhihiriki bayana. Ni wimbo ambao mtunzi anautumia baada ya kumsawiri Mari. Mari ni mhusika ambaye amekengeuka kiasi cha kudharau na kutotambua mambo na hali ya bara la Afrika, bara lake. Mari anathamini na kutukuza ya Mzungu. Wimbo huu basi unaelekea kuwakashifu Waafrika wanaodunisha hali yao kwa kufuata ya kigeni. Ame na Zidi wanaimba:

Tunaimba wimbo huu  
Wimbo wa fahari na makuu  
Tunaimba kuisifu rangi hii ya fuu  
(wanaonyesha ngozi zao)  
(uk. 27)

Huu ni wimbo wa kiuhalisia, hauna maudhui ya kiudhanaishi. Hali ya Waafrika ambao ni maskini, kutegemea na kufurahia visivyo vyao kama magari, vifarua, mavazi na vyakula, ni dhahiri. Hata hivyo, mwishoni mwa wimbo huu, tunapata miale ya ubwege. Taswira ya watu wazembe na wasio na uwezo wa kutekeleza lolote lenye manufaa ila kungojea majaaliwa hubainika. Wanatuambia:

Na kazi, ya nini kazi?  
Haina haja kazi!  
Ya nini uvumbuzi?  
Tu huru: tumejitawala!  
Tuna kila kitu  
kwa fedha zetu  
Tuvumbue, tuvumbue nini?  
Tutawalipa wanaovumbua...  
Wanaotuvumbulia (uk. 28)

Ni wimbo unaokejeli Waafrika kwa kujidai kuwa wako huru huku wakiendelea kumtegemea Mzungu. Aidha, unatupatia picha inayokaribiana na ya Vladimir na Estragon katika *Waiting for Godot*. Wahusikia hawa wanasawiriwa kama vibonzo kwa kukaa, kupiga domo ovyo ovyo huku wakimngojea Godot. Ni wahusika ambao hawana hata uwezo wa kuvua viatu (uk. 9).

Tukumulika wimbo wa Mwalimu na Wanafunzi tunapata maudhui yanayopingana na mkabala wa kiubwege. Wimbo huu unabeba ujumbe wa kihalisia kuhusu bara la Afrika. Malighafi za Mwafrika ni nyingi lakini Mwafrika amezidi kuteseka na kutawaliwa na Mzungu kwa miaka mingi sasa. Mwandishi analikejeli bara la Afrika kwa kulilinganisha na tajiri aliyelala na kuacha mali yake ikiibiwa na watumishi wake. Wanaimba hivi:

Tajiri kashiba,  
Kashiba, kashiba  
Ndiyo maana kalala  
Ashibaye hulala  
Huku wengine humpakuwa  
Ah-kuvumbua kwa nini?  
Alalaye hafikiri, huota!  
Ah-kuvumbua kwa nini?  
Alalaye huvumbua ndotoni  
Ah-na kuunda kwa nini?  
Alalaye huunda ruwiyani.....

(uk. 34)

Hali hii ya Waafrika kufurahia uhuru wa bendera na kusherehekea kulala kwao huku wakitegemea vya ng'ambo hubainika pia katika wimbo mwingine wanaoimba Ame na Zidi katika onyesho la nane. Nchi za Kiafrika zilitawaliwa kwa miaka mingi. Baada ya kuzinduka, Waafrika walipigana vikali na kuwafukuza Wakoloni. Waafrika wakaanza kujiongoza wenyewe. Badala ya kufanya wajibu wao kazini kwa kutia bidii na kurekebisha hali ya maendeleo ya bara lao, viongozi hawa waliiga mbinu na mielekeo ya Kizungu na kuitumia. Hali hii iliendelea na bado inaendelea kuzorotesha uchumi wetu; bado Mzungu anazidi kututawala kisiri. Haya ni matendo ya kihalisia na yamo katika wimbo huu. Wimbo unaanza hivi

Miaka mia tulikuwa vile vile  
leo tuko hivi hivi  
Tu papo au tumeendelea  
Tu macho tumelala  
Au tumelala tu macho.  
(uk. 68)

Katika kimalizio chake, mwandishi anatupatia wimbo mwingine. Mara hii si wimbo wa mzee ambaye amekula chumvi nyingi, ni Wimbo wa Mtoto Asiyezaliwa. Wimbo huu umebeba maudhui mazito ya matumaini, maudhui ambayo yanapuuza kabisa kanuni za kiubwege na imani za kidhanaishi. Tukitazama kichwa cha wimbo huu yaani “Wimbo wa Mtoto Asiyezaliwa”, tanapata hisia za mama mjamzito ambaye anatazamia kujifungua. Kila mzazi huwa na matumaini ya kufurahia matunda ya jasho la uzazi wake. Hali hii inapingana na mtazamo wa drama ya kiubwege, chambilecho Kitchin (1966:31):

Haja kubwa ya drama ya kiubwege ni kuwoko  
kwa binadamu katika hali ya kukata tamaa, na  
isiyo na matumaini wala maana yoyote ulimwenguni.  
(Tafsiri yetu)

Bila shaka, wimbo huu si wa kukatisha tamaa, si wa kiubwege. Hali hii inathibitika zaidi tunapokumbana na wimbo wenyewe. Tunaimbiwa kuwa:

Huu ni mwelekeo wa uhai  
wa watakao kuishi  
Kuishi na siyo kuwepo!  
(uk. 86)

Kiubwege, suala la maisha, uhai na kifo husisitizwa. Binadamu huwepo tu ulimwenguni akisubiri hatima yake, kifo. Hivyo basi, maisha hayawezi kuwa na furaha, na uhai si jambo au kitu cha milele. Maisha angalau, ni kufa pole pole na binadamu hana hiari ya kuchagua kati ya kuishi au kufa, ila kufuata mkondo wa maisha kulingana na majaaliwa. Ukweli huu wa tapo hili unapingwa na ujumbe tunaopata katika wimbo huu, hasa kauli kama vile “uhai wa watakao kuishi”.

Aidha, katika kimalizio hiki, mwandishi anakaidi imani ya kidhanaishi kuwa kitu cha mwisho ambacho binadamu anangojea ni kifo. Madai ya kuwa wafu na vilema wote wataponywa ni imani ya kidini ambayo inapingwa na muktadha wa ubwege. Binadamu hana shuruti yoyote ya kumtegemea wala kumtukiza Mungu. Ulimwengu tuliomo ni dhalimu na fikira za binadamu kuokolewa siku moja baragumu itakapolia ni ndoto, mzaha tu.

Kimalizio hiki ni matumaini ya mwandishi kuwa siku moja Afrika itazaliwa upya na maendeleo kupatikana. Viongozi wa Kiafrika pamoja na mashirika ya Kiafrika kama Muungano wa nchi huru za Afrika (OAU), COMESA, ECOWAS, SADCC na IGADD, wanashawishiwa kutekeleza wajibu wao ili kurudishia bara hili heshima yake iliyopotea. Ni dhahiri kuwa mwito kama huu ni wa kihalisia; unakiuka mawazo ya kiubwege.

#### 4.5 MATUMIZI YA SAUTI, KICHEKO NA KILIO

Sauti, kilio na kicheko ni baadhi ya vinyume ambavyo mwandishi ametumia katika tamthilia yake kuendeleza maudhui yake. Waandishi wa tamthilia hutumia vicheko na vilio kama njia ya kukejeli matendo ya wahusika wao. Tamthilia *Mashetani*, yake E. Hussein ni mfano wa kazi ambazo zimesheheni matumizi ya vicheko na sauti.

Kuna matumizi kadhaa ya sauti katika tamthilia ya *Amezidi*. Mwandishi ametumia sauti kuendeleza hali ya utupu inayolizunguka pango, nchi ya Amezidi. Sauti hii aghalabu husikika katika masikio ya wahusika kama mwangwi. Sauti kwa ujumla imetumiwa kama njia ya kudhihaki matendo ya wahusika. Mambo mengi wanayofanya Ame na Zidi ni ya kijinga, kipumbavu na hayana mashiko. Hivyo basi, sauti inaingilia kati kama njia ya kuwakumbusha wahusika hawa kuwa wao ni maskini, wanaoishi katika bara lenye mateso mengi, na sharti wajizatiti ili kulikomboa bara lao. Sauti

husaidia kuwatia changamoto ili wajisake vizuri na kujielewa. Katika onyesho la tatu, kuna sauti ya Ame:

Mari: Hodi mpaka ndani.

Zidi: Ndani, ndani mwako....kaa...  
keti kwenye sofa (sofa halipo)

Sauti ya

Ame: (inacheka kutoka nyuma ya jukwaa)  
Ha, ha, ha...

Mari: (Bado amesimama!) Nikae wapi?...  
(liko wapi hilo sofa?)

Sauti ya

Ame: (Kutoka nyuma ya jukwaa) Ha, ha, ha...  
(uk. 19-20)

Sauti hii ya Ame inatumiwa kuwakejeli Zidi na Mari kutokana na mazungumzo na matendo yao ya kidhahania – wanazungumzia mambo yasiyokuwepo. Zidi anaamini kuwa kuna maendeleo na vitu vingi ndani ya pango lao ambalo wanaliita kasri, huku Mari akikataa katakata kwamba kuna lolote la maana katika pango hilo. Sauti hii inatumiwa kutuonyesha mikinzano hii baina ya Mari na Zidi. Sauti hii ya Ame, hata hivyo haisaidii wahusika hawa kujipima upya na kujielewa.

Kuna sauti ya redio, sauti ambayo inajitokeza katika mandhari ya darasani wakati mwalimu na wanafunzi wake wamelala:

Hii ni sauti ya Amezidi... Taarifa  
tuliopata punde hivi inasema  
kwamba katika kijiji cha Fujo,  
maelfu kwa maelfu ya watu  
wanakufa kwa njaa kila siku...

(uk 35)

Hii ni sauti ya idhaa ya Amezidi. Ni sauti inayobainisha ukweli juu ya bara la Afrika, bara ambalo limekumbwa na ukame, vita vya wenyewe kwa wenyewe, na umaskini. Labda ndiyo sababu linaitwa Kijiji cha Fujo.

Kuna sauti ya Zidi. Ni sauti ambayo tunapata baada ya kifo cha Zidi:

Sauti: Wako wapi hao mafunza?

Ame: Wewe huwaoni eti, kwa kuwa umeshapita hatua ya uhai, uko katika hatua ya ufu.

Sauti: Nani mfu hapo, mimi au wewe?

Ame: Awe nani tena? Aaaaaaaa.

(Anazidi kugaragara)

Zidi: Nini?

Ame: Tumbo...tumbo...tumbo...

Yallah, mtume...

sina hata mtu wa kunisaidia...

hata wa kunisaidia kwenda msalani...

(uk. 84)

Onyesho lote la kumi linaigizwa na Ame pamoja na sauti ya Zidi. Sauti hii ni ishara ya kujitambua na kujielewa kwa Zidi baada ya kifo. Mwandishi anaelekea kusema kwamba, baada ya mateso ya miaka mingi, mateso ambayo yamemwangamiza Mwafrika (kifo cha Zidi), Mwafrika amepata nafasi ya kujitambua na kuelewa ujinga wake, ni hali ya ubwege.

Sauti hii ya Zidi, ni fundisho kwa wenzake kama Ame ambao wamebaki. Sauti ina shabaha ya kumshurutisha Ame ajitafute na kubadili mwelekeo wake wa maisha. Hata hivyo, Ame naye anakufa, na kifo chake kinatokea katika mazingira na hali sawa na kile cha Zidi. Kifo cha Ame, ni ishara kuwa hata baada ya kuzinduliwa, Mwafrika bado hajarekebisha hali yake. Hawa ni wahusika ambao hawana haja ya kuboresha hali yao, wamezoea kufurahia uduni wao.



Mohamed ametumia kicheko kuonyesha ukengeushi wa wahusika wake. Vicheko vimetumiwa kuelezea utata na ukinzano ulioko katika maisha ya watu wa Amezidi. Wafula (1999:81) anasema:

Vicheko vya wahusika ni majoho  
ya kinafiki yanayosetiri vilio vyao.  
Katika sehemu kadhaa za tamthilia,  
kicheko kimehusishwa na kilio.  
Kicheko kimetumiwa kuficha hali  
halisi ama wanayoogopa au  
wanayokataa kuikubali wahusika.

Katika onyesho la nne, mwandishi anatupatia vicheko na vilio darasani:

Mwalimu: Mnacheka tu...kicheko tu...  
kicheko...kicheko...lakini  
mnaloulizwa hamjui, kicheko.

Wanafunzi kwa

Pamoja: Hapana, mwalimu...kilio...kilio...kilio

Mwalimu: Tulie pamoja basi

Mwalimu: Tucheke basi (uk. 31)

Wanafunzi wanajikuta katika hali tatanishi. Mwalimu wao ni duni, na hafai lolote. Wanayofundishwa hayana maana kwao, na wao wenyewe ni zogo. Wanafunzi wanalia kwa sababu ya kugundua kwamba wamepoteza muda kujidanganya kuwa wamesoma. Mwandishi anakejeli elimu wanayopata wanafunzi na hivyo kutoa kilio kuashiria hali duni na ya kusikitisha ya elimu hii.

Kwa upande mwingine wanafunzi wanamchekea mwalimu wao ambaye hana ujuzi wa kuwaelekeza darasani. Inabainika kuwa si mwalimu si mwanafunzi anayejua wala kuelewa mada iliyo mbele ya darasa.

Mwalimu: Vizuri.

Mwanafunzi: Kwa vipi?

Mwalimu: Nyambizi.

Mwanafunzi: Amefanyaje?

Mwalimu: Maana yake nini?

Mwanafunzi: Maana yake nini?

Mwalimu: Nakuuliza wewe (uk. 31)

Aidha, wanafunzi wanajicheka wenyewe kwa kutokuwa na uwezo wa kujisaidia. Hawajui lolote na mwalimu wao hana msaada wowote kwao. Hali hii inaendeleza imani ya kidhanaishi kuwa, binadamu hana uwezo wowote wa kuibadilisha hali yake wala Mungu hana lolote la manufaa kwa binadamu ulimwenguni. Hivyo basi, inadhihirika wazi kuwa, wahusika wa Mohamed wanacheka ili wasilie kutokana na hali yao ya ukengeushi, kusikitisha, kuhuzunisha na kukatisha tamaa. Ni dhahiri kuwa vicheko vya Ame na Zidi, wanafunzi na mwalimu, na kadhalika vinachukiza na kukatisha tamaa zaidi hata kuliko vilio vyao.

Ndoto za maendeleo wanazoamini Ame na Zidi pia zinadhihakiwa. Kicheko cha Mari kinakejeli imani potovu za maendeleo zinazofuatwa na Ame na Zidi. Matendo yao yanawacheka.

Ame: Utajiri wetu au sivyo?

Zidi: Enh!

Kicheko

cha Mari: Ha, ha, ha...

Zidi: Nani huyo anayecheka?

Ame: Nafsi yako.  
 Zidi: Nafsi yangu imefanyaje?  
 Ame: Inajicheka.  
 Zidi: Labda inajicheka au inatucheka  
       Mimi na wewe.  
 Ame: Sasa?  
 Zidi: Sasa nini?  
 Ame: Kuhusu Mari  
 Zidi: Nilimwonesha kasri letu.  
 Kicheko  
 cha Mari: Ha, ha, ha...

(uk. 24-25)

Vicheko hivi, ambavyo havijulikani vinakotokea vinatumiwa na mwandishi kuwakilisha mtazamo wa mapinduzi ya kimaendeleo ambao unahitaji viongozi na raia kwa ujumla kama Ame na Zidi, wajitolee katika kujijua na kujitambua vyema zaidi ili waweze kuboresha maisha yao. Hata hivyo, vicheko hivi haviwasaidii kurekebisha hali zao. Ni hali inayoendeleza vipengele vya drama ya kiubwege.

#### 4.6 LUGHA NA MAWASILIANO

Wahusika wa kiubwege wanapotumia lugha inayotatiza mawasiliano, wanafanya hivyo kimakusudi ili kudhihirisha kuwa lugha imeshindwa na jukumu lake la kimawasiliano, inajirejelea yenyewe. Mawasiliano, au mazungumzo yanayovunja kaida za kimawasiliano na yasiyo na mantiki mwafaka ni dhihirisho la lugha kujirejelea yenyewe kuwa imeshindwa katika wajibu wake.

Tamthilia za kiubwege hutazamwa kama vitendawili mzunguko, vichekesho vya huzuni, kejeli kwa maumivu, mizaha ya kipumbavu na masihara dhanaishi. Ni aina ya michezo inayoafikiana na usemi wa Sigmund Freud<sup>5</sup>:

Binadamu anaogua kutokana na  
maambukizo ya huzuni; amefanywa  
bubu kutokana na kuporomoka kwa  
lugha na mantiki, na anaweza tu  
kuipaaza sauti yake hoi kwenye  
ombwe lisilo na furaha.

(Tafsiri yetu)

Kawaida, lugha ya sanaa ya kiubwege hukwamiza mawasiliano. Njogu na Chimerah (1999:75) wanaeleza kuwa lugha ya sanaa ya kiubwege hairahisishi mawasiliano; badala yake hukinzana na jukumu lake la mawasiliano. Ugumu wa kuishi unaashiriwa na ugumu wa mawasiliano katika sanaa ya aina hii. Hii ni sanaa inayoonyesha uvunjaji wa kaida za lugha, na inasawiri mdundo wa uvunjikaji wa lugha inavyotumiwa kwa minajili ya mazungumzo mengi ya kidhahania; kwa mfano, uhusiano wa kifo na uhai, kulala na kuamka.

Hali hii ndiyo hubainika katika tamthilia ya *Amezidi*. Katika onyesho la kwanza, Ame na Zidi wanajadiliana:

Ame: Suruali au ghuba?

Zidi: Suruali.

Ame: Suruali imeliwa na panya.

Zidi: Panya ameliwa na suruali...  
na nyani haoni ghubaye.

Ame: Suruali imeliwa na panya  
na hapa hapana nyani...

Zidi: Aha... unasema mhogo uliovunda?

(uk. 5)

Haya ni mazungumao yasiyokuwa na mantiki wala maana yoyote. Wanazungumza juu ya suruali, kisha ghafla kuingilia mhogo bila kutuonyesha mwingiliano wowote. Haya ni mawasiliano ya kiubwege, ambapo lugha na kaida zake huvurugwa ili kuashiria hali ya maisha yenye fujo.

Drama ya kiubwege hubainisha tanzia ya lugha kama chombo cha mawasiliano. Katika sanaa ya aina hii, tunapata kuwa mawasiliano yanakwamizwa makusudi. Hakuna mawasiliano ya moja kwa moja kwa sababu binadamu ameshindwa kujifahamu, hana uwezo wa kudhibiti uhusiano unaofaa na binadamu wenziwe, au hata na mazingira au ulimwengu wake.

Lengo la drama hii ya kiubwege ni kuonyesha kuwa binadamu ameshindwa kuidhibiti na kuitawala dunia yake sawa na kama vile alivyoshindwa kudhibiti chombo chake cha mawasiliano, yaani lugha. Waandishi mashuhuri wa kiubwege kama Ionesco na Beckett wanathibitisha hali hii ya lugha inayokatisha tamaa, lugha ambayo haitekelezi lolote la maana ila kuvuruga mawasiliano.

Katika mtazamo wa kiubwege, ukanganyifu wa lugha unaojibainisha kwenye sanaa ya kibwege ni jazanda ya ukanganyifu wa jamii isiyoweza kujielewa. Katika drama ya aina hii, lugha hutumiwa si kama chombo cha mawasiliano bali kama sehemu ya mchezo. Lugha hutumiwa kuonyesha upotevu na kuchanganyikiwa kwa binadamu kutokana na hali yake ulimwenguni. Lewis (1962:259) anasema:

Binadamu yuko pweke na amepotea  
katika ulimwengu ambamo Mungu  
amemtupa; sayansi na kufikiria ni  
madanganyo; binadamu ametekwa  
na ulimwengu katili. Kitu dhahiri  
ambacho kimebaki ni kifo, ambacho  
ni kitendo cha mwisho cha ubwege.  
*Mawasiliano hayapo tena kwa vile  
hata lugha imekufa.* Ulimwengu ni fujo.  
(msisitizo ni wetu) (Tafsiri yetu)

Tamthilia ya *Amezidi* na zingine za ubwege zinaafikiana na usemi huu.

#### 4.7 PLOTI

Ploti kwa kifupi ni ule msuko wa vitushi na namna vitushi hivyo vinavyosababishana; ni sehemu muhimu ya tamthilia. Ploti nzuri, aghalabu hubainika pale ambapo kuna migogoro, na mgogoro mmoja husababisha mgogoro mwingine, na mivutano hiyo ndiyo inayosukuma mbele tamthilia hadi kufikia upeo wa juu.

Tamthilia za ubwege hupuza kipengele cha ploti. Kazi hizi hukosa migogoro ambayo tunaweza kusema kuwa imejengwa na kusuluhishwa. Hivyo basi ni vigumu kubainisha kilele cha kazi ya kiubwege. Kile ambacho hubainika katika tamthilia za kiubwege ni mzunguko wa matukio. Maisha ya binadamu huwa ni tendo la kuzunguka duara lile lile bila kusonga mbele.

Waandishi wa tamthilia za ubwege huashiria hali hii kwa kutoa ploti mzunguko. Badala ya mtiririko wa vitushi kama ilivyo kawaida ya tamthilia za kiuhalisia, sanaa hii ya kiubwege huipa hadhira mpangilio wa kauli na taswira zinazolingiana na kushajiishana<sup>6</sup>.

Katika *Amezidi*, Ame na Zidi wanajihusisha na vitendo ambavyo vinawafanya wategemea na kusubiri misaada. Kusubiri huku na kutegemea huku kwa misaada ndicho kigezo cha maana kinachozunguka matendo yao. Hatuoni vitushi vikisababishana bali matendo yanaendelea na kurudi pale pale yalipoanzia; ni mzunguko wa matendo.

Hali hii ndiyo hubainika katika tamthilia ya Beckett, *Waiting for Godot*. Tunapatiwa mabwege wawili Vladimir na Estragon ambao hawatendi lolote la maana ila kukaa chini ya mti wakimsubiri Godot. Kusubiri huku kunatawala tamthilia nzima kwa vile hadi mwishoni, bado wahusika wanaendelea kumtarajia Godot, ambaye pengine atawaokoa kutoka kwa changa walilomo. Godot katika *Waiting for Godot* ni sawa na wafadhili katika *Amezidi* ambao wahusika wanawasubiri wawape misaada ingawa misaada hiyo haifai matumizi yao. Haya ni maisha ya mzunguko na ambayo yanaafikiana na mtazamo wa kiubwege chambilecho Esslin (1961:365):

Nyingi za tamthilia za kiubwege  
huwa na muundo wa kiduara,  
ambapo zinaisha vile ambapo  
zilianza; zingine huendelezwa na  
kukua kwa hali iliyotangulia.  
(Tafsiri yetu)

Ploti ya mzunguko huashiria maisha ya binadamu ambayo kiubwege kamwe hayasongi mbele bali yanaendelea kuzunguka duara katili, ulimwengu dhalimu, na ambao humtesa.

Hali ya Mohamed kutokuza wahusika wake inaifanya ploti ya tamthilia ya *Amezidi* kutatanisha. Ploti tunayopatiwa si ploti kulingana na kaida za kiuhalisia. Mwandishi anapuza suala la ploti na hivyo kuitia tamthilia yake katika mkabala wa tamthilia za kiubwege, tamthilia ambazo zinabainisha mzunguko wa matukio huku zikipuza kipengele cha ploti.

Maisha ya mhusika kikawaida yanahusiana na ukuzaji wa ploti. Ploti nzuri ni ile ambayo huonyesha mabadiliko ya maisha ya wahusika katika mpito wa wakati. Kinyume na hali hii, *Amezidi* imetumia wahusika wasiokuwa na mielekeo au nia ya kuboresha hali zao za kimaisha. Kwa kufanya hivyo, tamthilia hii inaua ploti yake. Wafula (1999:78) anasema:

Mohamed anadai kwamba hapana haja  
kuwapa watu historia iwapo hawastahili  
historia hiyo. Wazo hili lina mizizi  
katika ghadhabu za mtunzi juu ya juhudi  
duni alizofanya Mwafrika katika harakati  
za kujitawala.

Inabainika kuwa, Mohamed ameathiriwa na mtazamo wa kiubwege. Kiubwege, wahusika hawaendelezwi kihistoria. Wahusika huonyesha ubatili wa maisha ya binadamu katika mazingira dhalimu yanayokatisha tamaa. Pengine Mohamed ameiga mtindo wa maandishi kama Samwel Beckett, *Waiting for Godot*, *End game* na Eugene Ionesco, *The Lesson*, *The Chairs* na *The Killer*.

Irungu (1999) anaeleza kuwa maisha ya binadamu ni safari ya kuzunguka kwenye duara. Katika *Amezidi* wahusika wanazunguka kwenye shida ya umaskini na uhitaji wa misaada. Hali hii pia hubainika katika kazi za kiudhanaishi kama za Kezilahabi. Mwandishi huyu katika *Mzingile* (uk. 5) anatumia sitiari ya sayari na jua kuonyesha jinsi maisha ya binadamu yalivyo. Sayari huwa mbioni kulizunguka jua, vivyo hivyo binadamu huwa mbioni kuusaka ukweli na uhalisi wa maisha yake, na ni kama kwamba huwa mbioni kulizunguka jua lake lisiloonekana. Maisha ni mzunguko, ni duara. Binadamu amefumbwa macho ndiposa anatafuta kitu kilicho wazi, ukweli wa maisha yake ulimwenguni.

Katika *Amezidi*, Mohamed amesawiri wahusika wanaoishi katika pango. Pango ni ishara ya mzunguko. Ndani ya pango sawa na ndani ya shimo hamna mwangaza. Hivyo basi, wahusika Ame na Zidi huzunguka duara lao ovyo ovyo kama vipofu. Hii ni hali duni ya maisha kuashiria mateso na utupu wa binadamu ulimwenguni.

#### 4.8 HITIMISHO

Sura hii sawa na ya tatu imemulika vipengele muhimu hasa vya kifani ambavyo hufanya tamthilia ya *Amezidi* kuwa na mwelekeo wa kiubwege. Aidha tumebainisha kuwa tamthilia ya *Amezidi* inaweza kufananishwa na tamthilia za ubwege za Kimagharibi mfano *Waiting for Godot* yake Samuel Beckett na *The Lesson* yake Eugene Ionesco.

*Amezidi* inawakilisha ubwege wa Kiafrika na kwa kiasi inatofautiana na tamthilia zingine za ubwege. Ingawa wahusika wake wanakatisha tamaa wanasawiri chembechembe za matumaini.



## TANBIHI

---

- <sup>1</sup> Taz. Kezilahabi, E. (1974) *Kichwamaji*.  
East Africa Publishing House. Nairobi.  
Uk. 101-102.
- <sup>2</sup> Mhusika Mkuu Katika *Kichwamaji*  
Kama Namba Moja Hapo Juu
- <sup>3</sup> Sartre Jean-Paul (1985) *Reporieve*.  
Penguin Books, England.  
Utangulizi.
- <sup>4</sup> Wafula, R. M. (1999) *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake*.  
Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi  
Uk. 76
- <sup>5</sup> Taz. Sigmund Freud (1961) *The Future of an Illusion*.  
W. W. Norton and Co. Ltd. New York.  
Uk. 102
- <sup>6</sup> Taz. Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji Wa Fasihi: Nadharia na Mbimu*.  
Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi.  
Uk. 76

## 5.0 SURA YA TANO

### 5.1 UTANGULIZI

Katika sura hii tunatazama jinsi mwandishi wa *Amezidi* amelishughulikia suala la maisha. Tutachunguza na kupima mawazo ya Mohamed ili kubainisha jinsi alivyoathiriwa na tapo la ubwege.

Maana ya maisha ni suala la kimsingi katika tapo la ubwege. Kiudhanaishi, maisha ya binadamu ulimwenguni hayana maana. Ulimwengu anamoishi binadamu ni katili na humtesa bila huruma. Greene<sup>1</sup>, anaeleza kuwa kuteseka na kuhisi maumivu kwa binadamu ni hali ambayo haiwezi kuepukika ulimwenguni. Binadamu ni sharti ayaishi maisha jinsi yalivyo bila kuyakwepa. Binadamu hujikuta katika hali fulani na ingawa hakuchagua hali hiyo, analazimika kushikamana nayo kwa vile hana uwezo wa kutengana nayo.

Waandishi kadhaa wa tapo hili wamelishughulikia suala hili la maisha kupitia kazi zao. Kezilahabi amedhihirisha kuwa maisha ni fujo na hayana thamani yoyote kwa mwanadamu. Beckett, Ionesco na Genet, wamejaribu kubainisha kuwa maisha ni maumivu ya kusubiri kifo. Mawazo haya juu ya maisha yanakatisha tamaa, chambilecho Kierkegaard<sup>2</sup> anaposema kuwa:

Ni vigumu kutohisi kuwa hali ya kukata  
tamaa inaweza pia kuchaguliwa kama  
njia rahisi ya kuishi; ikiwa kila kitu hakina  
maana, hatuna haja ya kujisumbua;  
tunaweza kuafikiana na hali hiyo...  
Udhanaishi unatokana na kukata tamaa.  
(Tafsiri yetu)

## 5.2 MAANA YA MAISHA

Kiudhanaishi, maisha ni hatua ya kuelekea kifo. Binadamu pamoja na vitu vyote vilivyomo ulimwenguni vinazungukwa na ubwege, utupu. Vitu huzaliwa bila mpango wala sababu. Aidha, vitu hivyo vinajidunisha vyenyewe kwa unyonge, na hufa kwa unasibu tu.

Katika kuvitalii vina vya sababu na umuhimu wa kuwepo kwa binadamu ulimwenguni, udhanaishi unatuonyesha dhahiri ombwe lenye giza totoro ambalo huwakilisha uduni na unyonge wa binadamu ulimwenguni. Kile ambacho ni bayana, ni binadamu kukaa tu huku akisubiri kifo. Inabainika pia kuwa, binadamu hana uwezo wa kuchagua matendo yake, ila kufanikisha majaaliwa yake. Matumaini ya maisha mema siku zijazo ni maliwazo tu kwa binadamu. Sartre (1985:157)<sup>3</sup> anasema:

Sisi ni viumbe tuliofungamanishwa  
kwa ulimwengu – na hicho ndicho  
kitovu cha matatizo yetu yote.  
(Tafsiri yetu)

Njogu na Chimerah (1999:75) wanaeleza kuwa ubwege ni maumivu ya kifalsafa kuhusu maisha ya binadamu yasiyokuwa na mwelekeo na yaliyotamauka. Hii ndiyo tasnifu ya maisha kufuatana na maandishi ya kibwege. Kwa wahusika wa kiubwege, maisha ni ruiya tu. Wahusika hawa hujiepusha na kutenda, na badala yake huketi tu na kuzungumza. Hii ni sanaa ya kupotea kwa nafsia, na kwao wokovu haujibainishi. Wahusika hawa hawatendi la maana kwa sababu wokovu ni jambo linalowazidi uwezo. Kwao, maisha ni kama ndoto, ni kama mazigazi ndiposa Ame katika *Amezidi*, anasema:

... tunafurahi ... na mbele yetu mazigazi ...  
mazigazi ... mazigazi ... nini basi  
kama si ndoto ya kujidanganya tu?  
(uk. 83)

Inabainika kuwa, kinyume na tamthilia nyingi za kibwege, tamthilia ya *Amezidi* huendeleza suala la matumaini katika maisha; yaani haikatishi tamaa. Japo wahusika wake hawaonyeshi matumaini makubwa ya hali yao kuboreka, mwandihsi anaonekana kuamini kwamba hali hizo zinaweza kubadilika binadamu mwenyewe akijitolea muhanga. Hali hii inathibitika kwa mfano kupitia Wimbo wa Mzee, dondoo kutoka *Kilio cha Haki*, na Wimbo wa Mtoto Asiyezaliwa.

Katika kianzio, tunamwona mzee akiathirika kutokana na hali aliyo nayo. Anamuaga mwenziwe aliyetangulia kuondoka duniani. Mzee anachungulia kaburi na hali anayoiacha nyuma haimfurahishi. Matumaini ya mema kupatikana baadaye ni hafifu ndiposa asema:

Siku zangu zimefika na kwangu si hasara  
kwani kuna hawa, hawa waliozaliwa  
wal'oandaliwa mazingira ya uvivu na balaa  
Hawa watakula kelele 'talala juu ya kelele  
wataoza kwa kelele  
wimbi la maneno na kelele  
wimbi la maangamizo, kelele!  
(uk. 1)

Kwa mujibu wa mzee huyu, kupiga domo tu ndiko kutakaoliangamiza bara la Afrika. Viongozi wa kizazi kipya hawampi mzee matumaini yenye uhakika kwa vile ni zogo la viongozi ambao uhusiano wao si mzuri. Hata hivyo, kwa mbali, mzee anahisi miale ya mema katika kifo. Kifo chake kitamletea usahaulivu na kwake hakitakuwa hasara bali baraka. Ni kifo ambacho kitaleta mwanzo mpya. Freeman (1971:5) anatetea kifo cha aina hii anaposema kuwa:

Kifo kinaweza kuleta maana katika  
maisha katili na yasiyo na maana (Tafsiri yetu)

Hali hii ya kifo kuleta maana maishani mwa binadamu hubainika katika tapo la kiubwege. Katika *Amezidi*, tunampata Zidi akigundua ukweli juu ya uhusiano wao na EC kupitia tisho la kifo. Wanagundua kuwa matatizo yao pamoja na vifo vyao vimechochewa na misaada waliyopata. Wanasemezana:

Ame: Kufa raha?

Zidi: Ndiyo, kufa ni raha; si ndiyo  
maana sisi tumekuwa tukikutafuta  
siku zote hizi? Tulikuwa tukikuhimiza  
kuje haraka haraka!

Ame: Hapana, usife! (anamsogelea na kumkumbatia).

Zidi: Usinikumbatie...usiniguse...usisahau kwamba  
nina kipindupindu mimi...

Ame: Haidhuru!

Zidi: Kwaheri basi, Ame! (uk. 79)

Zidi amegundua uovu wa EC na Mzungu, ndiposa anamwambia Ame hasimkumbatie, yaani aachane na EC kwa vile EC haina chochote cha maana kwa Mwafrika ila maangamizo. Hali hii inaumana na imani ya kidhanaishi kuwa binadamu amekuwa akiutafuta ukweli juu ya maisha yake bila mafanikio. Ukweli upo lakini kwa vile binadamu amefumba macho yake hauoni. Warnock (1970:78) anasema:

Ukweli upo kwa sisi sote, lakini  
ni wajibu wa kila mmoja wetu  
kuutafuta na kuupata. (Tafsiri yetu)

Maisha ya Mwafrika kwa miaka mingi yamekuwa yakielekea kuzimu bila ya Mwafrika mwenyewe kutambua. Kejeli ni kwamba Mwafrika pia ameshiriki katika njama ya kulinyonya bara la Afrika.. Baada ya kifo cha Zidi, Ame anaanza kujielewa. Mwandishi anatilia shaka mielekeo ya nchi za Kiafrika. Ndoto za Waafrika zinafichuliwa wakati Ame anakumbana na sauti ya Zidi.Sauti inaelezea bara la Afrika kuwa kuzimu.Ame anagundua ukweli kuhusu nchi yake. Ukweli unaonata.ni kama

kuota ndoto ukaelekea kiza. Ni kama kugeuka nyuma na kuelekea mbele iwapo kote kuna kiza.

Kuishi kuzimu ni sawa na kifo. Maisha yanayozungukwa na kiza pande zote yanachukiza. Afrika ni sharti ifuate mikakati inayofaa ili kutia misingi imara ya maendeleo na maisha bora. Watu wa nchi ya Amezidi wamekuwa wakijidanganya kwa muda mrefu, maisha yao ni ya kindoto, ya kiubwege.

Kifo cha Zidi (uk. 84) ni kifo ambacho mtunzi amekitumia kutoa fundisho kwa jamii. Anaelekea kutuambia kuwa kifo cha kimwili cha watu waliofungwa kwa minyororo ya ukoloni, na ukoloni mamboleo, ni upeo wa juu wa kifo cha polepole cha kiroho na kisaikolojia. Suala hili huashiria maisha ya Waafrika katika vipindi vyote vya utawala; kabla ya ukoloni, kipindi cha ukoloni, na uhuru. Inabainika kuwa, hakuna la maana ambalo bara la Afrika limepata. Tunaambiwa:

Mbali kule tunatoka... na mbali kule  
tunakokwenda... Na sasa kiza mbele!  
Tumetoka huko au pengine hatujatoka...  
Pengine tumesimama pale pale,  
tokea siku ile; au tumepiga hatua nyuma  
pasi na kujua, pasi na kutambua...  
Na sasa kiza! Kiza kushoto; kiza kulia...  
kiza nyuma... kiza mbele... tumeshatoka  
huko au hatujatoka? Nawauliza 'sa!  
(kwa hadhira) Tumefika tunakokwenda?  
(uk. 82).

Ame naye anakufa kutokana na hali na mazingira sawa na yale yaliyosababisha kifo cha Zidi. Vifo vya Ame na Zidi vinalingana na kuendeleza ubwege wao. Kuhusu vifo hivi, Wafula (1999:75) anaeleza kwamba kwa mujibu wa tamthilia ya *Amezidi*, vifo vya

nguli visiwe visingizio vya kukata tamaa. Waafrika wanapaswa kutua na kujisaili. Vifo hivyo vinapasa kuanzisha tarehe mpya katika maisha ya wakazi wa Amezidi, yaani Waafrika.

Labda hii ndiyo sababu Mohamed akahitimisha tamthilia yake kwa usemi ufuatao:

“Tumevinjari Afrika,  
Tumesimama nguvu moja  
kuzibeba nafsi zetu wenyewe  
kwa hatima yetu wenyewe  
Nzito ingawaje, nafsi zetu  
tutazibeba!  
Chafu ingawaje,  
tutazisafisha!  
Tutaisafisha hata heshima yetu iliyochafuka  
Tutaibeba mizigo yetu,  
Sasa isiyobebeka!” (uk. 87)

Kifungu hiki kinatoa chembechembe za matumaini, ingawa kuanzia mwanzo, tamthilia hii kwa ujumla inakatisha tamaa.

Maisha ya Ame na Zidi ni ya taabu kwa vile wamekwama katika umaskini uliokithiri. Hali hii huwafanya wahitaji wa misaada- misaada ambayo inawabomoa zaidi. Utegemeaji huu wa misaada katika jamii unaungwa mkono na Marx (1963:81) anaposema:

... ili wajikimu kwa mahitaji yao,  
wasionacho hulazimika kutoa huduma  
kwa wenye nacho hivyo basi  
kuwategemea kimaisha.  
(Tafsiri yetu)

Nchi ya Amezidi, ina ukwasi mwingi wa malighafi. Ingawa hivyo, wakazi wake hawafanyi lolote la maana kutumia rasilmali zao kuboresha maisha yao. Ame na Zidi ni wazembe na wafisadi. Vitendo vyao ni vya kiubwege kwa vile vinaenda kinyume na matarajio ya kihalisia. Nchi za Kiafrika zilipata uhuru ili ziweze kujizatiti na kuleta maendeleo na usawa kwa wote.

Mahitaji ya nchi za Kiafrika yalimsukuma Nyerere (1967:1) kusema kuwa, kusiwe na kiongozi wa chama au serikali ambaye anahusika na vitendo vya ubepari na umwinyi. Viongozi kwa maoni yake, hawaruhusiwi kujilimbikizia mali na kujitajirisha haraka haraka kwa kutumia madaraka yao. Madaraka wanayopewa viongozi ni ya kuwasaidia wawatumikie vyema umma na wala sio wawe mabwana wakubwa wa kuwanyonya wanyonge.

Viongozi tunaopata katika Amezidi ni wenye ubinafsi wa maisha. Wanajijali zaidi huku wakipuuza matakwa ya nchi yao. Ame na Zidi maisha yao ni kuzembea kazi na kutumia vibaya rasilmali za nchi yao. Katika onyesho la sita wanashiriki katika ufidadi wa hali ya juu wakiwa mkaguzi na mkaguliwa ofisini. Wanasemezana hivi:

Zidi: Unafikiri nini?

Ame: Nafikiri...

Zidi: Kuhusu nusu bin nusu?

Ame: Kuhusu nitaipata wapi nusu bin nusu?

Zidi: Kwa nini?

Ame: Nimeshaitafuna yote, milioni nzima!

Zidi: Aaa, hiyo rahisi! Chukua....chota  
nyingine unipe....

Ame: Kisha?

Zidi: Tutachoma nyaraka.

(uk. 51)



Haya ni maisha ya kukatisha tamaa kwa umma. Ni maisha ambayo hayatoi matumaini kwa watu wapenda maendeleo, na ambao wanataka kuboresha nchi yao maskini. Ame na Zidi wanategemea misaada badala ya kutumia malighafi yao kujitegemea. Misaada wanayopewa haifai na hata hawajui kama wataendelea kupatiwa. Haya ni maisha mithili ya ajali asemapo Greene (1960:7):

Binadamu ni ajali, hali yake haina  
utaratibu na muhimu zaidi ulimwengu  
umeumbwa kwa hali ya usahaulifu.  
(Tafsiri yetu)

Katika onyesho la tisa, Ame na Zidi wanapanga sherehe ya kusherehekea siku ya kuzaliwa kwao. Wanatumia pesa nyingi za umma kukumbuka siku ya uhuru wao, siku ambayo hawaelewi umuhimu wake (uk. 75). Wanatumia shilingi milioni arobaini na kualika wageni wengi. Tunaambiwa:

Ame: Lakini sherehe ya shilingi milioni arobaini  
na kualika wageni wapatao laki nne itakuwa  
sherehe kubwa kwa siku ya kuzaliwa tu...  
Zidi: Wewe namna gani bwana, siku ya kuzaliwa  
unaiona ndogo...? Watu waliitungia mashairi  
na nyimbo...  
(uk. 74)

Ruhumbika (1983:1) anapinga hali hii ya viongozi kuchukua muda mrefu kupanga sherehe kubwa na zisizokuwa na manufaa. Kwake, huo ni utumiaji mbaya wa pesa au mali ya nchi. Kejeli ni kwamba, Ame na Zidi wanasherehekea siku ya uhuru wao, na bado wanaendelea kuwategemea wahisani kwa misaada. Huu si uhuru kamwe, bali ni utumwa au uhuru wa bendera tu na ambao haupaswi kuandaliwa sherehe kubwa namna hiyo.

Kiudhanaishi, maisha ya binadamu husawiriwa kama fujo. Hali hii hubainika kupitia shughuli mbalimbali za binadamu ambazo hazidhihirishi utaratibu wowote. Matendo ya binadamu maishani ni shaghalabaghala kwa vile kila mtu hutenda atakavyo na hashurutishwi na yeyote, si hata Mungu, kutenda atendavyo au kusema asemavyo. Hali hii hubainika katika *Amezidi* tunapowapata wahusika wakitenda watakavyo mfano kutoenda kazi, kutegemea misaada, kuiba mali ya umma na kulala; na kusema wayapendayo mfano kuliita pango lao kasri na kulipamba kwa utajiri mwingi wa kindoto.

Aidha, katika onyesho la nne, tunapatiwa mandhari ya darasani, ambayo huendeleza wazo la maisha kama fujo. Wanafunzi ni zogo, mwalimu ni kibonzo asiyelewa kazi yake na amekiuka kaida za ualimu; sauti ya redio inasikika katikati ya kipindi na kuna kucheka na kulia darasani na kadhalika. Kweli haya ni mazingira yasiyopendeza na yanayoendeleza hali ya maisha kama fujo.

Waandishi kadhaa wameshughulikia wazo hili la maisha kama fujo. Kezilahabi katika *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975:92), amesawiri dunia kama uwanja wa fujo. Inabainishwa kwamba, kila mwanadamu ameumbwa kufanya fujo zake halafu ajiondokee ulimwenguni. Uzito wa fujo hutofautiana kwa vile kuna watu ambao hufanya fujo zaidi ya wengine. Maisha hayana lolote la maana ila kufanya fujo huku ukingojea kifo.

Uhusiano kati ya kifo na maisha ni suala la kimsingi katika tapo la kiubwege. Kiudhanaishi maisha ni kufa pole pole. na kifo si jambo la kumshughulisha binadamu kwa vile ndicho hatua ya mwisho anayoisubiri. Baada ya kuishi kiubwege, Ame na Zidi wanakufa, kifo cha maumivu na raha.

Wazo la chanzo cha maisha ya binadamu na kifo limemsumbua na kumpumbaza binadamu kwa muda mrefu. Binadamu ametumia wakati wake mwingi kufikiria juu ya suala hili bila kupata ukweli. Maisha ya binadamu ni mithili ya kitendawili chepesi, lakini kwa vile binadamu ameamua kutofikiria, ameshindwa kukitegua. Kuhusu hali hii, Ignace Lepp<sup>4</sup>, anasema:

Badala ya kufikiria kifo kama mwisho  
wa maisha, napendekeza tukitazame kama  
kitendo cha mwisho katika kutimiliza maisha  
ya muda. Basi itafuatia kwamba, tukifaulu  
katika kuyapa maisha yetu maana, vivyo hivyo  
kifo kitakuwa na maana. (Tafsiri yetu)

Katika tamthilia ya *Amezidi*, wahusika Ame na Zidi wanakufa huku wakicheka. Kifo chao kimegubikwa katika furaha. Zidi anapokaribia kufa analia:

Aaaaa... ma... mau... mau... mivu...  
maumivu... aaa, tumbo. Aaaaa, nyama  
mbovu... EC... EC... EC... kifo... kifo...  
Aaaaa, raha... raha... raha, ah, raha, ya  
kifo... hata kufa kunanipa raha, Ame!  
Ni... niku... nikumbuke... Mari... Mari...  
yuko wapi?... Mari...  
(*Zidi anakufa*) (uk. 80)

Naye Ame anapoelekea katika kifo chake anatuambia:

Jamani raha... kuzimu kule nakuona... Zidi yuleeeee...  
Zidi aaaaa, sasa maumivu yanazidi, aaaaaaa sasa  
raha inazidi. Raha ya maumivu na maumivu ya raha.  
Je, (*anaigeukia hadhira*) na nyinyi mnataka mwende  
nasi katika maumivu haya ya raha? Fanyeni  
basi au bora niseme msifanye kitu basi! Ah, nakufa  
jamani. Kifo cha raha! Naku... na... naku... naku...  
fa... NAKUFA! (*Ame anakufa*)  
(uk. 85)

Mwandishi anamithilisha maisha ya binadamu na vurumai zake. Maisha ya binadamu na kifo chake ni sawa. Tofauti kati ya kifo na maisha ni nyembamba mno chambilecho Beckett<sup>5</sup> anapodai kuwa maisha ni kuendelea kufa, mfanyiko ambao unaendelea mpaka kiwango kitakiwacho, kifo cha hakika.

Hali ya kifo chenye raha pia inabainika katika novela ya Kezilahabi itwayo *Nagona*. Katika uk. 62, tunapata wazo la kejeli kuhusu maisha. Mwandishi anatumfahamisha juu ya watu ambao walikufa huku wakicheka na kushangilia.

Ni dhahiri kuwa Mohamed amelipatia wazo hili la kifo nafasi kubwa katika tamthilia ya *Amezidi*. Licha ya vifo vya Zidi na Ame, tunaambiwa juu ya Mzee anayekaribia kufa na kumfuata mwenzake aliyetangulia (uk. 1). Pia tunaambiwa juu ya watu wengi, na kijiji kizima ambacho kiliteketea (uk. 79, 85). Katika onyesho la tisa, tunapata vifo zaidi:

Zidi: Lakini ada ya maji tunalipa...

Ame: Hiyo si hoja.

Zidi: Japo kwa majirani kaniombee.

Ame: Hakuna jirani aliyebaki,

tumbaki mimi na wewe;

wengine wote wameshatangulia...

Wameshakwenda... wamefyekwa na

ukame na msaada na EC.

(uk. 76)

Kwa ujumla, maisha ya binadamu ulimwenguni yamejaa utata, ni yenye ugumu na uvundo. Waandishi wa kiubwege sawa na wa kiudhanaishi, wanakubaliana kuwa, hakuna furaha katika maisha. Maisha ni mateso, ni adhabu. Kezilahabi anayaona maisha ya binadamu kama tambara bovu. Maoni haya yana mashiko na yamo katika kazi zake mfano katika *Kichomi* ambapo anasema:

Ni adhabu ya kutosha kupaswa  
kuishi juu ya sahani yenye joto  
kali, ya kukaangia. Na yaliyopita,  
yamepita.  
(uk. 7)

Kwake, sawa na Mohamed kupitia *Amezidi*, maisha ni mchezo, ni mzaha. Hali ya kindoto inayotawala tamthilia hii ya *Amezidi* ni sababu mojawapo muhimu ambayo humtambulisha Said Ahmed Mohamed kama mwandishi asiyeamini sana juu ya uhalisia. Wahusika wake, Ame na Zidi, wanaishi katika dunia ya kufikirika, ya kidhahania. Armeathiriwa na maandishi ya kidhanaishi. Kezilahabi katika *Mzingile* anatupatia usemi wa mzee:

Maisha yenyewe ni mzaha mkubwa  
kuliko yote. Ndiyo maana yanaweza  
kuishika.  
(uk. 13)

Maisha ya binadamu ulimwenguni ni fujo na hayana maana wala furaha. Kauli ya Camus<sup>6</sup> kuwa furaha ya kudumu haiwezi kupatikana katika maisha ya binadamu na kuwa maisha yake ni ya huzuni tupu, husisitiza hali hii.

### 5.3 HITIMISHO

Tumebainisha mtazamo wa maisha katika tamthilia ya *Amezidi* na kudhihirisha mawazo ya mwandishi na yale ya waandishi wengine wa tapo la ubwege na udhanaishi kwa ujumla.

Hali ya maisha kukosa maana inasawiriwa vyema katika kazi za Beckett na Ionesco. Katika *Waiting for Godot*, kwa mfano, Gogo na Didi (Vladimir na Estragon) wanajaribu mara mbili kujiua bila mafanikio. Hata hivyo, hawakati tamaa ya kutekeleza lengo lao siku moja. Beckett pia anatumia majina mengi kutambulisha wahusika wake. Vladimir na Estragon tunaambiwa kuwa ndio tena Gogo na Didi. Hali ya kubadilisha majina ya wahusika inadhihirika pia katika *Amezidi* ambapo Ame na

Zidi hubadilisha nafsi zao katika jamii. Kwa mfano wanakuwa mwalimu na mwanafunzi; Bosi na msaidizi wake; na mkaguzi na mkaguliwa.

Kimaisha, tabia hii huonyesha hali ya tamaa na kutotosheka kwa mwanadamu. Binadamu hana furaha, na mara kwa mara hujaribu kutafuta njia ya kujipatia maisha bora. Juhudi zake hata hivyo, huishia ukingoni kwa vile hana uwezo wa kuleta mabadiliko ya maana maishani mwake. Hii ndiyo sababu, Ame na Zidi, ingawa wanajaribu kuwa hivi na vile, hawafaulu kuboresha hali ya maisha yao. Ni kejeli kuwa, hata baada ya kusawiriwa kama Bosi na msaidizi wake, na halafu kuiba pesa nyingi, maisha yao bado ni ya kiubwege. Binadamu hana mwelekeo ulimwenguni. Muhimu kwake ni kuzunguka duara lake duni bila matumaini ya kuona mbele. Foulquie (1947:56) anafafanua hali hii anaposema:

Binadamu anaendesha maisha yake  
katika giza totoro la usiku kwenye  
barabara yenye mabonde. Mwingine  
anaweza kudai kuwa anaweza kungoja  
hadi wakati wa mchana, lakini ukweli  
ni kwamba hawezi, kwa vile mchana huo  
hautafika.

(Tafsiri yetu)

Hali hii hukatisha tamaa na ni dhihirisho kuwa maisha si kitu cha maana, ni usumbufu.

## TANBIHI

- 
- <sup>1</sup> Taz. Greene, N. N. (1960) *Jean-Paul Sartre: The Existentialist Ethic.*  
The University of Michigan Press,  
U.S.A. uk. 9-10.
- <sup>2</sup> Taz. Roubiczek, P. (1964) *Existentialism for and Against.*  
Cambridge University Press,  
London. uk. 113.
- <sup>3</sup> Mhusika mkuu, Mathiew katika *Iron in the Soul.*  
Penguin Books, England.  
uk. 157.
- <sup>4</sup> Taz. Lepp, I. (1968) *Death and Its Mysteries.*  
Burns and Dates. London.  
uk. 139.
- <sup>5</sup> Taz. Mueller, R. W. (1964) *The Testament of Samwel Beckett.*  
Faber and Faber, London.  
uk. 110.
- <sup>6</sup> Cruickshank, J. (1958) *Albert Camus: The Literature of Revolt.*  
Oxford University Press, London. uk. 27.

## 6.0 SURA YA SITA

### HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 6.1 HITIMISHO

Katika tasnifu hii tumeshughulikia tamthilia ya *Amezidi* kama kazi ya kiubwege. Tumehakiki tamthilia hii kwa upande wa maudhui na fani na kubainisha jinsi Said Ahmed Mohamed alivyoathiriwa na tapo la ubwege.

Katika sura ya pili tumetalii historia na tanzu za drama. Tumeona kuwa tamthilia sawa na tanzu zingine za fasihi andishi ina asili yake katika fasihi simulizi. Aidha, tumeonyesha kuwa, drama inaweza kugawanywa katika tanzu mbalimbali zikiwemo futuhi, tanzia, drama ya kiubwege, melodrama, kichekesho, tamthilia tatizo na mchezo adilifu. Maendeleo ya jamii huathiri fasihi na tunatambua kuwa mabadiliko hayo yatasababisha kuwoko kwa tanzu nyingi zaidi ya zile ambazo tumeshughulikia.

Katika sura ya tatu na ya nne tumeyachungua maswala muhimu ambayo tamthilia ya *Amezidi* inayashughulikia na kujadili jinsi ambavyo imeathiriwa na tapo la ubwege. Tumeona jinsi Mohamed anavyotazama mazingira ya binadamu ulimwenguni. Kupitia wahusika wake, anaonyesha mateso yanayomkabili binadamu katika mazingira yake machafu na ya kukatisha tamaa. Aidha, tumeona msimamo wa mwandishi kuwa lugha na mawasiliano ya binadamu yamekufa. Ameonyesha juhudi za binadamu kuwasiliana kupitia nyimbo, elimu, vicheko na vilio pamoja na sauti bila mafanikio. Kushindwa kutumia lugha ni dhihirisho la ugumu wa maisha yake.

Waaidha tumeona jinsi ambavyo mwandishi amelishughulikia suala la Mungu. Kinyume na tamthilia za kiubwege, Mohamed amemtambua Mungu katika tamthilia ya *Amezidi*. Tumesisitiza kwamba kuwoko kwa Mungu hutiliwa mashaka katika tapo la ubwege. Waandishi katika tapo hili wakiwemo Beckett na Ionesco wameonyesha kwamba Mungu hana lolote la maana kwa binadamu, na binadamu hana shuruti yoyote kumtegemea.



Mohamed anakiuka mwelekeo huu kwa kuwapa wahusika wake wazo la wokovu kutoka kwa Mungu.

Katika sura ya tano tumejadili maana ya maisha kama ambavyo imejibainisha katika tamthilia hii. Tumeonyesha jinsi mwandishi alivyoathiriwa na waandishi wakongwe wa tapo la ubwege na hivyo kuyaona maisha ya binadamu kama usumbufu usio na maana yoyote kwake

Sawa na Beckett na Ionesco, Mohamed amebainisha kwamba maisha ni duara, ni mzunguko. Amepuuza suala la ploti na badala yake kusawiri wahusika ambao hawatendi lolote la maana ila kuzunguka kwenye pango duni lililojaa matatizo.

Aidha, tumeyajadili maswala ya kufikiri na ukweli. Kiubwege, ukweli na kufikiri ni mambo ambayo yamemshughulisha binadamu kwa muda mrefu. Friedrich Nietzsche<sup>1</sup> alisisitiza kuwa binadamu ni sharti ajizatiti katika tendo la kufikiri ili aweze kujielewa. Hata hivyo binadamu hana uwezo huo ndiposa ameshindwa kutambua ukweli kuhusu maisha yake.

Ukweli kuhusu maisha ya binadamu upo lakini umemkwepa binadamu kokote kule anakoutafuta. Warnock (1970:78) anaeleza kuwa ukweli upo kwa kila mtu na ni wajibu wetu kuutafuta. Katika *Amezidi*, ukweli unapatikana katika kifo. Kifo cha Zidi kinamfanya Ame kugundua ukweli juu ya uhusiano wao na EC.

Katika kushughulikia maisha, mwandishi pia ameonyesha kuwa tofauti kati ya maisha na kifo ni nyembamba mno. Tumeonyesha jinsi alivyoshughulikia suala la kifo kwa kulipatia nafasi kubwa katika *Amezidi*. Hivyo basi Mohamed anashangilia kifo sawa na waandishi wa tapo la ubwege.

*Amezidi* kwa ujumla ni tamthilia inayokatisha tamaa. Wafula (1999:69) anaeleza kuwa mwito wa kutokata tamaa haupatikani katika tamthilia ya *Amezidi*. Inabainika kuwa, mwandishi amekasirikia ashabu wote wanaoishi barani Afrika. Ingawa kimalizio cha tamthilia hii – “Wimbo wa Mtoto Asiyezaliwa” kinatuarifu kwamba

kuna matumaini ya kuzaliwa upya kwa Mwafrika na hivyo kujiingiza kwenye mkondo wa maendeleo, hakuna uhakika wa kutimia kwa tumaini hili katika mtiririko wa tamthilia. Jamaa tunaokumbana nao ni vinyago, ni vikaragosi ambavyo daima vimeshindwa kuumiliki ulimwengu wao.

Binadamu ambaye hushindwa kuumiliki ulimwengu wake ni wa kiudhanaishi. *Amezidi* ni kazi ya fasihi iliyojaribu kuzingatia ubwege lakini haikufanikiwa sana kama kazi za waandishi wa kibwege wa Kimagharibi. Mohamed ameshughulikia vipengele vya ubwege, na pia vya uyakunifu – ni tamthilia mseto, na ambayo ni mfano wa ubwege wa bara la Afrika.

## 6.2 MAPENDEKEZO

Tunapendekeza kuwa watafiti waifanyie utafiti zaidi tamthilia hii kwa kutumia nadharia nyingine, kama vile umuundo.

Aidha, tunatoa rai kwa wahakiki kufanya utafiti wa kiulinganishi wa *Amezidi* na tamthilia nyingine katika tapo hili ili kubainisha zaidi ufanisi wake.

Kutokana na mipaka na muda uliokuwepo wa kuandika tasnifu hii tumejibana zaidi katika vipengele muhimu ambavyo mwandishi alitumia kupitisha mawazo yake. Hivyo basi hatujashughulikia vipengele vyote vya usanifu wa tamthilia. Tunapendekeza basi tamthilia hii ifanyiwe utafiti zaidi hasa katika upande wa fani.

## TANBIHI

---

<sup>1</sup> Taz. William, H. na Levey, J. S (Wahariri) (1975) *The New Columbia Encyclopaedia* Columbia University Press, New York.  
Uk. 256

## MAREJELEO

- Alembi, E. (2000) Appreciating Drama  
Acacia Stantex Publishers, Nairobi.
- Alvarez, A. (1971) The Savage God: A Study of Suicide  
Penguin, England.
- Anderson, M. J. (1965) Classical Drama and its Influence  
Methuen, London.
- Anderson, K. E. (1972) Introduction to Communication Theory  
and Practice. Methuen, London.
- Arege, T. I. M. (1998) Ushairi Huru wa Kiswahili: Mchango wa Euphrase  
Kezilahabi  
Tasnifu ya M.A Haijachapishwa
- Aristotle (1934) The Poetics  
J. M. Dent & Sons Ltd., New York.
- Aylen, A. K. (1976) Wema Hawajazaliwa  
Heinemann Educational Books,  
Nairobi
- Aylen, L. (1964) Greek Tragedy in the Modern World  
Methuen, London.
- Beckett, S. (1955) Waiting for Godot  
Faber and Faber, London.
- \_\_\_\_\_ (1958) End Game Faber and Faber, London.

- Bertoncini, E. Z. (1959) Outline of Swahili Literature: Prose, Fiction and Drama.  
Leiden, E. J. Brill. UK.
- Brecht, B. (1964) Brecht on Theatre  
Shenval Press, London.
- Camus, A. (1953) The Rebel  
Hamish Hamilton, London.
- \_\_\_\_\_ (1984) The Myth of Sisyphus  
Penguin, London.
- Cruickshank, J. (1958) Albert Camus: The Literature of Revolt.  
Oxford University Press, London.
- \_\_\_\_\_ (1960) Albert Camus and the Literature of Revolt.  
Oxford University Press, London.
- Cuddon, J. A. (1979) A Dictionary of Literary Terms  
Andre Deustch Ltd., London.
- Encyclopedia Americana Corporation (1977)  
The Encyclopedia Americana.  
Grolier Ltd. New York.
- Esslin Martin (1974) The Theatre of the Absurd  
Methuen, London.
- Foulquie, P. (1947) Existentialism  
Dennis Dobson Ltd., London.
- Freeman, E. (1971) The Theatre of Albert Camus  
Methuen, London.

- Fugard, A. (1960) Nongogo  
Guernsey Press, London.
- \_\_\_\_\_ (1967) The Coat  
Oxford University Press, London.
- \_\_\_\_\_ (1974) The Island Channel Islands:  
Guernsey Press, London.
- \_\_\_\_\_ (1974) Sizwe Bansi is Dead  
Oxford University Press, London.
- \_\_\_\_\_ (1974) No Good Friday  
Oxford University Press, Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (1975) The Blood Knot  
Oxford University Press, Nairobi.
- Gill, R. (1985) Mastering English Literature  
Macmillan Educational Ltd.,  
London.
- Greene, N. N. (1960) Jean-Paul Sartre: The Existentialist Ethic.  
The University of Michigan Press,  
U.S.A.
- Heinemann, F. H. (1958) Existentialism and the Modern Predicament  
Harper & Brothers Publishers, New York.
- Hoffman and Johnston (1987) Literature: Art and Artifact  
Harcourt Brace Jovnovch, London.

- Holman, C. (1972) A Handbook to Literature  
The Bobbs Merrill Company, New York.
- Hornby, A. S. (1989) Oxford Advanced Learners Dictionary  
Oxford University Press, New York.
- Hough, G. (1962) An Essay on Criticism  
Gerald Duckworth and Co. Ltd., London.
- Hussein, E. (1969) Kinjeketile  
Oxford University Press, Da- es-Salaam.
- \_\_\_\_\_ (1971) Mashetatni  
Oxford University Press, Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (1983) "Hatua Mbali Mbali za Kubuni na  
Kutunga Tamthilia Kufuatana na Misingi  
ya Ki-Aristotle" Katika Fasihi III  
Makala za Semina, Dar-es-Salaam.
- International Bible Society (1973) Holy Bible  
New International Version. New York
- Irungu, C. M. (1999) Dhana ya Maisha Katika Novela Mbili  
za Euphrase Kezilahabi: Nagona na Mzingile.  
Tasnifu ya M.A. Hajjchapishwa.
- Ionesco, E. (1962) The Chairs  
Reading: Cox and Wyman Ltd., London.
- \_\_\_\_\_ (1962) Rhinoceros  
Reading: Cox and Wyman Ltd. London.

- \_\_\_\_\_ (1962) The Lesson  
Reading: Cox and Wyman Ltd., London.
- Katalambulla, F. H. (1976) Mirathi  
East African Literature Bureau, Nairobi.
- Kaufmann, W. (1956) Existentialism from Dostoevsky to Sartre.  
Meridian Books Inc. New York.
- Kezilahabi, E. (1971) Rosa Mistika  
Kenya Literature Bureau, Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (1974) Kichwamaji  
East African Publishing House.  
Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (1974) Kichomi  
Heinemann Educational Books  
(E.A) Ltd., Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (1981) Dunia Uwania wa Fujo  
East African Publications Ltd.  
Arusha.
- \_\_\_\_\_ (1990) Nagona  
Dar-es-Salaam University Press  
Dar-es-Salaam.
- \_\_\_\_\_ (1991) Mzingile  
Dar-es-Salaam University Press  
Dar-es-Salaam.

- Killam, C. D. (Mhariri) (1973) African Writers on African Writing  
Heinemann, London.
- King'ei, K. (1997) Mwongozo wa Amezidi  
East African Educational Publishers, Nairobi.
- Kitchin, L. (1966) Drama in the Sixties  
Faber & Faber Ltd. Nairobi.
- Kiteki, B. N. (1998) Fani Katika Tamthilia za  
Emmanuel Mbogo: Uhakiki  
wa Ploti na Usawiri wa Wahusika.  
Tasnifu ya M.A. Haijachapishwa.
- Laing, R. D. (1960) The Divided Self  
Penguin, England.
- Lepp, I (1968) Death and its Mysteries  
Burns and Oates. London.
- Lewis, A. (1962) The Contemporary Theatre  
Crown Publishers, Inc.  
New York.
- Macquarrie, J. (1972) Existentialism  
World Publishing Co.  
New York.
- Maneno, S. K. (1997) Mwongozo wa Amezidi  
Oxford University Press, Nairobi.
- Marx, K. (1959) Capital  
Random House, New York.



- \_\_\_\_\_ (1963) Early Writings  
C. A. Watts & Co. Ltd., London.
- Masoko na Mdee (1984) MULIKA NA 16. Chuo  
Kikuu cha Dar-es-Salaam – TUKI,  
Dar-es-Salaam.
- Mbatiah, M. (1997) ‘Mienendo Mipya Katika  
Uandishi wa Kezilahabi’.  
Makala haya hayajachapishwa.
- \_\_\_\_\_ (2001) Kamusi ya Fasihi  
Standard Textbooks Graphics and  
Publishing. Nairobi.
- Miller, J. (1992) The Heath Introduction to Drama  
D.C Heath and Company, Toronto.
- Mlama, P. O. (1983) “Utunzi wa Tamthilia Katika Mazingira ya  
Tanzania.” Katika Fasihi III Makala za  
Semina, Dar-es-Salaam.
- Mohamed, S. A. (1978) Asali Chungu  
Shungwaya Publishers. Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (1980) Sikate Tamaa  
Longman, Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (1980) Utengano  
Longman, Nairobi.

- \_\_\_\_\_ (1981) 'Kupatana na Riwaya Zangu'  
Makala Yaliyotolewa kwa  
Kongamano Katika Ukumbi  
wa Kenya Polytechnic.
- \_\_\_\_\_ (1984) Kina cha Maisha  
Longman, Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (1988) Pungwa  
Longman, Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (1988) Kiza Katika Nuru  
Oxford University Press, Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (1990) Kuvuli Kinaishi  
Oxford University Press, Nairobi
- \_\_\_\_\_ (1995) Amezidi  
East African Educational  
Publishers, Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (1995) Kunga za Nathari ya Kiswahili  
East African Educational  
Publishers, Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (2000) Kitumbua Kimeingia Mchanga  
Oxford University Press, Nairobi.
- Mueller, R. W. (1964) The Testament of Samwel Beckett  
Faber and Faber, London.

- Musau, P. M. (1985) Euphrase Kezilahabi:  
Mwandishi Aliyekata Tamaa.  
 Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu  
 cha Nairobi. Haijchapishwa.
- Mushi, S. (1971) Mfalme Edipode  
 Oxford University Press, Dar-es-Salaam.
- Ndalu, E. A. (1998) Mwongozo wa Amezidi  
 City Book Publishers, Nairobi.
- Ngara, E. (1990) Ideology and Form in African Poetry  
 Heinemann Kenya, Nairobi.
- Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) Ufundishaji wa Fasihi:  
Nadharia na Mbinu.  
 Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.
- Nyerere, J. K. (1967) Elimu ya Kujitegemea  
 Mpiga Chapa wa Serikali, Dar-es-Salaam.
- \_\_\_\_\_ (1967) Socialism and Rural Development  
 The Government Printer, Dar-es-Salaam.
- \_\_\_\_\_ (1968) Freedom and Socialism  
 Oxford University Press, Nairobi.
- Ongeti, K. (1984) Visiki  
 East African Educational Publishers, Nairobi.
- Onimus, J. (1970) Albert Camus and Christianity  
 Gill & Macmillan, London.

- Pasquier, A. (1950) Les Docrines Sociates en France. Paris.
- Roberts and Jacobs (1972) Literature: An Introduction to Reading and Writing.  
Printice Hall, New York.
- Rodney, W. (1982) How Europe Underdeveloped Africa  
Howard University Press, Washington D.C.
- Roubiczek, P. (1964) Existentialism for and Against  
Cambridge University Press, London.
- Ruhumbika, G. (1983) Uwike Usiwike Kutakucha  
East African Literature Bureau.  
Arusha.
- Sarara, M. M. (1997) Maudhui Katika Tamthilia za S. A. Mohamed.  
Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu Cha Nairobi  
Haijachapishwa.
- Sartre, Jean-Paul (1985) Reporieve  
Penguin Books, England.
- \_\_\_\_\_ (1985) Iron in the Soul  
Penguin Books, England.
- Serumaga, R. (1976) Maiangwa and A Play  
Heinemann, Nairobi.
- Sigmund, F. (1961) The Future of an Illusion  
W. W. Norton and Co. Ltd.  
New York.

- Soyinka, W. (1974) Masaibu ya Ndugu Jero  
Oxford University Press, Nairobi.
- Steinburgh, S. H. (1953) Cassel's Encyclopaedia of Literature. Vol. 1.  
Cassel and Co. Ltd., London.
- Styan, J. L. (1960) The Elements of Drama  
Cambridge University Press, London.
- \_\_\_\_\_ (1965) The Dramatic Experience  
Cambridge University Press, London.
- Syambo na Mazrui (1992) Uchambuzi wa Fasihi  
East African Educational  
Publishers, Nairobi.
- The University of Chicago (1968) Encyclopaedia Britanica. Vol. 8  
William Benton. Chicago.
- TUKI (1981) Kamusi ya Kiswahili Sanifu  
Oxford University Press, Nairobi.
- Vifu (1983) Aina za Tamthilia za Kiswahili  
Katika A. G. GIBBE (Mhr).  
The Spectator, No. 1.  
Educational Services Services Centre,  
Dar-es-Salaam.
- Vuzo, A. M. (1997) Mwongozo wa Amezidi  
Macmillan Kenya Ltd., Nairobi.

- Wafula, R. M. (1999) Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake  
Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.
- Wamitila, K. W. (1991) 'E. Kezilahabi: A Professor of the Absurd'  
Katika Kiswahili Juzuu 58  
Jarida la Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili. Dar-es-Salaam.
- \_\_\_\_\_ (1997) 'Contemptus Mundi and Carpe Diem Motifs in Kezilahabi's Works.'  
Katika Kiswahili. Juzuu 60. Dar-es-Salaam.
- Warnock, M. (1970) Existentialism  
Oxford University Press, London.
- Webb, E. (1972) The Dark Dove: The Sacred and Secular in Modern Literature  
Seattle, University of Washington Press Washington D C.
- Williams, R. (1966) Modern Tragedy  
Chatto & Windus Ltd., London.
- William, H. & Levey, J. S (Wahariri) (1975) The New Columbia Encyclopaedia.  
Columbia University Press, New York.
- Wilson, E. na Goldfarb, A. (1991) Theatre the Lively Art  
McGraw-Hill, Inc. New York.